KUCHUNGUZA DHAMIRA NA FANI KATIKA NYIMBO ZA TAARAB ASILIA: MIFANO YA NYIMBO ZA SHAKILA SAIDI KHAMISI

ASHA RASHID ABDALLA

TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNIKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M. A. KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2018

UTHIBITISHO

Alieweka saini hapo chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa: "**Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo za Taarab Asilia: Mifano ya Nyimbo za Shakila Saidi Khamisi"** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa Shahada ya uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

_____

Dkt. Mohammedi Omary Maguo

(Msimamizi)

_____

Tarehe

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kuzalisha au kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii bila kibali cha maandishi kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, isipokuwa kwa shughuli halali, kama vile kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma.

TAMKO

Mimi, **Asha Rashid Abdalla,** ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe, na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada ya uzamili au shahada nyengine yoyote.

_____

Saini

_____

Tarehe

TABARUKU

Tasnifu hii ni hidaya maalumu kwa wazazi wangu Bi Suria Said Hassan na Bwana Rashid Abdalla Khamis kwa kunilea na kunisomesha kwa juhudi zao kubwa hadi wakaniweka katika mwanga wenye virutubisho. Sina cha kuwalipa ila nawaombea dua kwa Mwenyezi Mungu (S.W) awape wepesi katika maisha ya dunia na akhera. Pia kwa mume wangu kipenzi Bwana Masoud Fadhil Saleh kwa kuniwezesha kihali na mali kuikamilisha kazi hii huku akiwa na subra ya hali ya juu na kuniridhia kutumia hata muda wake katika kulifanikisha hili. Allah (S.W) amlipe kheri. Vile vile kwa mama mkwe wangu kwa kunistahamilia wakati alipokosa huduma stahiki, na mwisho kwa watoto wangu Humud Masoud Fadhil, Tamir Masoud Fadhil na Rumaiswaa Masoud Fadhil kwa kuwa watulivu na wasikivu walipokuwa na upweke wa kukosa huduma na penzi la dhati kutoka kwa mama yao. Mungu awakuze kiujasiri na kuwapa elimu yenye manufaa.

SHUKURANI

Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa kunijaalia uhai, uzima na ufahamu wa mambo katika kipindi chote cha masomo yangu. Hivyo nasema Alhamdullillah.

Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu wa tasnifu hii Dkt. Mohammedi Omary Maguo kwa kuniongoza vyema katika kila hatua hadi utafiti huu kukamilika. Msaada wake haulipiki kwa thamani yoyote ila nasema ahsante. Allah (S.W) ambariki na amjaalie maisha marefu yenye tija duniani na akhera.

Tatu, napenda kutoa shukurani kwa wahadhiri wangu wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, kwa msaada wao wa kunijenga kiujasiri na kitaaluma. Nawashukuru kwa kunipa elimu yao bila kuwa na choyo cha aina yoyote. Wahadhiri hao ni pamoja na Prof. Sengo, Prof. Mbogo, Dkt. Hilda Pembe, Dkt Khadija Jilala na Dkt Zelda Elisifa. Mungu awanyanyulie daraja zao na awazidishie imani za kutulea na kutusaidia kitaaluma.

Nne, napenda kutoa shukurani zangu zenye uzito wa pekee kwa Mwalimu Bakar Kombo Bakar kwa kunisaidia kutatua changamoto, kunifuta machozi yaliyotiririka nilipokumbwa na vikwazo vya safari ya kimasomo, kunipa moyo na kunionesha njia ya kupita ili safari hii ikamilike salama. Kwa ufupi namuomba Allah (S.W) ampe neema za ziada.

Pia, napenda kutoa shukurani maalumu kwa Bw. Khamis Hamad; Mwandishi mpiga picha wa Kampuni ya Ukombozi Uni Ltd, kwa kutoa ushirikiano wa dhati kabisa katika kukamilisha tasnifu hii.

Vile vile, napenda kutoa shukurani za dhati kwa walimu wangu wapenzi Bi Fatma Hamad Rajab na Mwalim Sharif Juma Fakih kwa msaada wao mkubwa. Nawashukuru kwa ustahamilivu wao walionionesha wakati wote ambao nilihitaji msaada kutoka kwao hata ikiwa ni muda wao wa mapunziko. Kwa hakika walinijali sana. Malipo yao nawaombea kwa Allah awazidishie imani na awaongoe zaidi katika kheri ili kuwe na kila sababu ya kawalipa pepo yenye kupita mito chini yake na wakae humo milele, Amin. Na kwa wote niliowataja na nisiowaataja nawaombea kwa Allah neema nyingi zenye manufaa kwao.

IKISIRI

Lengo la utafiti huu ni Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo za Taarab asilia za Shakila Saidi Khamisi. Ili kukamilisha lengo hili, utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi mawili ambayo ni (i) Kuchambua dhamira katika nyimbo teule za Shakila Saidi Khamisi na (ii) Kubainisha mbinu za kisanaa zinazojitokeza katika nyimbo teule za Shakila Saidi Khamisi. Data za utafiti huu zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na upitiaji wa nyaraka maktabani. Utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaelezo. Hoja zilijengwa na kujengewa misingi imara ya kinadharia. Nadharia iliyotumika katika uchambuzi wa data ni zile za Mwitiko wa Msomaji na Simiotiki. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa kuna dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika nyimbo za taarab asilia za Shakila Saidi, miongoni mwa dhamira hizo ni pamoja na zile zinazohusiana na mapenzi, utamaduni, usaliti, dini na imani, elimu, ukweli na uwazi, ukombozi, umalaya na dhamira nyenginezo. Pia utafiti huu umebaini mbinu za kisanaa zilizomo katika nyimbo za taarab asilia za Shakila Saidi. Miongoni mwa mbinu hizo za kisanaa ni tamathali za semi kama vile kejeli, tashtiti, majazi, taswira na ishara, sala, takriri na nyenginezo. Vile vile utafiti umegundua kuwa msanii Shakila Saidi alibobea sana katika matumizi ya mbinu za kisanaa na kanuni za kimapokeo jambo ambalo lilirahisisha ujengaji wa dhamira za nyimbo zake.

YALIYOMO

UTHIBITISHO ..... **ii**

HAKIMILIKI ..... **iii**

TAMKO ..... **iv**

TABARUKU ..... **v**

SHUKURANI ..... **vi**

IKISIRI ..... **viii**

SURA YA KWANZA **1**

1.0 UTANGULIZI **1**

1.1 Usuli wa Mada 1

1.2 Usuli wa Bi Shakila Saidi Khamisi 4

1.3 Tatizo la Utafiti 7

1.4 Malengo ya Utafiti 9

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti 9

1.4.2 Malengo Mahsusi 9

1.5 Maswali ya Utafiti 9

1.6 Umuhimu wa Utafiti 9

1.7 Mawanda ya Utafiti 10

1.7 Muundo wa Tasnifu 11

SURA YA PILI **12**

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MIKABALA YA KINADHARIA **12**

2.1 Utangulizi 12

2.2 Ufafanuzi wa Istilahi 12

2.2.1 Taarab 13
2.2.2 Wimbo 13
2.2.3 Dhamira 16
2.3 Tafiti Tangulizi Kuhusu Nyimbo za Taarab 17
2.4 Mkabala wa Kinadharia 21
2.4.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji 22
2.4.2 Nadharia ya Simiotiki 24
2.5 Hitimisho 26
SURA YA TATU 27
3.0 MBINU ZA UTAFITI 27
3.1 Utangulizi 27
3.2 Eneo la Utafiti 27
3.3 Usanifu wa Utafiti 28
3.4 Kundi Lengwa 28
3.5 Sampuli na Usamplishaji 29
3.6 Data za Utafiti 30
3.6.1 Data za Msingi 30
3.6.2 Data za Upili 30
3.7 Mbinu za Kukusanyia Data 31
3.7.1 Usomaji Makini 31
3.7.2 Upitiaji wa Nyaraka 32
3.8 Uchambuzi wa Data za Utafiti 32
3.9 Hitimisho 33

SURA YA NNE..... 34

4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTAFITI ... 34

4.1 Utangulizi..... 34

4.2 Utafiti na Malengo Yake..... 34

4.2.1 Dhamira zilizojitokeza katika Nyimbo za Taarab Asilia za Shakila Saidi 34

4.2.2 Dhamira ya Tanzia (Ukiwa)..... 69

4.3 Mbinu za Kisanaa zinazojitokeza katika Nyimbo za Shakila Saidi Khamisi 101

4.3.1 Matumizi ya Kejeli..... 102

4.3.2 Matumizi ya Tashtiti 104

4.3.3 Matumizi ya Methali 107

4.3.4 Matumizi ya Majazi 109

4.3.5 Matumizi ya Takriri 110

4.3.6 Matumizi ya Taswira/Ishara..... 114

4.3.7 Matumizi ya Sala..... 117

4.3.8 Matumizi ya Misimu 121

4.3.9 Matumizi ya Uhamishaji wa Ndimi 123

4.3.11 Mbinu ya Mshonano wa Mawazo (Muundo)..... 129

4.4 Hitimisho..... 131

SURA YA TANO 133

5.0 HITIMISHI, MUHUTASARI NA MAPENDEKEZO 133

5.1 Utangulizi..... 133

5.2 Hitimisho..... 133

5.3 Muhutasari wa Tasnifu..... 133

5.4 Mapendekezo ya Utafiti 134

5.4.1 Mapendekezo ya Kitaaluma 134

5.4.2 Mapendekezo ya Kijamii 135

5.4.3 Mapendekezo kwa Tafiti zijazo 135

5.4.4 Mapendekezo kwa Wasanii 135

5.4.5 Mapendekezo kwa Serikali 136

5.4.6 Mapendekezo kwa Vyombo vya Habari 136

5.5 Hitimisho la Sura ya Tano 136

MAREJELEO 137

VIAMBATANISHO 141

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Wataalamu mbalimbali wamejitahidi kuzungumzia suala la taarab asilia pamoja na historia ya kuibuka kwake. Miongoni mwa wataalamu hao ni Makilla (2011:11) ambae anaeleza kuwa taarab asilia si muziki wa kucheza bali ni wa kutazama, kusikiliza, kutafakari na kutunza. Ni muziki ambao nyimbo zake hutungwa kwa kutumia lugha ya mafumbo, mvuto na mnato ambao hauzuwii familia kwa mfano baba, mama na watoto kuzitazama au kuzisikiliza wakati wakiwa pamoja. Huu ni muziki unaotumia ala kama vile filda, dumbaki, ganuni, kinanda na dabalibesi ambazo hutoa muziki mororo unaofanya msikilizaji au mtazamaji atikise kichwa na kuchezesha vidole pole pole.

Historia inaonesha kwamba taarab asilia ilibisha hodi ndani ya visiwa vya Zanzibar mnamo mwaka 1870 kutokea katika nchi za Arabuni. Umaarufu wake ulikuwa ni katika sehemu maalumu za kuwastarehesha viongozi/watawala ambao wengi wao walikuwa na asili ya Kiarabu. Jambo hili lilipelekea nyimbo hizo ziimbwe kwa lugha ya Kiarabu. Waimbaji na vifaa vililetwa Zanzibar kutoka Arabuni, hasa kutoka nchi za Yemen na Misri. Neno taarab lina asili ya Kiarabu lenye maana ya raha, starehe na furaha (Yego, 2011).

Nyimbo za taarab zilianza kuimbwa kwa lugha ya Kiswahili kwenye miaka ya 1990. Vipaji vya Wazanzibari vimepelekea uasili mpya wa taarab asilia na leo hii baadhi ya wataalamu wanadiriki hata kuandika kuwa, asili ya taarab ni Uswahilini na makao

makuu yake ni Zanzibar. Kwa mfano Mgana (1996:125) anafafanua kuwa “Zanzibar ndicho kisiwa kilichodaiwa kuwa muziki wa taarab ndipo ulipoanzia miaka 100 iliyopita na ndio makao makuu ya muziki huo”.

Taarab asilia iliingia visiwani Zanzibar ikiwa na lengo kuu la kumpatia burudani mfalme wa wakati huo Sayyid Said Bin Sultan na waandamizi wake, pale alipohitaji raha na starehe ya kupumzisha akili yake wakati wa jioni na usiku. Pia maendeleo makubwa ambayo mtawala huyu alikwishayafikia kiasi ambacho hakuwa na shida yoyote. Alitamani zaidi burudani, starehe na anasa. Haya yanathibitishwa na Sheikh Shaib alienukuliwa na Khatib (1992) akisema, Sayyid Said alikuwa mtu wa anasa na starehe na alikuwa hawezi kuishi bila ya kupata muziki wa taarab, hivyo yeye ndiye aliyeanzisha muziki wa taarab Zanzibar na baadae ukaanza kusambaa hadi kufika Tanganyika. Miongoni mwa viashiria vya ukomavu wa taarab asilia Zanzibar ni uanzishaji wa vikundi vingi ambavyo vilivuma na kuwa na uwezo mkubwa katika ulimwengu wa taarab..Vikundi vyenyewe ni pamoja na Naad Ikhwan Swafaa (1905) pamoja na Nadi Suub (1908). Kadri siku zilivyosonga, vikundi vingine vya taarab vilianza kuchipuka. (Mgana, 1991; Farhan, 1992 na Khatib, 1992:27) wanaelezea kwamba, mnamo mwaka 1945 kuliibuka vikundi vya wanawake pekee, mfano wa vikundi hivyo ni kama vile Royal Airforce, Navy, Nurul –Uyuni, Sahib el- An na Banati el kher. Vile vile, kuna vikundi vingine vilikuwa na mchanganyiko wa wanawake na wanaume, kwa mfano, Michenzani Social Club (1954), Kwaalimsha Social Club, Miembeni Club (1957), Yaasu Social Club (1960), Ghazy (1961), Kiembe Samaki Musical Club (1963). Pia vikundi kama vile Culture Musical Club (1965), Sabran Jamil (1985), vikundi vya majeshi (1985), Ilyas na Twinkling Star na

Bwawani (1989). Waimbaji mashuhuri kwa wakati huo walikuwa ni Siti Binti Saad, Mbarouk Suwed, Bakari Abedi, Maalim Shaaban na wengineo (Rajab, 2016).

Baada ya muziki wa taarab kusambaa kwa kiasi kikubwa ulivuka mipaka ya visiwa na kuingia Tanzania Bara katika sehemu za Dar es Salaam, Bagamoyo hadi Tanga ambapo muimbaji Shakila Said alizaliwa. Pia muziki huu ulisafiri na kuvuka mipaka ya nchi na kuvuma sana sehemu za Lamu na Mombasa nchini Kenya. Aidha muziki wa taarab uliweka maskani yake katika mataifa mbalimbali ikiwemo Uganda, Rwanda na Burundi.

Wanafasihi waliowahi kufanya tafiti zinazohusu nyimbo za aina mbalimbali zikiwemo za taarab asilia ni wengi kiasi kwamba haitokuwa rahisi kwa mtafiti kuwataja wote katika utafiti huu. Miongoni mwa watafiti hao ni, Mgana (1991) aliyeandika kuhusu Jukwaa la taarab Zanzibar, Ameir (2007) aliyeandika kuhusu maadili yanayopatikana katika nyimbo za ukungwi za Zanzibar, Mzee (2011) aliyechunguza athari za nyimbo za mipasho katika jamii ya Wazanzibari, Yego (2011) aliyeandika kuhusu nafasi ya mwanamke jinsi inavyotetewa katika nyimbo za taarab Zanzibar, Khamis (2012) aliyechunguza matumizi ya mafumbo na taaswira katika nyimbo za mapenzi za taarab asilia Zanzibar, Fair (2013) alichunguza historia ya jamii ya Zanzibar na nyimbo za Siti Binti Saad, na Mbwana (2016) alietathmini mabadiliko ya matumizi ya nyimbo za harusi za kipemba kwenda katika kasida za harusi. Wengine walioandikia eneo hili ni Wazir (2016) aliyechunguza dhima ya nyimbo za singo katika kijiji cha Uzini Zanzibari na Rajab (2016) aliyechunguza chanjo ya mapenzi katika nyimbo za taarab asilia za Seif Salim. Watafiti hawa

wamefanya kazi nzuri na kubwa sana katika uwanja huu wa fasihi kwenye nyimbo za aina mbalimbali hasa za taarab na hasa zile za Zanzibar. Hata hivyo watafiti hawa hawakuangazia dhamira na fani katika nyimbo za Shakila zilizoteuliwana mtafiti wa kazi hii. Mtafiti wa kazi hii ameona kwamba ni muhimu sana kwa jamii ya Waswahili wa Afrika Mashariki kulielewa hilo. Pia ni sehemu ya kumuenzi msanii huyu ambaye ameshafariki katika mwaka 2016 hivyo utafiti katika eneo hili unahitajika.

1.2 Usuli wa Bi Shakila Saidi Khamisi

Shakila binti Saidi ambaye alihusika moja kwa moja na utafiti huu alizaliwa mwaka 1949, Pangani mkoani Tanga. Mnamo mwaka 1953, Shakila alianza kusoma elimu ya kur-ani katika madrasa ya mwalimu Awadhi. Kutokana na hamu na bidii kubwa aliyokuwanayo Shakila, alihitimu juzuu kadhaa kwa muda mfupi. Pia alikuwa msomaji mzuri wa qaswida jambo ambalo liliibua kipaji chake cha uimbaji wa taarab ambacho kilichochewa na uwezo wake wa kughani na kutunga nyimbo zake mwenyewe. Miaka mitatu baadae Bi Shakila alianza kusoma elimu ya msingi katika shule ya Kimba huko Pangani na alikuwa mwanafunzi hodari mwenye nidhamu ya hali ya juu. Mwaka 1958, Bi Shakila akiwa ni mwanafunzi wa darasa la tatu katika shule yake hiyo alipata bahati ya kushiriki katika ngoma ya msanja iliyotayarishwa kwa ajili ya kumburudisha kingozi mkuu wa TANU; marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipotembelea shuleni hapo. Katika tukio hilo lililohudhuriwa na viongozi mbalimbali, Bi Shakila aliimba bila khofu na kwa kujiamini kiasi kwamba kila mtu alieshuhudia aligundua kipaji chake na wengi wao walishindwa kujizuia. Wapo walioshangilia, wapo waliomtunza na kucheza hadi alidhaniwa kuwa

angekuwa manju wa msanja lakini mambo yalikuwa tafauti kwani alikuwa manju wa taarab asilia.

Katika masuala ya ndoa, Bi Shakila aliwahi kuolewa na waume wanne na kubahatika kupata watoto kumi na mbili (12). Kwa mara ya kwanza, Bi Shakila aliolewa mwaka 1960 akiwa na umri wa miaka 11 na mwanamume alieitwa Ayoub Kombo ambaye alizaa naye mtoto mmoja ndani ya mwaka 1961. Mtoto huyo alijulikana kwa jina la Wazir. Mume huyu hakuishi nae muda mrefu kwa sababu hakuwa chaguo lake. Mnamo mwaka 1968 aliolewa na mume mwengine alieitwa Khatibu Akida ambae alikuwa mutrib wa taarab na ndie aliemuhamasisha zaidi Bi Shakila kukuza kipaji chake cha utunzi na uimbaji. Bwana huyu alizaa nae watoto wanne, mmoja wa kiume na watatu wanawake. Mtoto wa kiume alizaliwa mwaka 1969 na alijulikana kwa jina la Salum. Watoto wa kike walikuwa ni Luckstar aliyezaliwa mwaka 1972, Mwanahawa aliyezaliwa mwaka 1974 na Mwanaate aliyezaliwa mwaka 1976. Mume wa tatu wa Bi Shakila aliitwa Kibwana Saleh Mkali alieishi nae kwa muda wa miaka minane na kuzaa nae watoto wane; mmoja mwanamme alieitwa Rashid ambaye kazaliwa mwaka 1978. Watoto watatu aliowazaa na mzee Kibwana walikuwa wanawake ambao ni Bijaa aliyezaliwa 1980, Khadija aliyezaliwa 1983 na Mape aliyezaliwa 1986. Bi shakila aliachana na bwana huyu kutokana na wivu wake. Kibwana hakupenda mkewe awe muimbaji. Mume wanne wa Bi Shakila alikuwa ni Bwana Sadoo Amiri, aliezaa nae watoto watatu. Mmoja kati yao alikuwa wa kiume. Kijana huyu aliyezaliwa mwaka1988 aliitwa Bachu., Wawili walikuwa ni wanawake ambao ni Mgeni aliyezaliwa mwaka 1990 na Shani ambae alikuwa ndie kitinda mimba wa Bi Shakila alizaliwa mwaka 1994.

Katika watoto hawa 12 wa bi Shakila, Luckystar alifariki akiwa na umri mdogo. Kati ya watoto 11 waliobakia kuwa hai ni wawili tu ambao ni Khadija na Mape waliorithi kipaji cha uimbaji kutoka kwa mama yao Bi Shakila na wanaimba katika kikundi cha Modern taraab (Mahojiano ya Starehe [mwandishi wa habari wa gazeti la nipashe] na Shakila, 2016).

Katika uimbaji, Bi Shakila aliibuka na kipaji cha utunzi na uimbaji tangu utotoni mwake kupitia katika michezo ya watoto. Kwa kipaji hicho alidai kuvutiwa sana na sauti ya Ummukulthum aliekuwa muimbaji wa Misri na marehemu Siti binti Saad aliekuwa muimbaji wa zamani wa taarab Zanzibar. Hao miongoni mwa waliomshawishi zaidi kuingia katika uimbaji wa taarab. Msanii huyu alianza kuimba akiwa na umri mdogo sana kwani ni mwaka mmoja tu baada ya kuolewa na alijiunga na kikundi chake cha kwanza kilichoitwa *Young Novelty* mnamo mwaka 1961. Katika kikundi hiki Shakila aliimba wimbo wa kwanza ulioitungwa na Mutrib wa kikundi hicho bwana Ndorobo Salehe. Wimbo huo ulijulikana kwa jina la “Ulikuwa ghali sana”. (1961) na aliuimba kwenye sherehe za harusi, pia huu ndio uliokuwa wimbo wa kwanza wa taarab za Waafrika katika shughuli za harusi. Mnamo mwaka 1962, Bi.Shakila alijiunga na kikundi cha taraab cha Black Star chini ya uongozi wa Mutribu, Khatib Akida akiwa pia ni mume wake wa wakati huo. Katika mwaka 1970 kilianzishwa kikundi chengine cha taraab kilichoitwa Lucky Star kikiwa na makao makuu yake barabara ya 13 Mjini Tanga, Bi. Shakila na mumewe pamoja na watribu wengine kutoka Black Star walijiunga na kikundi hicho kilichofadhiliwa na Bw. Nassor Saidi. Bi. Shakila alifanyakazi na kikundi cha bend cha JKT kwa zaidi ya miaka 30 kutoka mwaka 1985 hadi kufariki kwake, ambapo aliimba nyimbo zenye

dhamira mbali mbali zikiwemo za kimapenzi, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa. Kabla ya kufariki kwake mwishoni mwa mwaka 2016. Miongoni mwa nyimbo za msanii Shakila ni pamoja na: Pazia, hujui alacho kuku, aloanza pekepeke, mapenzi ni kama donda, nimezama kwa mapenzi, mpenzi unisamehe, kuku na yai, mkuna na mkunwaji, oh! Rabbi, Viva Frelimo n.k. Na baada ya kustaafu katika kikundi cha JKT msanii alidai kuwa tayari alikwishaanzisha kikundi chake binafsi kilichojulikana kwa jina la *Mama na mwana* ambacho kilikuwa kikimilikiwa ni yeye na mtoto wake (Starehe 2016).

Bi Shakila ana mchango mkubwa katika utamaduni wa Mswahili kwani alionesha uzalendo wa hali ya juu katika matumizi ya Kiswahili fasaha kwenye nyimbo zake, tafauti na wasanii wengine kama vile wa nyimbo za mipasho na bongo fleva wanaochanganya lugha Omari (2006). Pia, Bi Shakila hutumia jukwaa kwa kuangalia na kuzingatia maadili, mila na desturi ya jamii yake hali inayompelekea kutumia mafumbo ili kuepuka lugha ya matusi. Sambamba na hilo msanii huyu alichukua nafasi ya kuendeleza muziki huu wa taarab asilia katika pwani ya Afrika Mashariki ikiwa ni sehemu ya utamaduni ya wakaazi wa sehemu hizo. Kwa hivyo mchango wa msanii huyu kwa nchi za Waswahili na wasiokuwa Waswahili ni mkubwa, kwa upande wa utamaduni na nyanja nyengine za maisha hivyo anafaa kuenziwa ili kuendeleza mchango huo kwa kizazi kilichopo na kijacho.

1.3 Tatizo la Utafiti

Katika usuli wa mada zimebainishwa tafiti nyingi zilizozungumzia nyimbo za aina mbalimbali zikiwemo nyimbo za taarab asilia. Mfano wa tafiti hizo ni ile ya Mlama

(1996) aliyeangalia baadhi ya sanaa za maonyesho na kugundua kwamba katika sanaa, watu hupiga ngoma, huimba, hughani mashairi na kucheza.

Mzee (2013) alichunguza “Nafasi ya maudhui katika nyimbo za taarab za Bi. Shakila zinavyosawiri hali halisi katika jamii”. Mbwana (2016) alitathmini mabadiliko ya matumizi ya nyimbo za harusi za Kipemba kwenda katika kasida za harusi. Matokeo ya tathmini hii ni kwamba nyimbo na kasida za harusi za Kipemba zina mfanano uliosababishwa na mazingira, utamaduni na shughuli za kikazi zinazofanywa Uswahilini.

Mzee (2016) alichunguza dhima ya nyimbo za singo katika kijiji cha Uzini. Matokeo ya utafiti huo yameonyesha nyimbo za singo zina dhima kubwa ya nyimbo ya kuendeleza utamaduni wa watu wa Uzini na zinatoa mafunzo maalumu kwa maisha ya wanandoa. Rajab (2016) aliyechunguza chanjo za kimapenzi katika nyimbo za taarab asilia za Seif Salim aligundua kwamba chanjo zote za kimapenzi katika nyimbo za msanii huyo, zimetawaliwa na maneno yenye michomo mikali na hisia za wazi za kimapenzi.

Licha ya kuwepo tafiti nyingi zilizokwishafanywa zikiwemo zile zinazohusu nyimbo za Shakila kwa jamii ya Waswahili wa Afrika Mashariki lakini hakuna utafiti ulioangazia dhamira na fani katika nyimbo za Shakila. Hivyo mtafiti huyu ameona ipo haja ya kufanya uchunguzi katika eneo hili la dhamira na fani katika nyimbo za Shakila ili kuziba pengo lililopo.

1.4 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yamegawanyika katika sehemu mbili kuu, ambazo ni: Lengo kuu na lengo mahsusi.

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo za taarab asilia: Mifano ya nyimbo za Shakila Saidi.

1.4.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahususi ya utafiti huu ni:-

i) Kuchambua dhamira katika nyimbo teule za Shakila Saidi

ii) Kubainisha mbinu za kisanaa zinazojitokeza katika nyimbo za Shakila Saidi.

1.5 Maswali ya Utafiti

Maswali ya utafiti huu ni haya yafuatayo:-

i) Ni dhamira gani zinazopatikana katika nyimbo za Shakila Saidi?

ii) Ni mbinu gani za kisanaa zinazojitokeza katika nyimbo za Shakila Saidi?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu mkumbwa katika maeneo mbalimbali.

Kwanza, kwa wanafasihi watautumia kama marejeleo ya kazi zao hasa pale utakapokuwa tayari umehifadhiwa maktaba. Pili utafiti huu utasaidia sana kunyanyua viwango vya ufahamu wa taaluma ya fasihi hasa katika utanzu huu wa ushairi (nyimbo) kwa walimu na wanafunzi wa shule za sekondari, Vyuo vya ualimu na Vyuo vikuu. Tatu, utafiti huu utakuwa kichocheo chema cha kuamsha ari na kujaza

hamu na raghba kwa watafiti chipukizi kufanya tafiti zaidi katika eneo la fasihi, hasa kwenye eneo la nyimbo za waimbaji mbalimbali wa taarab.

Vile vile utafiti huu utawaonyesha mwanga walio na nia na shauku ya kuandika vitabu vinavyohusu historia, fani na dhamira ya nyimbo mbalimbali za taarab asilia hasa katika usanii wa Shakila binti Said na waimbaji wengine wa ukanda wa Afrika Mashariki.

Aidha, utafiti huu utasaidia katika kuhifadhi na kurithisha utamaduni wa jamii za kiafrika uliokolezwa ndani ya nyimbo za Shakila Saidi.

1.7 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu umejishugulisha na uchunguzi wa dhamira na fani katika nyimbo za taarab asilia, uchunguzi huo ulijikita moja kwa moja katika nyimbo za taarab za muimbaji maarufu wa mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki Bi. Shakila bint Said. Utafiti huu haukuhusika kamwe na uchunguzi wa nyimbo zote za Shakila bali ulijihusisha na uchambuzi wa dhamira na fani katika nyimbo 15 za msanii huyu. Pia katika utafiti huu kimaudhui mtafiti aliangalia dhamira za nyimbo hizo kiuchumi, kimapenzi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Kifani utafiti huu ulitupia jicho katika mbinu za kisanaa alizotumia msanii katika utunzi na uwasilishaji wa nyimbo zake. Miongoni mwa mbinu hizo za kisanaa ni pamoja na mbinu ya kejeli, mbinu ya tashtiti, mbinu ya majazi, mbinu ya taswira na ishara, mbinu ya sala, mbinu ya takriri na mbinu nyenginezo za kisanii.

1.7 Muundo wa Tasnifu

Utafiti huu una sura tano. Sura ya kwanza imehusu utangulizi juu ya taarab asilia, usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, na mpangilio wa utafiti. Sura ya pili imehusu mapitio ya kazi tangulizi na mikabala ya Kinadharia ambayo imemuongoza mtafiti kufanya kazi hii. Sura ya tatu imeelezea mbinu za utafiti, eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za kukusanya data, mbinu za uchambuzi wa data, usahihi wa data za utafiti, maadili ya utafiti na hitimisho. Wakati sura ya nne imezungumzia uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti. Na sura ya tano imetoa muhutasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo.

SURA YA PILI

2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MIKABALA YA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii imehusisha mapitio ya machapisho na kazi tangulizi mbalimbali zinazozungumzia mada inayofanana au kukaribiana na mada iliyofanyiwa utafiti. Sura hii pia imebainisha nadharia zilizotumika katika kukamilisha utafiti huu. Mtafiti alipokuwa akisoma nyaraka, machapisho na kazi tangulizi mbalimbali alizingatia mambo muhimu na ya msingi yaliyosaidia kuongeza maarifa ya kukamilisha lengo la utafiti huu kwa usalama na kwa ufanisi zaidi. Mambo ambayo mtafiti aliyatupia jicho kwa umakini kabisa ni pamoja na dhana ya taarab asilia, maana ya nyimbo, aina za nyimbo, dhima za nyimbo na maana ya dhamira.

Baada ya kazi kubwa ya upitiaji wa kazi tangulizi, nyaraka na machapisho maarifa ya mtafiti yalitanuka kwa kiwango cha juu kabisa. Enon (1998) anaelezea kuwa, kazi tangulizi ni maarifa yanayopatikana kwa kuzamia mbizi maandishi ya huko nyuma ambayo hufanikisha taarifa zinazopatikana ndani ya utafiti wa sasa. Vile vile baada ya usomaji wa maandishi ya watafiti watangulizi, mtafiti alipata maarifa juu ya maeneo ambayo yameshaandikiwa na kujiepusha na urejeaji usio wa lazima, pia alipata mwanga uliomsaidia kuwasilisha kazi yake ya utafiti kwa utaratibu unaopendeza na kupata maarifa juu ya nadharia zinazowiana na mada yake.

2.2 Ufafanuzi wa Istilahi

Katika sura hii mtafiti alifafanua istilahi mbalimbali ambazo zilitoa dira katika utafiti wake. Istilahi zilizofafanuliwa ni dhana ya taarab, wimbo na dhamira. Ufafanuzi huu

ulikuwa na malengo ya kumfanya msomaji wa utafiti huu kuelewa kwa urahisi kilichokusudiwa na kupata msaada atakaouhitaji kuhusiana na utafiti huu.

2.2.1 Taarab

Khamis (2005:133) anaeleza kuwa taarab ni neno la Kiarabu lililotokana na neno tariba, ambalo lina maana ya kujitikisa, kufurahi, kuimba na kupiga muziki kwa ajili ya kujifurahisha na kucheza. Makilla (2011:11) kwa upande wake anaeleza kuwa taarab asilia si muziki wa kucheza bali ni wa kutazama, kusikiliza, kutafakari na kutunza. Taarab ni muziki unaoleta furaha na kuondoa mawazo ili kuleta hisia zenye raha na anasa unaombatana na maneno ya kishairi yanayotumia ala za kimuziki (Rajab, 2016). Kwa hivyo, neno taarab kwa mujibu wa utafiti huu ni aina ya mchezo unaoambatana na muziki unaokwenda sambamba na wimbo ambao huingia ndani ya nyoyo za watazamaji.Wasikilizaji wa taarab hupata mihemko inayowafanya kushindwa kujizuia kudemkademka, kuifatafata nyimbo kwa kuitikia na hata kunyanyuka na kutunza na kupiga makofi kwa furaha na raha zilizowaenea ndani ya roho na viungo vyote. Mtafiti wa utafiti huu anaona kwamba taarab ni muziki wa Kiswahili unaochezwa hadhira ikiwa katika hali ya kukaa na muimbaji akiwa amesimama na kudemkademka kwa kuongozwa na muziki na wimbo anaouimba.

2.2.2 Wimbo

Mulokozi (1996:64) anaeleza kuwa nyimbo ni kile kinachoimbwa. Mambo muhimu yanayoutambulisha wimbo ni muziki wa sauti ya muimbaji au waimbaji, muziki wa ala (kama upo), matini au maneno yanayoimbwa, hadhira inayoimbiwa na muktadha uliofungamana na wimbo huo kwa mfano sherehe, ibada, kilimo, n.k. Wimbo ni

sanaa yenye dhima kubwa katika jamii za Kiafrika. Hutumika kwa kuburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko, kuonya, kufunza, kuarifu, kunogesha hadithi, kuombolezea, kubembelezea watoto ili walale, kuongeza hamasa katika kuchapakazi, n.k. Wamitila (2003) ana maoni kwamba, 'Nyimbo ni tungo yenye mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizo huundwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha na mapigo ya silabi. Hupangwa kwa utaratibu wenye muwala wenye mapigo ya kimuziki. Wamiltila (keshatajwa) aliendelea kufafanua kuwa wimbo ni utungo wa shairi au utungo mfupi ulioundwa kwa maneno yenye muziki na yanayoleta mvuto katika kuimbwa au uimbaji. Kwa mawazo ya Rajab (2016) nyimbo ni kijitanzu kidogo kilichomo ndani ya utanzu mkubwa wa ushairi ambao hupangwa kwa mpangilio maalum wenye kutumia maneno yanayoweza kulainisha mioyo ya watu na hutolewa kwa njia ya uimbaji ambao hutoa ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa. Kwa maana hizo za wataalamu mbali mbali kuhusu nyimbo mtafiti anapata mwanga na kuibuka na kusema kuwa nyimbo ni aina ya ushairi iliyojaa usanii ndani yake inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno fasaha na wenye muwala yenye kuleta taswira, ishara, picha na sitiari iwe katika usemi au maandishi ili kuleta wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisia fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayoibua hisia kwa wahusika.

2.2.2.1 Aina za Nyimbo

Wataalamu mbalimbali wameelezea na kugawanya aina za nyimbo kulingana na vigezo mbalimbali, kama vile mazingira na wakati. Mulokozi (2013) amezigawa nyimbo katika makundi ya nyimbo za kidini, nyimbo za kazi, nyimbo za taifa, nyimbo za kuwindia, nyimbo za watoto, nyimbo za jando, nyimbo za unyago na

nyimbo za harusi. Fenegan (1970) anafafanua kuwa, nyimbo zinaweza kutofautiana katika muundo, mtindo, maudhui na dhima. Hata hivyo ufanano mkubwa wa nyimbo ni matumizi yake hivyo tunaweza kuwa na nyimbo za siasa, nyimbo za watoto na nyimbo za kazi kama vile kilimo, uvuvi, ukwezi, ulinzi na uwindaji. Hivyo kulingana na maelezo na vigawanyo vya nyimbo vya wataalamu hao ni dhahiri kwamba zipo nyimbo za aina tofauti na kiashiria kikubwa kinachoonesha tafauti kati ya nyimbo moja na nyengine ni mazingira, wakati, wahusika na hata malengo ya nyimbo hiyo.

2.2.2.2 Dhima za Nyimbo

Dhima kubwa ya nyimbo katika jamii yoyote ile ni kuburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko, kuonya, kufunza, kuarifu, kunogesha hadithi, kuombolezea, kubembelezea watoto ili walale, na kuhamasisha watu wanaochapakazi. Pia tunaweza kusema kuwa dhima za nyimbo hutegemea mazingira, wakati na lengo la muimbaji. Kwa mfano Lucus (1975) anaelezea kuwa nyimbo za msanja na jando lengo lake kuu ni kutoa mafunzo, malezi na maadili mema yanayowasaidia wanajamii kujua namna ya kuishi. Seif (2011) anaelezea kuwa kila nyimbo zina dhima zake. Dhima kubwa ya nyimbo za unyago ni kumuandaa msichana kukabiliana na utu uzima ikiwa ni pamoja na matakwa na kanuni za ndoa. Sambamba na hilo Gibbe (1980) anadai kwamba jukumu kubwa la nyimbo za harusi ni kuwaelimisha wanandoa kuwa na maadili mema, unyenyekevu, utulivu, ustahamilivu, hekima na kuwa na adabu nzuri. Msokile anasisitiza kwa kusema kwamba nyimbo lazima zikubaliane na jamii na wakati katika kupokea ujumbe. Kwa hivyo mtafiti anakiri hayo kwani hata tunapoangalia dhima kuu ya nyimbo bembelezi ni kuwatuliza watoto na kuwafariji wazee wa watoto hao.

2.2.3 Dhamira

Senkoro (1982) amefafanua kuwa dhamira ni jumla ya mambo yanayojadiliwa katika kazi ya fasihi. Jilila (2016:189) anaelezea kuwa dhamira katika kazi ya fasihi ni zile zinazojitokeza kulingana na matokeo ya kijamii, wakati, mabadiliko ya kijamii na historia ya jamii.

Ndungo na Wafulla (1993) wanasema kwamba dhamira ni sehemu moja tu ya maudhui ya kazi ya fasihi. Hivyo dhamira ni kiini cha suala linalozungumzwa na mwandishi (msanii) katika kazi ya fasihi. Waandishi hawa wamezigawa dhamira katika makundi mawili nayo ni dhamira kuu na dhamira ndogo ndogo.

Msokile (1993:78) anasema, dhamira ni wazo kuu katika kazi ya fasihi. Pia ni mawazo mengine katika hiyo kazi ya sanaa itumiayo lugha.

Wamitila (2002: 53) anasema kwamba dhamira ni jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake.

Hivyo tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa dhamira ni jumla ya wazo/mawazo, kiini, makusudio, ambayo mwandishi au msanii amekusudia kufikisha kwa jamii husika. Dhamira hulenga katika nyanja zote za maisha ya wanaadamu, yaani kisiasa, kiuchumi, kijamii na hata kiutamaduni tofauti hujitokeza kulingana na kilichomfuma mwandishi kwa wakati huo kwani hakuna ulazima wa dhamira hizo kujitokeza kwa pamoja.

Dhamira huwepo kuu yaani kubwa ambazo hubeba wazo kuu la msanii na dhamira ndogondogo ambazo hutumika kujenga dhamira kuu.

2.3 Tafiti Tangulizi Kuhusu Nyimbo za Taarab

Mlama (1996) aliziangalia baadhi ya sanaa za maonyesho. Miongoni mwa sanaa alizoziangalia ni tambiko, miviga, ngoma, jando, unyago na majigambo. Mlama (keshatajwa) aligundua kwamba katika sanaa alizozichunguza watu hupiga ngoma, huimba, hughani mashairi na kucheza. Mlama hakugusia kabisa kuhusiana na taaabu asilia, hata hivyo kazi yake imemuongezea mtafiti mbinu za kutambua na kuona ni kwa namna gani sanaa hizo alizoziangalia zimeleta mabadiliko katika jamii. Kazi kuu ya mtafiti wa kazi hii ni kuchunguza dhamira na fani katika nyimbo za Shakila Said.

Khamis (1999) aliandika kuhusu nafasi ya utandawazi ndani ya sanaa ya taarab. Matokeo ya utafiti alioufanya ni kwamba, taarab ya Waswahili tayari imeiga baadhi ya mitindo kutokana na athari za utandawazi. Mfano, upigaji, uimbaji wa kushuka na kupanda kwa sauti. Pia amegundua mabadiliko katika vifaa vya muziki kama vile ala. Rayya, (2002) amechunguza mitindo katika nyimbo za harusi za wanawake wa Mombasa. Alichokigundua katika nyimbo hizo ni kuwa utanzu wa nyimbo ni utanzu muhimu katika maisha ya kila siku ya jamii. Hii ni kweli kwa sababu kama ilivyo aina nyengine ya tanzu za fasihi nyimbo zinakwenda na wakati na mazingira ya jamii husika. Kwa mfano, nyimbo huimbwa wakati mtoto anapozaliwa, katika utoto wake huimbiwa, katika ujana pia huimbiwa, Huimbiwa pia wakati wa kupata ukubwa na

pia katika wakati wa ndoa. Kazi ya Rayya (keshatajwa) ina uzito mkubwa na imesaidia kutoa mwanga kwa mtafiti katika kuzihakiki nyimbo za taarab asilia.

Ameir (2007) alichunguza maadili yanayopatikana katika nyimbo za ukungwi za Zanzibar. Katika kazi yake aligundua kwamba nyimbo hizo zinatoa mafunzo makubwa ya maadili katika maisha ya ndoa na maisha ya kawaida. Utafiti wa Ameir ulimsadia mtafiti wa kazi hii kuona mafunzo ya kimaadili yanayopatikana katika nyimbo za Shakila kama zilivyo nyimbo za ukungwi. Pia kazi ya Ameir imekuwa ni kama mwenge uliomuongoza mtafiti juu ya namna ya kuchambua dhima mbalimbali zinazojitokeza katika nyimbo za taarab asilia za Shakila Said. Samweli (2010/2011) alichunguza mapenzi katika nyimbo za Bongo Fleva. Matokeo ya uchunguzi wake ni kuwa, ingawa mapenzi yanazungumzwa katika nyimbo za Bongo Fleva lakini pia wasanii wa fani hii, wanazungumzia kuhusu matabaka, siasa, ufisadi, ubaguzi na unyonyaji.

Mzee (2011) aliandika kuhusu athari za nyimbo za mipasho katika jamii ya Wazanzibari. Mzee aligundua kwamba mara nyingi nyimbo za mipasho huitoa hadhira katika malengo na kufikia mwisho usiotarajiwa. Katika nyimbo za mipasho watu huanza kuotezana vidole na wakati mwengine huishia kupigana. Pamoja na kwamba Mzee hakujadili masuala ya taarab asilia lakini kimaudhui kazi yake imemsaidia mtafiti wa kazi hii kuhakiki dhamira za kiutamaduni katika mwendelezo wa kazi yake. Yego (2011) alichunguza nafasi ya mwanamke jinsi inavyotetewa katika nyimbo za taarab za Zanzibar. Yego (keshatajwa) alifanya uchunguzi wa jambo hilo katika nyimbo mbili tu nazo ni “Kibiriti upele” na “Tupendane Wabaya

waulizane". Katika utafiti wake aligundua kwamba mwanamke wa Kizanzibari kwa namna alivyochorwa katika nyimbo hizo anatafsirika kwamba bado yuko katika hali isiyoridhisha pamoja na utetezi mkubwa wa nyimbo za taarab. Hivyo mtafiti ameona ipo haja ya kuangalia mchango wa nyimbo za Shakila kuhusu dhima mbalimbali zikiwemo hizo za uchumi na utamaduni.

Khamis (2012) alichunguza kuhusu matumizi ya mafumbo na taaswira katika nyimbo za mapenzi zaTaarab asilia Zanzibar. Katika utafiti wake aligundua kuwa ni kweli nyimbo za mapenzi za taarab asilia za Zanzibar hutumia taswira nyingi wakati wa kufikisha maudhui kwa jamii. Amebaini taswira kama za kuonekana, kuonja na zile za namna. Fair (2013) ameandika kuhusu historia ya Jamii ya Zanzibar na nyimbo za Siti binti Saad. Utafiti wake umechambua vipengele kama vile, taarab na ubunifu mwengine unaopatikana Zanzibar. Kazi yake imemsaidia mtafiti kupata mwanga wa kutosha kuhusu historia ya taarab Zanzibar hasa kwa vile ni eneo ambalo mtafiti amelifanyia kazi katika kukamilisha utafiti huu. Mzee (2013) alichunguza "Nafasi ya maudhui katika nyimbo za taarab za Bi.Shakila zinavyosawiri hali halisi katika jamii". Utafiti wa Mzee umemsaidia mtafiti kupata maarifa ya ziada katika uchambuzi wa nyimbo za Shakila. Utafiti wa Fatma kwa upande mwengine umemsaidia mtafiti wa kazi hii kugundua pengo la utafiti ambalo mtafiti wa kazi hii ndilo aliloamua kulifanyia kazi.

Rajab (2016) alijihusisha na uchunguzi kuhusu Chanjo za Kimapenzi katika nyimbo za taarab asilia za Seif Salim. Rajab (keshatajwa) aligunduwa kwamba, chanjo zote za kimapenzi katika nyimbo za msanii huyo, zimetawaliwa na maneno yenye

michomo mikali na hisia za nje nje za kimapenzi. Michomo hiyo inapatikana zaidi katika chanjo zinazotokana na nyimbo ya Nyonda, Waridi lisilomiba, Zabibu na Sega la asali. Pia amegundua kuwa nyimbo za Seif Salim zinazungumzia mapenzi ya kweli na mapenzi ya uongo, majigambo, maadili mazuri, wivu, khiyana, mabadiliko na maendeleo katika mapenzi, dhuluma na uonevu, usaliti na nafasi ya mwanamke. Mwisho Rajab (keshatajwa) amegundua kwamba, uhalisia wa nyimbo za Seif Salim na namna zinavyotumika kwa kuliwazana, kuburudishana na kufurahishana. Kazi ya Rajab imemsaidia mtafiti wa kazi hii kwa kiasi kikubwa kuelewa namna ya kubainisha dhamira katika nyimbo za taarab asilia. Hata hivyo dhima zilizobainishwa katika nyimbo za Seif Salim, zilijikita kwenye mapenzi tu bila kugusia masuala ya uchumi, siasa na utamaduni katika nyimbo hizo. Mtafiti wa kazi hii yeye kwa upande wake ana lengo na dhamira za kubainisha dhima za aina zote zinazojitokeza katika nyimbo za Shakila Said. Pia utafiti wa Rajab umemsaidia mtafiti kupata mwanga wa kuchambua dhima mbalimbali zinazohusu nyimbo za taarab asilia za Shakila.

Mbwana (2016) alitathmini mabadiliko ya matumizi ya nyimbo za harusi za Kipemba kwenda katika kasida za harusi. Matokeo ya tathmini hii ni kwamba nyimbo za harusi za Kipemba na kasida za harusi zina mfanano mkubwa katika muktadha na dhima ya nyimbo/kasida hizo. Mfanano huo umesababishwa na mazingira, utamaduni na shughuli za kikazi zinazofanywa Uswahilini. Kazi ya Mbwana ilimsaidia mtafiti huyu kuyabaini makusudio ya nyimbo na namna yanavyochukua nafasi ya kufikisha dhima zake kwa jamii ya Waswahili wa Afrika Mashariki.

Wazir (2016) alichunguza dhima ya nyimbo za singo katika kijiji cha Uzini. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kwamba nyimbo za singo bado zina dhima kubwa. Miongoni mwa dhima hizo ni pamoja na kuendeleza utamaduni wa watu wa Uzini na kuwasinga wari kwa kutumia nyimbo hizo ambazo zinatoa mafunzo maalumu kwa maisha ya wanandoa. Wazir (keshatajwa) amefanya kazi nzuri kwani kwa kiasi kikubwa mtafiti wa kazi hii alipata muongozo mzuri kuhusu dhana nzima ya nyimbo na namna ya kuchambua data zinazotokana na nyimbo. Baada ya mapitio ya kazi tangulizi, mtafiti wa kazi hii amegundua kuwa ingawaje wapo watafiti walioandika kuhusu nyimbo za Shakila lakini hawajagusia hata kidogo kuhusu mchango wa nyimbo za Shakila kwa jamii ya Waswahili wa Afrika Mashariki katika maeneo ya kiuchumi, mapenzi, siasa na utamaduni. Kwa hivyo ili kupunguza mwanya ulioachwa na watangulizi wake, mtafiti ameona ipo haja ya kufanya utafiti katika eneo hilo ili kuchambua na kuona mchango wa muimbaji Shakila kupitia baadhi ya nyimbo zake alizoziteuwa.

2.4 Mkabala wa Kinadharia

TUKI (2004:300) wanafasili nadharia kwamba ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kutekeleza jambo fulani. Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi kuifahamu kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Wanaendelea kufafanua kwamba nadharia ni maelezo ya jambo kufungamana na vigezo vilivyowekwa au vinavyozalika kutokana na majaribio ya jambo hilo. Hii inamaanisha kwamba nadharia inaweza kutokana na mawazo yaliyoundwa kitambo na jopo la wataalamu au inaweza kutokana na

usomaji makini wa kazi ya fasihi na mtu binafsi. Mdee na wenzake (2011) wanaifasili nadharia kama ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani. Kwa mwelekeo wa fasili hii ni kuihalalisha mipango yote ya mawazo iliyotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani iwe ni nadharia. Si kila mpango ulio hivyo unaweza kuitwa nadharia, mpango ambao utaweza kuitwa nadharia ni ule tu wa kitaalamu.

Jilala (2016) anaifasili nadharia kwa kusema kuwa ni wazo ambalo huibuliwa kama mwongozo kwa msomaji ama mchambuzi na hata mwanafasihi linganishi katika kutoa majumuisho ya kazi za fasihi na zisizo za fasihi. Anaendelea kufafanua kwa kusema kuwa aidha ni wazo kuu, fikra kuu, mwongozo wa mtu au watu au jamii ya mahali fulani wakati fulani kwa lengo maalumu. Aidha, anaendelea kusema kwamba nadharia humwongoza mtu kutenda jambo fulani kwa utaratibu mzuri. Kwa hiyo, nadharia ndio msingi mkuu wa kuweza kuelezea jambo fulani ili liweze kukubalika, kuaminika na kufanyiwa kazi na watu wa jamii husika ama taaluma ya fani husika. Kutokana na fasili hizo tunaweza kusema kwamba; nadharia ni muongozo, kanuni au dira inayomsaidia mtu katika kueleza mawazo yake katika kuchambua au kufanya kazi yeyote ile. Mtafiti wa kazi hii ameteuwa nadharia mbili ambazo ni nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya Simiotiki. Nadharia zote mbili zilikwenda sambamba katika kukamilisha uchambuzi wa data na kukidhi mahitaji ya lengo la kwanza na la pili la utafiti huu

.

2.4.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Njogu na Wafula (2007) wanaeleza kwamba, nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

ambayo husisitiza nguvu za msomaji, iliasisiwa na wahakiki wa Kijerumani mwishoni mwa miaka ya (1960). Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Robert C. Holub, Hans Robert Jauss na Wolfagang Isser. Njogu na Wafula wanamnukuu Holub akieleza kwamba, nadharia ya upokezi (nadharia ya Mwitiko wa Msomaji) ni mabadiliko ya jumla ya umakinikaji kutoka kwa mwandishi na kazi yake kwenda kwa matini na msomaji.

Wanaitifaki wa nadharia hii wanashikilia kwamba, kazi ya fasihi hupata maana baada ya kukabiliwa matini hiyo na msomaji. Msomaji au mpokeaji huipa maana kazi hiyo kutokana na uzoefu wake wa maisha. Kwa upande wake, Adena Rosmarin (Murfin, 1991) anadai kuwa kazi ya fasihi ni kama kinyago ambacho hakijakamilika na kwa hivyo mchongaji hujaribu kukikamilisha. Hivyo, mihimili ya nadharia hii ni kwamba, msomaji huikamilisha kazi ya sanaa kwa kuijaliza kwa usomaji makini au kuidhalilisha kwa usomaji holela. Iser na Fish (1870) wanadai kwamba kazi ya fasihi huwa na mapengo mengi ambayo msomaji hulazimika kuyajaliza. Kwa hivyo, msomaji hushurutika kutunga matini mpya ambazo zimechochewa na kuzalika kutokana na matini asili zilizoko kwenye kurasa. Kwa hivyo, nadharia ya mwitiko wa msomaji hufasili fasihi kama mchakato wa namna msomaji na msanii wanavyoathiriana. Uzoefu wa maisha wa msomaji unaweza kusaidia katika kutoa tafsiri ya kazi ya fasihi na kupata tafsiri tofauti kati ya msomaji mmoja na mwengine. Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inaelezwa kuwa na mapungufu kwamba, inaifanya kazi ya fasihi kutokuwa na maana mpaka pale inapoingia mikononi mwa msomaji. Pia nadharia hii inatabia ya kuchukuwa mawazo ya kila msomaji wa kazi ya fasihi na kuyafanya kuwa ni sahihi, jambo ambalo sio sahihi kuwa, kila mtu ana

uwezo wa kutoa tafsiri sahihi juu ya kazi fulani ya fasihi. Mtafiti wa utafiti huu amechagua nadharia hii ili imuongoze katika kufanya uchambuzi wa dhamira mbalimbali na baadhi ya mbinu za kisanaa zilizojitokeza katika kazi iliyotafitiwa. Nadharia hii imemsaidia na kumpa fursa mtafiti katika kuihukumu kazi kutegemea uzoefu wake alionao na kwa mujibu ya ufahamu wake baada ya kuisoma na kuielewa.

2.4.2 Nadharia ya Simiotiki

Wamitila (2002) na Njogu na Chimerah (2007) wanaelezea Simiotiki kuwa ni neno la kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo hutumiwa kuelezea mielekeo na makundi fulani ya kiuhakiki. Nadharia hii imeasisiwa na Ferdinand Dessoussure 1857 mpaka 1913. Anafafanua katika matumizi ya lugha kuna vitu viwili, kuna kitaja na kitajwa na mara nyingi hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kitaja na kitajwa bali kuna ishara, picha, taswira au misimbo. Hata hivyo vipo baadhi ya vitu ambavyo huleta uhusiano kati ya kitaja na kitajwa hasa utakapotumia anamatopea (sauti mwigo).

Barthes (1994) anaeleza kuwa kuna aina tano za misimbo, kuna alama ambazo hutumiwa na wanaadamu katika mawasiliano ya kila siku. Anazitaja aina hizo kuwa ni msimbo wa kimatukio, msimbo wa kihemenetiki, msimbo wa kiseme, msimbo wa kiishara na msimbo wa kirejelezi.

Dr. Maguo katika mhadhara aliofanya tarehe 18/07/2016 kwa wanafunzi wa M. A. Kiswahili katika ukumbi wa Madungu Chake - Chake Pemba aliainisha aina tano za

misimbo kuwa ni msimbo wa kihemenitiki, msimbo wa kimatukio, msimbo wa kiutamaduni, msimbo wa kisemantiki na msimbo wa kirejelezi/ishara.

Msimbo wa kimatukio ni msimbo ambao kutokea kwa visa na matukio yanakuwa kialama au kimsimbo, kwa mfano mbwa anaingia jikoni. Huu ni msimbo kwani matendo haya hayamuhusu mbwa bali yanamuwakilisha mtu mwenye tabia za mbwa (Maelezo ya mhadhara wa Omari, 2016).

Msimbo wa kihemenitiki, msimbo huu unahusishwa na anuwani ya kifasihi. Anuwani hii inaweza kuwa jina la kitabu, jina la sura, kichwa cha shairi ama kichwa cha habari (Omari, 2011).

Msimbo wa kiutamaduni, msimbo huu unazungumzia maeneo ya kiutamaduni yanayoainishwa katika kazi ya fasihi. Kwa mfano kutajwa kwa aina ya chakula, mavazi, makazi na sehemu zinazofanyiwa mambo ya kiutamaduni, mfano Giningi (Mhadhara wa Omari, 2016). Hivi vyote vinaashiria misimbo ya kiutamaduni.
Msimbo wa kirejelezi/kiishara ni msimbo unaojengwa kutokana na viashiria vya utamaduni unaorejelewa katika kazi husika ya kifasihi (Wamitila, 2002).

Ubora wa nadharia ya Simiotiki ni kumsaidia mchambuzi wa kazi ya fasihi kufumbua mafumbo ambayo isingekuwa rahisi kuyafumbua kwa kutumia nadharia nyengine. Upungufu wa nadharia hii ni kuwa inachukulia kwamba ishara zote kila mahali na wakati wote zitakuwa na maana, ambapo ishara zingine huwa hazina ujumbe wa aina yoyote. Griffen (1997: 118) ni kweli kuwa, simiotiki ina

hatari ya kuwa juu ya kila kitu kiasi cha kupoteza uhalisia. Kauli hii inathibitisha kuwa waumini hao wa nadharia ya simiotiki msimamo wao ni kwamba kila ishara katika kazi ya fasihi ina maana jambo ambalo sio sahihi. Kwa upande mwengine nadharia hii imekuwa na upungufu kwani haiwezi kutumika katika kazi ambayo iko wazi na inaeleza uhalisia wa mambo.

Mtafiti wa kazi hii ameamua kutumia nadharia ya simiotiki kwa sababu nadharia hii kazi yake kubwa ni kufumbua mafumbo katika kazi za kifasihi zilizojengeka kiishara wakati utafiti huu una lengo la kuchunguza dhamira na fani zilizojificha ndani ya mafumbo ya nyimbo za Shakila zilizokolezwa lugha ya ishara kama ni sehemu ya kuboresha usanii wa mtunzi na muimbaji.

2.5 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti ameelezea mapitio ya kazi tangulizi na mikabala ya kinadharia iliyokwenda sambamba na ufafanuzi wa istilahi ambazo zinahusika moja kwa moja katika utafiti huu na pia zinauhusiano na nyimbo za taarab asilia. Aidha nadharia ambazo zimemsaidia mtafiti katika kuchambua data zimefafanuliwa kwa upeo mpana ili iwe msaada kwa watumiaji wa utafiti huu. Ifuatayo ni sura ya tatu ambayo ilielezea kuhusu mbinu za utafiti.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii imezumgumzia mbinu mbalimbali za utafiti zilizotumika katika utafiti huu.Vipengele vilivyoainishwa katika sura hii ni pamoja eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, aina za data zilizokusanywa, mbinu za kukusanyia data za msingi, mbinu za kukusanyia data za upili, mbinu za uchambuzi wa data na kumalizia na hitimisho.

3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni pahala ambapo mtafiti amekusudia kwenda au kutumia katika kukusanya data za utafiti (Enon, 1998). Utafiti huu umetumia nyimbo 15 za Shakila zilizorikodiwa na kuandikwa ili kurahisisha upatikanaji wa data za msingi.

Vile vile katika eneo hilo ndipo ambapo taarifa za msanii huyu ambazo ziliuwezesha utafiti huu kukamilika zilipatikana. Katika upatikanaji wa data za upili, Mtafiti alitumia maktaba ya Chuo Kikuu Huria tawi la Pemba na Makao Makuu ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar-es- Salaam, maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar- es Salaam, maktaba ya mjini Unguja, internet na Ofisi za Kampuni ya Ukombozi Uni Ltd Pemba. Mtafiti aliyatumia maeneo haya ili kutafuta kumbukumbu za msanii Shakila zilizokamilisha upatikanaji wa data za utafiti huu kuwa na viwango bora kulingana na mahitaji ya mada, na jamii itakayohitaji kutumia utafiti huo.Vyanzo hivi vya data viliweza kutosheleza mahitaji ya maswali ya utafiti huu bila kufika mjini Tanga ambako msanii Shakila Saidi alizaliwa.

3.3 Usanifu wa Utafiti

Kothari (2004) anafafanua kuwa hiki ni kipengele kinachoonesha taswira au picha kamili ya utafiti husika. Ni kipengele kinachoonesha kwamba utafanyika vipi, lini, wapi, kwa muda gani na kwa kutumia mbinu gani zinazosaidia kupatikana kwa data zenye mantiki zinazojibu maswali ya utafiti husika. Robson (2007) anaelezea dhana hii ya umbo la utafiti au usanifu wa utafiti kuwa ni mchoro au ramani inayoonesha namna utafiti utakavyofanyika tangu katika kukusanya data mpaka kuchambua data na kuandika ripoti ya utafiti.

Lyatuu (2011) amemnukuu Orodho (2003) ambaye anasema kwamba umbo la utafiti au usanifu wa utafiti ni mpangilio wa taratibu zinazotumika kukusanya na kuchambua data kwa namna ambayo inaunganisha data zinazopatikana na malengo ya utafiti. Utafiti huu umetumia umbo la kimaelezo. Umbo hili limeelezewa na Enon (1999) kuwa ni njia ya kukusanyia data na kuzifanyia uchambuzi kwa maelezo ambapo nambari huwa hazitumiki. Hivyo, data za utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa njia hiyo ya kimaelezo. Utafiti huu ni wa uchunguzi kifani na umechukua mifano ya nyimbo za taarab asilia zilizoteuliwa za muimbaji Shakila tu na sio za msanii mwengine yoyote. Mtafiti alichagua nyimbo za Shakila kwa sababu zilimuwezesha kufikia malengo ya utafiti huu. Pia mtafiti alitumia njia ya maelezo kuzichambua data kulingana na malengo mahususi ya utafiti huu na kwa muda uliopangwa.

3.4 Kundi Lengwa

Kwa mujibu wa Cooper (1989) na Vans (1990) kundi lengwa ni wanachama wote au

hata mtu mmoja, kundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Kundi lengwa la utafiti huu ni nyimbo za taarabu asilia za msanii Shakila Said. Utafiti huu ulitumia nyimbo 15 za taarab asilia za msanii Shakila Saidi ambae alikuwa ni muimbaji maarufu sana, na sauti yake ilisikika mwambao wote wa Mashariki ya Afrika. Na nyimbo zake bado zinaendelea kuchukua nafasi katika medali ya uimbaji. Zinafunza, zinaburudisha na zinadumisha utamaduni wa Waswahili.

3.5 Sampuli na Usamplishaji

Kothari (2004) anaelezea kuwa sampuli ni kundi dogo la watafitiwa linalochaguliwa na mtafiti kuwakilisha sifa na tabia za kundi zima ambalo humsaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo ili atoe majumuisho ya utafiti wake. Caeser (1998) anasema kwamba usampuishaji ni utaratibu wa kuchagua kundi ili kuwakilisha kundi kubwa kwa kupata taarifa za utafiti. Katika utafiti huu, mtafiti alitumia sampuli nasibu kwa sababu ameona kwamba atapata data za uhakika na kwa muda mfupi. Mtafiti ametumia nyimbo 15 za taarab asilia za muimbaji Shakila Said. Nyimbo zilizohusishwa ni Mapenzi yamepungua, Hujui alacho kuku, Mapenzi ni kama donda, Sasambua, Akukataaye hakwambii toka, Nimezama kwa mapenzi, Kuku na yai, Mpenzi unisamehe, Macho yanacheka moyo unalia, Kifo cha mahaba, Mkuna na mkunwaji, Yarabi sinipe mapenzi, Pazia, Viva FRELIMO na Aloanza pekepeke. Nyimbo hizi zimeteuliwa kama sampuli miongoni mwa nyimbo nyingi zilizoimbwa na Shakila Said.

3.6 Data za Utafiti

Katika utafiti huu mtafiti alikusanya data za aina mbili ambazo ni data za msingi na data za upili. Aina hizi za data zimefafanuliwa kama ifuatavyo:

3.6.1 Data za Msingi

Kothari (2004) anaeleza kuwa data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na kwa hivyo ni data mpya. Furlong (2000) anafafanua kwamba data za msingi ni zile ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwengine yeyote kwa lengo na matumizi kama yanayofanywa na mtafiti wa kwanza. Katika utafiti huu mtafiti alikusanya data za msingi kupitia uchambuzi wa nyimbo 15 za Shakila Saidi zilizoteuliwa ambazo ziliakisi mahitaji ya tatizo la utafiti huu.

3.6.2 Data za Upili

Cresswell (2009) anasema data za upili ni zile zilizokwisha kusanywa na watafiti wengine kwa ajili ya kutimiza malengo ya tafiti zao na kuandika ripoti, makala, majarida, vitabu tayari kwa ajili ya kusomwa kama marejeo katika maktaba mbalimbali. Data hizi zilitumika wakati wa kuchambua data za utafiti, kwa lengo la kutilia mkazo hoja za msingi na kuzifanya ziwe na nguvu zaidi. Maktaba alizotumia mtafiti kupata data za upili ni pamoja na Maktaba ya Chuo Kikuu Huria tawi la Pemba, Maktaba Kuu ya Chake - Chake, Makavazi ya Taasisi za Taaluma ya Kiswahili (TATAKI) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Katika maktaba hizi mtafiti alizisoma nyaraka kama vile Makala, tasnifu, majarida pamoja na vitabu vilivyolingana na mada ya utafiti huku akiangalia malengo mahsusi ya utafiti wake.

3.7 Mbinu za Kukusanyia Data

Kothari (2004) anaifafanua dhana ya ukusanyaji wa data kuwa ni zoezi la awali ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti. Mtafiti wa utafiti huu alikusanya data kwa kutumia mbinu ya usomaji makini kwa kupata data za msingi na upitiaji wa nyaraka maktabani kukusanya data za upili.

3.7.1 Usomaji Makini

Usomaji makini au wakati mwingine hujulikana kama usomaji wa kina ni mbinu ya kukusanya data za msingi kutoka kwenye matini zilizoteuliwa katika utafiti husika (Kothari, 1990). Kupitia mbinu hii, mtafiti huteua matini maalumu na kuzisoma kwa kina huku akidondoa baadhi ya maneno, sentensi au aya ambazo ndizo huwa data za utafiti wake. Mtafiti alitumia mbinu ya usomaji makini kwa kuzipitia nyimbo zote 15 za Shakila alizoziandika. Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kwa sababu ilimwezesha kupata data alizozihitaji na kukamilisha malengo ya utafiti wake.

Data za msingi katika utafiti huu ndizo zilikazokusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini kutoka katika nyimbo za Shakila Saidi. Katika kufanikisha zoezi hili la ukusanyaji wa data, mtafiti aliandaa daftari maalumu ambalo aliligawanya katika sehemu kuu mbili na kila sehemu ikiwa na kichwa cha habari kinachohusiana na malengo mahususi ya utafiti wake. Hii ilirahisisha zoezi la ukusanyaji wa data ambapo mtafiti kila alipobaini maneno, msitari au ubeti katika nyimbo teule

iliyohusiana na malengo yake ya utafiti basi aliyadondoa na kuyaandika katika daftari hilo kama alivyopanga.

3.7.2 Upitiaji wa Nyaraka

Upitiaji wa nyaraka maktabani ni mbinu ya kukusanya data za upili ambapo mtafiti hukusanya taarifa zinazohusiana na mada yake ya utafiti kutoka katika machapisho aliyoyasoma kwa uzingativu (Kothari, 1990). Data za upili hutumika kukazia hoja zilizotokana na data za msingi katika uchambuzi wa data. Pamoja na hayo, pia data za upili hutumika katika uandishi wa sura ya pili ya tasinifu “mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia". Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika machapisho mbalimbali katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania Tawi la Pemba, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Makavazi ya Taasisi za Taaluma ya Kiswahili (TATAKI), Maktaba Kuu ya Chake Chake na internet. Katika vyanzo hivi mtafiti alisoma makala, ripoti, tasnifu, majarida, vitabu na maandishi pepe katika wavuti na tovuti zilizohusiana na mada ya utafiti na kuweza kukamilisha utafiti huu kwa ufanisi.

3.8 Uchambuzi wa Data za Utafiti

Katika uchambuzi wa data za utafiti huu, mtafiti alitumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo katika kuchambua na kujadili data za utafiti na maelezo yake. Kwa mujibu wa Kothari (1990) mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huzichambua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya utafiti wake. Mtafiti alichagua kutumia mbinu hii katika kuchambua data zinazohusiana na fasihi kwa sababu fasihi ni taaluma ya maneno ama ya kuandikwa

au kuzungumzwa. Kwa muktadha huo mkabala huu ulitosheleza na kukidhi haja ya kiuchambuzi na kufikia malengo mahsusi ya utafiti huu.

3.9 Hitimisho

Sehemu ya tatu ya utafiti ni sehemu inayoeleza mambo ya msingi yanayowezesha mchakato wa kukusanya na kuweka msingi wa uchambuzi wa data za utafiti. Ukusanyaji wa data za msingi na data za upili kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka maktabani. Mbinu hizi huufanya utafiti kukamilika na kukidhi viwango vya kitaaluma. Sambamba na hayo sehemu hii imeelezea watafitiwa ni nani/nini na wameteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Baaba ya sura ya tatu ifuatayo ni sura ya nne itakayohusika na uwasilishaji, uchambuzi na matokeo ya utafiti.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti alishughulikia kuchambua data za msingi ambazo zilikusanywa moja kwa moja kutoka maktabani. Uchambuzi na uwasilishaji huu ulifanywa kulingana na malengo mahsusi ili kubaini kwamba yamefikiwa na mtafiti. Uchambuzi huu ulirejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na Nadharia ya Simiotiki. Pia sura hii inatambulisha dhamira na fani zilizomo katika nyimbo za Shakila Saidi Khamisi na inajibu maswali mawili ya utafiti yaliyoongoza utafiti huu.

4.2 Utafiti na Malengo Yake

Katika utafiti huu malengo yamegawika katika sehemu mbili. Lengo kuu na malengo mahsusi. Lengo kuu la utafiti lilikuwa ni Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo za Taarab Asilia: Mifano ya Nyimbo za Shakila Saidi Khamisi. Na malengo mahsusi yalikuwa ni:-

i) Kuchambua dhamira zilizojitokeza katika nyimbo teule za Shakila Saidi.

ii) Kubainisha mbinu za kisanaa zinazojitokeza katika nyimbo za Shakila Saidi.

4.2.1 Dhamira zilizojitokeza katika Nyimbo za Taarab Asilia za Shakila Saidi

Katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu, mtafiti amezingatia lengo mahsusi la kwanza la utafiti huu lisemalo: Kuchambua dhamira zilizojitokeza katika nyimbo teule za Shakila Saidi. Lengo hili linakwenda sambamba na swali la msingi la kwanza la utafiti huu linalosema: Ni dhamira gani zinazojitokeza katika nyimbo

teule za Shakila Saidi? Ili kufanikisha lengo mahususi la kwanza na kujibu swali la kwanza, mtafiti amebaini dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika nyimbo za Shakila Saidi. Mtafiti ameongozwa na nadharia ya simiotiki na mwitiko wa msomaji kama ifuatavyo:-

4.2.1.1 Dhamira ya Mapenzi

Mapenzi ni hisia kali za upendo ambazo humfanya mtu kujisikia furaha na amani katika moyo wake. Vile vile mapenzi yapo katika matabaka mawili. Tabaka la kwanza ni lile linalohusisha mapenzi ya jinsia mbili tofauti au moja kwa dhamira ya kuridhishana kingono. Tabaka la pili ni mapenzi yanayohusisha jinsia mbili tofauti au jinsia moja kwa dhamira ya urafiki na sio kingono (http://www.ackyshine.com/mahusiano:maana-ya-mapenzi). Kwa ujumla tunaweza kuelezea mapenzi kuwa ni hisia nzito za moyoni zinazomfanya mtu avutike, athamini na ajali mtu, kitu au jambo. Mapenzi yanaweza kujengeka kupitia katika misingi ya uvumilivu, hekima, busara, uwazi, upendo na heshima.

Mtafiti wa kazi hii katika kukusanya data zake na kuzichambua amegundua kwamba takriban wasanii wengi husanii kazi zao za kifasihi kutokana na misukumo mbalimbali iliyomo katika maisha ya jamii. Wasanii pia husukumwa na vichocheo vinavyowakabili yakiwemo mapenzi. Al-anisa Shakila pia na yeye alizungumzia suala zima la mapenzi yakiwemo mapenzi ya dhati, ya udanganyifu, mapenzi ya ndani ya ndoa n.k. Mara nyingi dhamira ya kimapenzi inakuwa kama kichocheo chanya kinachoongeza au kuchochea mihemko inayodumisha upendo na maelewano mazuri ya pande mbili. Mfano wa mapenzi yaliyogusiwa ni mapenzi ya mke na

mume, viongozi na raia, mwalimu na mwanafunzi na mapenzi ya aina nyenginezo. Katika kipindi cha ukusanyaji wa data kutoka katika vianzio husika mtafiti amegundua aina mbali mbali za mapenzi kama alivyoziorodheresha hapo chini.

4.2.1.1.1 Mapenzi ya Dhati

Rajab (2016) amesema kwamba: Mapenzi ya dhati ni mapenzi ambayo huonekana na umadhubuti usioyumba na usiokubali chokochoko na fitina za aina yoyote kwa wapendanao. Mapenzi haya hujengwa kwa watu kuthaminiana, kuenziana, kushibana, kukinaiana na kusaidiana kwa hali na mali katika mapenzi yao.

Mapenzi ya dhati yamejitokeza katika nyimbo za Shakila kama vile "*Aloanza peke peke",* katika wimbo huu mtafiti amegundua mapenzi ya dhati pale msanii aliposema katika ubeti wa pili wa wimbo huu:

Alitaka kututenga kutuweka mbali mbali
Shabaha aloilenga Mungu hakuikubali
Alitaka kututenga kutuweka mbali mbali
Shabaha aloilenga Mungu hakuikubali.

Mapenzi ya dhati yanaonekana kwamba hata hila na fitina ambazo zilikuwa ni kama cheche zilizopalilia uovu wa kutaka kuwatenganisha watu hawa lakini bado nyoyo zao zilishibana na kusabiliana kikweli. Kutokana na sababu hii haikuwa rahisi kuwatenganisha. Shakila aliangusha msisitizo kwa kusema kuwa "Mungu hakuyakubali" majungu hayo. Haya ni maono ya mtafiti kuifasili matini kulingana na mtazamo wake mwenyewe.

Vile vile katika Wimbo wa *"Mpenzi unisamehe"* nao pia msanii alikuwa akituonyesha mapenzi haya ya dhati pale aliposema katika beti ya 1 ya wimbo huu.

Kama kosa nimeridhi sirejei asilani
Mpenzi naomba radhi Tuishi kama zamani
Mpenzi naomba radhi Tuishi kama zamani
Kama kosa nimeridhi Sirejei asilani
Kama kosa nimeridhi Sirejei asilani
Adhabuyo nakubali Uniadhibu mwandani
Adhabuyo nakubali Uniadhibu mwandani

Beti hii ya wimbo inaonesha kwamba alifanya kosa kubwa dhidi ya mpenzi wake. Kutokana na mapenzi ya dhati aliyokuwa nayo alielewa kwamba kafanya kosa na analazimika kumuomba radhi mpenzi wake ili amsamehe kutokana na kosa hilo. Aliamua kuomba radhi kwa kutumia maneno adhimu ambayo aliyatoa kwenye moyo wake na kukiri kuwa yeye ndiye mwandani wake. Kama tunavyojua kuwa unapopewa cheo cha mwandani inamaana kwamba wewe ni mtu mwenye sifa za pekee. Mtu maalum aliyeingizwa ndani ya moyo na kupewa nafasi adhimu ya upenzi wa hali ya juu.

Dai hili pia lilitiliwa mkazo na Shaaban Robert katika kitabu chake cha *Maisha yangu na baada ya miaka 50* (2003) alimpa sifa mpenzi (mke) wake na kummiminia sifa nyingi wakati anamuaga baada ya mauti yake kwa kusema:-

Majonzi hayaneneki kila nikikumbukia
Nawaza kile na hiki naona kama ruia
Mauti siyasadiki kuwa mwisho wa dunia
Mapenzi tuloyafunga hapana wakufungua

Hii ni kuonyesha mapenzi ya dhati yaliyodondokezewa chembe za huzuni miongoni mwao. Haya ni maoni ya mtafiti mwenyewe kupitia nadharia teule ya mwitiko wa msomaji ambayo haimfungi mtafiti katika kuichambua kazi ya fasihi. Sambamba na

hilo mtafiti ameona kupitia nadharia hiyo dhana ya mapenzi ya dhati ina umuhimu mkubwa katika familia na jamii kwa ujumla.

Mapenzi ya dhati yamejitokeza tena katika wimbo **"***Oh Rabi sinipe mapenzi***".** Katika ubeti wa tatu wa wimbo huu msanii anasema:

> Kwa dhati nilimpenda haya nilikuwa sina
> Visa alivyonitenda ni fedheha kuvinena
> Niliuguwa vidonda oooh!
> Niliugua vidonda sasa nimekwisha pona

Katika ulimwengu vitu vikubwa vinavyoumiza na kupumbaza moja wapo ni mapenzi. Mapenzi yanaweza kumfanya mtu akawa chizi, akatokwa na haya au kutokwa na aibu. Hili limemkuta msanii wetu aliposema "*kwa dhati nilimpenda haya nilikuwa sina"*. Hii ni kuonyesha kwamba mapenzi ni sawa na wendawazimu yanapoingia moyoni. Mapenzi yanaweza kumpelekea mtu kufanya jambo lolote ikiwa la kuridhisha au la kukera. Mara nyingi mtu anapokuwa na mpenzi wake anaweza kufanya mambo ya kiajabu ajabu hata kuvua nguo, kujishebedua, kujirusha, kuchokora hiki na hiki. Yote hayo huyafanya kwa lengo la kukoleza penzi lao ili liwe na uimara usioshuka hadhi yake.

Msanii wa wimbo huu ameonesha kwamba yote ambayo yalimkuta ya madhila dhidi ya mpenzi wake lakini bado alikuwa na upenzi wa dhati na wa hali ya juu.Msanii kwa madai yake alifika kuugua kidonda cha moyo kwa sababu ya penzi hilo. Ingawa mziwanda wake hakuonyesha kujali na badala yake alimfanyia matendo ya kinyama ambayo ilimuwia vigumu kuvisema hadharani. Kwa binaadamu haya ni mambo ya kawaida kuwa yule anaempenda kwa dhati na kumfanyia yale yote yenye kuonyesha upenzi basi hatojali wala kufikiri matokeo yake atakulipa maovu. Hili pia

alilionyesha mwandishi Shaaban Robert katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, alivyomchora Adili na sifa zake njema na upenzi wa hali ya juu kwa ndugu zake. Matokeo yake ndugu hao walimfanyia Adili vitendo vya kumtosa baharini kutokana na uchoyo waliokuwa nao (uk: 31–32). Haya ni maoni ya mtafiti yakisaidiwa na nadharia ya mwitiko wa Msomaji.

Mapenzi mengine ya dhati yamejitokeza katika wimbo wa *Nimezama kwa mapenzi* Mtafiti wa kazi hii amegundua kuwa msanii katika wimbo huu aliingia ndani sana kuyachambua mapenzi ya ndani. Mapemzi yanagusa kiini cha moyo yanavyochokonoa hisia nzito zinazompata mtu anapozama katika dimbwi la mapenzi. Uthibitisho wa hilo ni pale msanii aliposema katika kiitikio cha wimbo huu:

> Nimezama kwa mapenzi
> Sijui kama tazuka
> Nimezama kwa mapenzi
> Sijui kama tazuka

Kutokana na maoni ya mtafiti akisaidiwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kupitia mihimili yake inayompa fursa mtafiti kutoa mawazo yake. Mtafiti amegundua kwamba msanii ameonyesha jinsi alivyoathiriwa na penzi zito na tamu lililomfanya ajielewe kuwa hatolikosa lile analohitajia kwa mziwanda wake. Alijifananisha na mtu ambaye yuko katikati ya bahari na hatarajii kuja juu tena kutokana na kina kirefu cha maji ya mkondo wa bahari hiyo. Msanii ana maana kwamba mapenzi ya mpenzi wake yamemuingia kwa kasi kubwa na yamejikusanya ndani ya moyo na kwamba sio rahisi kutoka. Msanii ameamua kumpenda hasa mpenzi wake. Sio kumpenda kiutani utani au kumpenda kwa mapenzi ya

udanganyifu. Mapenzi kama haya yameshadidiwa na Sengo (2007) katika Utendi wa Mambo Mambo (uk: 31) ubeti wa 176 ambapo anaposema:

> Mke na mume kifungo
> Wao kwa wao kiungo
> Kifamilia mtungo
> Daima kukumbukia

Hapa msanii ameonesha umuhimu na umadhubuti wa mapenzi ya kweli na namna wapendenao wanavyokuwa na mahusiano ya karibu na kushibana kiasi kwamba msanii anawapigiwa mfano wa kuwa kifungo. Mfano huu uinaashiria mshonano na mshikamano wa nyonda hawa hadi wanalinganishwa kuwa kiungo kimoja kutokana na mapenzi ya dhati waliyonayo wawili hawa. Mapenzi yao yamefikia kiwango cha juu kiasi kwamba kila mmoja anaathirika kwa mwenzake. Shida na raha ni zakwao pamoja kama msanii anavyotuonesha kuwa" kifamilia huwa kama mtungo" ana maana kwamba mapenzi ya dhati yaliyojikita kwao yamewasababisha wasiweze kutengana wawe kitu kimoja wakati wote na pahala popote.

Pamoja na hayo, mapenzi ya dhati hubeba shauku ya moyo kutaka kujua alilonalo mpenzi wake katika mapenzi yao kwa lengo la kuiridhisha nafsi yake ili iwe ni pumbazo linaloweka moyo sawa. Uthibitisho wa hili unaonekana katika wimbo wa "*Macho yanacheka"*. Kwa kuanzia na jina la wimbo, mtunzi au msanii ametumia tashhisi ambayo ilimpelekea kuipamba kazi yake ya fasihi ili iweze kuleta mvuto kwa msomaji. Katika ubeti wa tatu wa wimbo huu msanii ametuonyesha shauku au hamu ya kutaka kujua ni kiasi gani anapendwa au kutaka kujua anamuenzi kwa kiasi gani na jee penzi lake halijaingiliwa na mtu yoyote. Hivyo alimtaka mpenzi wake

amueleze ili moyo wake upate kutulia. Kutokana na maelezo hayo ndipo msanii alipoyapamba maneno yake na kuyateremsha katika ubeti wa tatu (3) aliposema:

> Uwache dhihaka mpenzi sikia
> Uwache dhihaka mpenzi sikia
> Moyo waniwaka kweli nakwambia
> Moyo waniwaka kweli nakwambia
> Moyo waniwaka kweli nakwambia
> Moyo waniwaka kweli nakwambia
> Wanipa mashaka kwa zako tabia
> Wanipa mashaka kwa zako tabia
> Wanipa mashaka kwa zako tabia
> Wanipa mashaka kwa zako tabia
>
> Mtafiti amegundua kwamba msanii anahisi tabia za mpenzi wake zimebadilika. Hivyo alitaka ili amridhishe moyo wake yuko tayari amuweke sawa moyoni mwake kwa kumueleza kile ambacho kimo moyoni kutokana na tabia na mwenendo aliokua nao sasa. Hii ilimpelekea kutoa msisitizo wa maneno yake aliyoyarudiarudia mara nyingi katika ubeti huu.
> Uwache dhihaka mpenzi sikia...Moyo waniwaka kweli nakwambia...Wanipa mashaka kwa zako tabia...

Alichokieleza msanii ni kwamba asifanye dhihaka katika suala zima la mapenzi. Aelewe kuwa kitu mapenzi hakiwezi kutiwa mkono au kuchezewa vilivyo sivyo. Hivyo anamuwasa mpenzi wake ili awe na tabia njema yenye kuridhisha kwa lengo la kuimarisha mapenzi yao. Mtafiti amebainisha mapenzi hayo kama yalivyoshadidiwa na nadharia teule ya mwitiko wa msomaji na kuitaka jamii isimame imara kuendeleza mapenzi ya dhati kwa lengo la kujenga jamii yenye mafanikio.

Mapenzi mengine ya dhati yamejitokeza katika wimbo wa *Kifo cha mahaba* Al anisa Shakila ameyaeleza mapenzi na vikorombwezo vyake. Katika wimbo huu anatuelekeza kwamba bora ufe kwa ajali au ugonjwa lakini usiombe kufa kwa

mahaba. Kifo cha mahaba kina idhilali kubwa na kinaumiza moyo kupita kiasi. Msanii ana lengo la kutufahamisha umuhimu wa mapenzi na athari zake. Mapenzi ni kitu ambachoo hakitaki kufanyiwa mchezo au masihara. Kwani kitu hicho kinaweza kupoteza uhai wa mtu. Uthibitisho wa hili ni pale Shakila aliposema katika ubeti wa kwanza (i) wa wimbo huo kuwa:

Kifo cha mahaba kina idhilali
Hakina haiba wala afadhali
Kifo cha mahaba kina idhilali
Hakina haiba wala afadhali
Hakina haiba wala afadhali
Bali tajikaba nifilie mbali
Bali tajikaba nifilie mbali
Bali tajikaba nifilie mbali

Mtafiti wa kazi hii amegundua kwamba anachokizungumza msanii ni kuwa watu wanatakiwa wajitahidi kuwa na mapenzi ya dhati ili kuepusha migogogro isiyo ya lazima na kuifanya mioyo yao iwe katika hali ya utulivu. Isitoshe kiumbe anapofikiria maamuzi ambayo yatakuwa kinyume na matakwa ya Mwenyezi Mungu basi huko ni kujitafutia adhabu ambazo zinaweza kumuweka mahali pabaya. Mfano wa hili ni pale Shakila aliposema katika ubeti wa pili (ii) wa wimbo huu:

Kufa kwa mahaba ni adhabu kali
Leo ni msiba usio mithali
Kesho ni adhabu mbele ya jalali

Kutokana na maoni ya mtafiti akisaidiwa na nadharia teule ya Mwitiko wa Msomaji kwa kuzingatia mhimili wake unaotoa fursa kwa mtafiti kutoa mawazo yake kupitia beti iliyotangulia ameichambua dhana hii kwa kuzingatia vionjo vifuatavyo:-

Kwanza mahaba hayakusisitizwa kuwa kitu cha msingi kwa binaadamu. Baadhi ya watu wanayachukulia mahaba kuwa ni sehemu ya starehe ambayo kila mtu

anastahiki kupata. Hii ina maana kwamba mtu anaweza kuwa na nyonda (mpenzi) wake lakini asimjali kwa lolote wala chochote. Mmoja akamsabilia penzi mwenzake lakini yeye akawa anamdanganya tu. Kwa upande mwengine mtu anaweza kuwa na mke/mume wa ndoa lakini akapumbazika na penzi la mtu mwengine asiyekuwa mkewe. Hapo ndipo imapojitokeza migogoro ya nafsi na kuutia joto moyo na hata kupelekea kufanywa yasiyostahiki kutendwa. Sambamba na hilo msanii ametuonyesha kuwa yule aliyeathirika na penzi la mpenzi wake anapaswa amuonee huruma. Analazimika aelewe kuwa moyo wa mwenzake umemshiba na hahitaji mwengine. Hili limejidhihirisha katika ubeti wa tatu (3) wa wimbo huu pale msanii aliposema:

Ewe Mahabuba niepushe hili
Ni wewe tabiba hapana wa pili
Tapanda jaziba tajiuwa kweli

Kutokana na maoni ya mtafiti amegundua kwamba msanii anamueleza mpenzi wake kuwa yeye ni muaminifu na mtii kwake. Anamsisitiza ajuwe kwa dhati kuwa yeye ndie tabibu wake wa mapenzi na hakuna mbadala wake. Kwa sababu hiyo anamuhimiza mwenzake waishi kwa nidhamu ili waliengeenge penzi lao na kulijengea umadhubuti mkubwa kwa lengo la kuepusha migogoro isiyo ya lazima. Hivyo kama atafanya vyenginevyo au atamuendea kinyume anaweza kuyaweka maisha yake hatarini kama alivyosema atapanda jaziba na kumkaribisha shetani mbaya ayachezee maisha yake kwa mauti ya kujitakia.

Mtafiti wa kazi hii anaendelea kuchambua athari za mapenzi ya dhati zinazojitokeza kwa binadamu kwa kusema kuwa vyote chezea lakini mapenzi sio kitu cha kujaribu

au kukifanyia mzaha. Anayefanya mzaha na mapenzi anaweza kuhatarisha maisha ya mtu mwengine au hata maisha yake mwenyewe. Msanii wa nyimbo hizi anazidi kutufafanulia ukweli huu katika wimbo wa *Mapenzi ni kama donda* katika ubeti wa pili (2) wa wimbo huu anaposema:-

Ni kama donda mapenzi leo nawaelezea
Ni kama donda mapenzi leo nawaelezea
Waweza funga pumzi kuzimu ukaingia
Waweza funga pumzi kuzimu ukaingia
Wala hayana mjuzi yoyote humwelemea
Wala hayana mjuzi yoyote humwelemea

Katika ubeti huu msanii anatuonyesha uzito wa penzi na athari zinazotokana na mapenzi. Ni ukweli usiofichika kwamba mtu anaweza kwenda kuzimu kwa sababu ya mapenzi. Kuna watu wanaojidhulumu nafsi zao kutokana na mapenzi kwa kukataliwa na wenza wao. Mara nyengine hujidhulumu nafsi zao kutokana na kuwaona wenza wao na wanawake/wanaume wengine au kuoa wake wengine. Yote hayo yanasababisha maumivu ya ajabu yanayomsukuma mtu kufanya lolote analojisikia kulifanya. Sambamba na hilo msanii anaielewesha jamii kuwa suala la mapenzi halina lawama. Si vyema mtu kumlaumu na kumlalamikia mwenziwe kwa kapata mtihani wa kimapenzi. Si vyema kumsimanga au kumcheka. Hili ni suala ambalo yeyote linaweza kumfika. Uthibitisho wa hili ni maneno ya msanii katika ubeti wa 2:-

Wala hayana mjuzi yoyote humwelemea
Wala hayana mjuzi yoyote humwelemea

Mtafiti amegundua kwamba kitu mapenzi ni sawa na mafuta ya taa kwa jinsi yanavyotambaa. Mapenzi hayachagui kiongozi au sheikhe. Hayabagui mwanamke au mwanamme, mtoto au mtu mzima. Kila binaadamu ni lazima apitie katika hatua hii.

Ndio maana msanii akazidi kuishadidia na kuirudiarudia ubeti huo ili kutoa msisitizo unaostahiki.

Katika wimbo wa *Mapenzi ni kama donda* kwanza kabisa msanii katumia tashbiha katika kuyalinganisha mapenzi na donda kwa kutumia kiunganishi “kama”. Isitoshe mapenzi ni kama donda ni ishara ya mapenzi ya dhati anakuwanayo mtu kwa mwenza wake. Msanii anasema mapenzi ni kama donda kwa maana kuwa mtu anapokuwa na donda mwenyewe halioni uchafu hata kama linatoa harufu mbaya. Mmiliki wa donda huliengaenga na kulinyavuanyavua huku akilipelekea pua kusikiliza harufu yake. Vile vile ni kawaida ya donda kuleta maumivu basi pia mapenzi yanapojaa katika moyo huleta athari ya maumivu pia.

Kitu mapenzi humfanya mpenzi aweze kutokwa na machozi au kulia kabisa anapofikwa na kadhia ya mapenzi kwa mtu ampendae. Mpenzi kwa mpenzi wake anaweza kutokwa na machozi katika hali mbili, moja ni machozi ya furaha wakati anapokumbuka yale mazuri ambayo aliwahi kufanyiwa na mpenzi wake. Kama wakati wa kupeana huba nzito na zinazogusa hisia na kuchomoa michokonoo ya huba iliyofichikana ambayo imeganda ndani ya moyo wa mpenzi huyo. Pia mpenzi anaweza kutokwa na chozi kwa sababu ya maumivu yanayoleta hisia kali za fikra ambazo alizitenda mpenzi huyo kwa lengo la kukuvunja nguvu au kumkataa au kumfanya ukate tamaa. Mambo yote yanaweza kutokezea katika mapenzi. Uthibitisho wa hili ni maneno ya msanii aliyoyasema katika ubeti wa kwanza (1) wa wimbo huu:-

Nimechoka vumilia leo nawapasulia
Nimechoka vumilia leo nawapasulia

Imekuwa siku hizi kila siku nnalia
Imekuwa siku hizi kila siku nnalia
Nanyi hamniulizi kipi nnacholilia
Nanyi hamniulizi kipi nnacholilia

Kutokana na maono ya mtafiti, msanii katika ubeti huu amekumbana na kadhia mzito inayomfanya ahitaji kueleza kile ambacho kinamuumiza katika moyo wake. Na hapa msanii anahitaji msaada kutoka kwa watu ijapokuwa ni kuulizwa suali ili apate kueleza kile ambacho kinamthakili katika moyo wake. Haya ni mawazo ya mtafiti ambayo anayatoa kwa kulindwa na nadharia ya Mwitiko wa msomaji ambayo imempa uhuru kuichambua matini kulingana na uoni wake mwenyewe.

4.2.1.1.2 Dhamira ya Mapenzi ya Nje ya Ndoa

Msanii katika mashairi yake hakuwa nyuma katika kuyaelezea mapenzi ya nje ya ndoa. Hii ni kutokana na kwamba jamii imegubikwa na wimbi kubwa la mapenzi ya aina hiyo. Hatima ya mapenzi ya aina hii ni kuibuka kwa migogoro miongoni mwa wanandoa. Kupitia nyimbo za msanii huyu mtafiti amegundua kwamba katika wimbo wa *Mpenzi unisamehe,* amemchora mpenzi mmoja kati ya wawili hawa anamuomba radhi mwenziwe kwa kosa la kumwendea kinyume.

Hivyo alipokiri kuwa amemkera mwandani wake hakuwa na ajizi aliamua kurudi nyuma na kumuomba mpenzi wake amsamehe kwa aliyoyafanya na anakiri kuwa hatorejea tena. Ushahidi wa hili unapatikana katika ubeti wa kwanza wa wimbo huu pale msanii aliposema:-

Kama kosa nimeridhi sirudii asilani
Mpenzi naomba radhi tuishi kama zamani
Mpenzi naomba radhi tuishi kama zamani
Adhabuyo nakubali uniadhibu mwandani

Ubeti huu wa wimbo unatuonesha namna msanii alivyoteleza na kutoka nje ya ndoa yake. Msanii anaendelea kuchokonoa msimamo wake wa kutaka asamehewe na kuyajutia yale aliyoyafanya kwa kumpa nafasi bilisi (shetani) atende maovu. Ndipo alipolidhihirisha dai hili katika ubeti wa pili wa wimbo huu kwa kusema:-

Niliyotenda kwa kweli wala sikukusudia
Shetani kanisaili ndipo yakatokezea
Shetani kanisaili ndipo yakatokezea
Na sasa nimemlani akili imenijia

Haya ni mawazo ya mtafiti kwa kuchambua ubeti huu kuwa shetani alimpitia na akajisahau na kutenda yale ambayo yalimkirihi au kumkera mziwanda wake. Lakini kama wahenga walivyosema “Majuto ni mjukuu, huja baada ya kitendo”. Baada ya kutenda alichokitenda msanii aliamua kuomba radhi baada ya kuyajutia makosa yake aliyoyafanya.

Dhamira ya mapenzi ya nje ya ndoa yaliyosababisha kuombana radhi yamejitokeza tena katika wimbo wa A*kukataae hakwambii toka.* Mtafiti wa kazi hii ameigundua dhamira hii katika ubeti wa tatu wa wimbo huu pale msanii Shakila aliposema:-

Watu hutendana zaidi ya hayo
Watu hutendana zaidi ya hayo
Watu hutendana zaidi ya hayo
Watu hutendana zaidi ya hayo
Wakatukanana kupita mifano
Wakatukanana kupita mifano
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno.

Wazo la mapenzi nje ya ndoa pia limetiliwa mkazo na waimbaji wengi wa taarab akiwemo Al - watan Seif Salum. Katika wimbo wake wa *Shada la mauwa* amedokeza kipengele hiki katika ubeti wake wanne (4) wa wimbo huo anasema;

Shada kiwekwa shingoni hupendeza sawa sawa
Huvutia kwa makini kama sahani na kawa
Huvutia mashetani na majini wenye mbawa
Malaika na ruhani wote wanalitambua.

Kutokana na uoni wa mtafiti wakati wa uchambuzi wa data zake na kusaidiwa na nadharia teule ya mwitiko wa msomaji kupitia mihimili yake inayotoa fursa kwa mtafiti kuichambua kazi ya fasihi kulingana na uelewa na uzoefu wake ameona kwamba “mashetani” na majini wenye “mbawa” ni ishara tosha ya mapenzi ya nje ya ndoa. Mtafiti katika uoni wake amegundua kwamba majini ni sawa na wale wanawake au wanaume wasioweza kujituliza katika ndoa zao. Misukumo hii hutokea katika jamii pale ambapo mwanamke au mwanamme amepata kishawishi cha mtu mwengine. Mtu wa aina hiyo kuhadalika na penzi na kuanza kumtoroka mwenza wake kwa njia ya siri ili kutafuta starehe na faraja zilizo nje ya eneo. Hufanya hivyo ili aweze kukidhi kiu inayomthakili moyoni mwake.

Kwa hakika dhana ya mapenzi ya nje ya ndoa (mapenzi ya uongo/ yasio ya dhati) bado imezagaa katika jamii zetu. Hivyo ni vyema wanajamii wakaachana na tabia hiyo na kuwa na mahusiano mema hasa katika mapenzi ya ndoa ili kuweza kujenga familia bora na zenye amani. Upendo na maendeleo ya familia na taifa kwa ujumla.

4.2.1.1.3 Athari ya Mapenzi

Pamoja na uhondo, raha na starehe za mapenzi alizozionesha msanii, pia ametuonyesha athari zinazowapata wale ambao huathirika kwa mapenzi. Watu wanakumbwa na wasiwasi wa kuona kuwa wapenzi wao wanachukuliwa na watu wengine au wanapokuwa mbali nao hupata hisia kwamba wanaweza kupata

kichocheo cha kuwapelekea kuwasaliti. Mfano wa hili upo katika wimbo wa *Nimezama kwa mapenzi* pale msanii aliposema katika ubeti wa kwanza (1) mshororo wa pili:

> Naiona yangu hali mimi imedhoofika
> mimi imedhoofika

Hii ni kuonyesha athari za mapenzi ya dhati yanayotokana na mawazo yaliyomthakili msanii kila wakati kumuwaza ampendae inampelekea asitamani jambo lolote na hata kupelekea kudhofu kwa hali yake. Hali hiyo inamtokea kutokana na kukumbwa na maradhi hatari yasiyo na dawa (mapenzi). Kwa maoni ya mtafiti ni vyema mtu ajitahidi kumuomba Mungu amuhifadhi lakini mtu asimsimange aliyefikwa na maradhi haya. Hali hii ni sawa na mbio za vijiti watu huenda kwa kupokezana. Aidha, athari ya mapenzi imegunduliwa na mtafiti katika wimbo wa msanii *Nimezama kwa mapenzi* ubeti wa 6 msanii anaposema:

> Nimezama nimezama kwenye bahari ya huba
> Moyo wangu walalama nalia hitia toba
> Nimezama nimezama kwenye bahari ya huba
> Moyo wangu walalama nalia hitia toba
> Ilahi Mola karima kanepushia adhaba
> Ilahi Mola karima kanepushia adhaba

Ubeti huu unaonesha jinsi msanii anavyosikitika juu ya suala la mapenzi. Alimpenda nyonda wake bila kifani penzi lake likakosa thamani. Aliteseka na kudhalilika kiasi kwamba alidhamiria kujiua, ila aliposikiliza nasaha za wenzake kaacha kujiua na sasa anasema kuwa analia huku akitia toba. Analeta toba kwa kumuomba Allah (SW) amsamehe kutokana na dhambi kubwa aliyokuwa amedhamiria kuifanya. Haya ni maoni ya mtafiti aliyoyatoa kwa kuongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

inayotoa fursa kwa mtafiti kuwa huru kuipa matini chanzi maana kwa kadiri alivyoielewa.

Vile vile, athari nyengine ya mapenzi inaoneshwa na msanii katika wimbo wake wa *Pazia* ubeti wa tano (5) wa wimbo huo anaposema:

Mimi sitoinunua pazia ya mlangoni
Hasara ikanitia kuifua kwa sabuni
Mimi sitoinunua pazia ya mlangoni
Hasara ikanitia kuifua kwa sabuni
Tena yatia udhia iwambapo mlangoni
Tena yatia udhia iwambapo mlangoni

Katika ubeti huu msanii amekusudia kuonesha athari ya mapenzi kiuchumi. Mtafiti amegundua hili katika mshororo wa ubeti unaosema kuwa “Mimi sitoinunua pazia ya mlangoni hasara ikanitia kuifua kwa sabuni” .Kwa kurejelea nadharia ya Simiotiki katika msimbo wa kihemenitiki neno “pazia” ni mke/mume wa nje ya ndoa na neno “sabuni” ni mali ambayo anatumia mmiliki kugharimia penzi lake. Hivyo tunapata jawabu kuwa, moja miongoni mwa athari za mapenzi ni kudhoofika kiuchumi kwani mwenye kupenda haoni ingawa macho anayo hivyo anaweza kutoa kila alichonacho ili kukidhi kiu yake na ya mpenzi wake bila mahesabu mwisho anaweza kuanguka kiuchumi.

4.2.1.2 Dhamira ya Utamaduni

Chapisho la sera ya Utamaduni Tanzania la mwaka (1997) linaeleza kuwa, Utamaduni ni jumla ya mambo yote yanayobuniwa na jamii ili kukidhi utashi na maendeleo yake. Jilala (2016) anaeleza kuwa: Utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii, mtazamo wao wa mambo, na taratibu zao za kuendesha maisha

zinazowatafautisha wao na jamii nyengine. Nguzo kuu za utamaduni ni mila na desturi, lugha, sanaa, michezo na historia za jamii. Mtafiti amegundua dhamira hii ya utamaduni imejitokeza katika nyimbo za Al-anisa Shakila na mfano wa wimbo ambao unazungumzia dhamira ya utamaduni ni pamoja na wimbo usemao: *Sasambu* tangu mwanzoni mwa wimbo huo hadi mwisho unaonyesha utamaduni wa Mswahili katika mambo manne makubwa ambayo ni: Utamaduni wa kumkaribisha mgeni, utamaduni wa kumfunza biharusi namna ya kuishi maisha mapya ya ndoa. Pia nyimbo hiyo imeonesha utamaduni wa mgeni kuja na zawadi na utamaduni wa jamaaa wa bi harusi kusasambua begi.

4.2.1.2.1 Utamaduni wa Kumkaribisha Mgeni

Kumkaribisha mgeni ni kitendo cha kumpokea mgeni anaefika katika sehemu hiyo huku akiwa na azima ya kupata mapokezi mema kutoka kwa mwenyeji wake. Mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayomsaidia mtafiti kuvumbua maana isiyokwenda kinyume na matini chanzi kupitia mihimili yake amegundua kuwa dhamira hii ya kumkaribisha mgeni imetumiwa na msanii Shakila katika nyimbo zake. Mfano mzuri tunaupata katika nyimbo iliyotajwa hapo juu (Sasambu) katika ubeti wa kwanza wa wimbo huo anaposema:

Mamie mwari sokaue so kauye mgeni kangia.
Mamie mwari sokaue so kauye mgeni kangia.
Mgeni wangu weee aaee kaue mgeni kangia
Mgeni na kapu aaee kaue mgeni kangia
Mgeni na kapu aaee kaue mgeni kangia
Mgeni na sembe aaee kaue mgeni kangia.

Kwa kuongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa msanii kuhakiki kazi ya fasihi kwa kadri alivyoelewa bila kupotosha maana halisi, msanii

katika maelezo haya amekusudia kuonesha utamaduni wa kumkaribisha mgeni na hapa alikuwa anamkaribisha mama wa bi harusi ili aje ampokee mkwe wake yaani mume wa mtoto wake tayari ameshafika anahitaji makaribisho kutoka kwa wenyeji wake ili akaribie na kutekeleza azma aliyokuwa nayo. Utamaduni huu wa kumkirimu na kumkaribisha mgeni ni sifa walionao Waswahili wote jambo linalowajengea umoja, upendo na mashirikiano katika shida na raha, hasa katika kipindi kama hichi cha siku adhimu ya kuoa au kuolewa ni lazima muhusika apewe makaribisho mema yaliyojaa furaha na bashasha. Haya yanatiliwa mkazo na jopo la Wanakadiria wanaposoma qaswida yao maarufu inayoitwa *Bwana harusi, ya* kuwakaribisha maharusi inayosema:

Bwana harusii na bibi harusi karibu ingia
Bwana harusii na bibi harusi karibu ingia
Tena bila wasi ni yako nafasi tushakupokea
Tena bila wasi ni yako nafasi tushakupokea

Maelezo hayo ya kaswida yanashadidia tu namna kipindi cha harusi kilivyo, na namna maharusi wanavyoenziwa na kukirimiwa na wanafamilia na watu wote waliopo katika shughuli hiyo.

4.2.1.2.2 Utamaduni wa Kumfunza Biharusi Maisha ya Ndoa

Ndoa ni muungano wa mwanamke na mwanamme wa kuishi pamoja kama mume na mke katika misingi ya uadilifu na sheria (Quran, 4:3). Mtafiti wa kazi hii anafasiri ndoa kuwa ni mkataba wa hiari kati ya mume na mke wa kuishi pamoja kwa wema na upendo kufuatana na masharti na taratibu zilizowekwa. Mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa msomaji inayotoa fursa kwa msomaji kufasiri kwa tajiriba yake, amegundua kwamba msanii Shakila amedhamiria kuelezea utamaduni wa

kumfunza mwari au biharusi maisha mapya ya ndoa ambayo ndio kwanza anakwenda kupambana nayo. hivyo akaonelea bora kupitia wimbo wake huu wa *Sasambu* aingize dhima ya nyimbo, ambayo ni kutoa mafunzo kwa jamii. Nkwera (1978) anaeleza kwamba nyimbo ni kipengele muhimu sana cha ushairi ambacho hubeba mafudisho ya hekima na malezi ya busara katika kipindi cha maisha na malezi ya mwanaadamu.

Kwa msisitizo huu wa Nkwera, Shakila nae akaona pia katika kipindi cha kuingia katika maisha ya ndoa mafundisho ni kitu muhimu sana na ndio kupitia wimbo wake huo akafunza kwa kusema:

Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore aee
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nakupa nsomore aee
Nakupa nsomore usomore ndembo yako
Nakupa nsomore usomore ndembo yako
Nakupa nsomore usomore ndembo yako
Nakupa nsomore usomore ndembo yako
Nakupa nsomore aee

Kwa mujibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayosaidia kuwaongoza wanajamii katika maadili yaliyosahihi mtafiti anachambua na kuitolea maelezo nyimbo hii. Katika uchambuzi wake mtafiti ameona kwamba msanii alikusudia kutoa mafunzo kwa biharusi na anaposema “nataka nsomore nsonore ndembo yangu”anakusudia kusema kuwa: Nataka kutoa mafunzo kwa ajili ya mwari wangu na anaposema “Nakupa nsomore usomore ndembo yako” anakusudia kumwambia mwari wake kuwa: Nakupa elimu au mafunzo ya kumuenzi mume na kuendesha

nyumba yako katika hali nzuri ili ndoa yako iwe imara muda wote. Bila ya kuwa makini ndoa haiwezi kuwa imara. Waziri (2015) anatilia mkazo kwenye wimbo wa Singo wa wanakijiji wa Uzini usemao:

Kungwi mwambie mwario
Asiwache ufunguo
Akiwacha ufunguo
Watafungua wenziwe

Wimbo huu unakusudia kutoa mafunzo kwa biharusi kwa kumwambia kuwa ni lazima awe makini kumuhudumia mume na kumtuliza ili abakie na aendelee kuwa wake. Akishindwa kufanya hivyo na kuanza kumbeza ataanza kutoka na watu watamchukua. Haya ni mawazo ya mtafiti yanayotiliwa nguvu na nadharia ya Mwitiko ya Msomaji inayotoa fursa kufasiri kazi ya fasihi kulingana na mawazo aliyonayo mtafiti ambayo yanashabihiana na dhima aliokusudia mtunzi.

Pia wimbo huu wa msanii Shakila unakusudia kutoa mafunzo ya usafi kwa mwari wake. Hii ni kwa sababu moja miongoni mwa siri za kuongoka na kupendeza kwa ndoa ni mwanamke kuwa msafi na kumudu kujinadhifisha mwili wake na mazingira ya ndani na nje ya nyumba yake. Mke nyumbani anatakiwa atandike vyema kitanda chake na kufukiza udi ndani mwake. Maelezo hayo ya mtafiti yanaongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji yanagogotezwa na wimbo wa singo kutoka katika tasnifu ya Waziri (ameshatajwa) unaosema:

Mwari kama hafyagii
Watafyagia wenzake
Kama hatandiki
Watatandika wenzake
Na kama hafukizi
Watafukiza wenzake

Kwa mujibu wa mawazo ya mtafiti yakiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji wimbo huu unakusudiwa kutoa funzo kwa mwari juu ya mila na desturi iliyomo katika utamaduni wa waswahili. Utamaduni wa Waswahili unahimiza utamaduni wa usafi. Usafi ni moja kati ya nyenzo muhimu ya kujenga ndoa kuwa madhubuti, kuzidisha raghba na kutimiza malengo ya ndoa. Pia ni wazi kwamba mwanamke ni pambo kwa mwanamme. Hivyo wakati wote anatakiwa kuwa msafi kwa mume wake na jamii iliyomzunguka.

4.2.1.2.3 Utamaduni wa Zawadi kwa Mgeni

Zawadi ni hiba, izi au hidaya inayotolewa/inayopokelewa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwengine. Mtafiti ameligundua hili kutoka katika wimbo wa msanii Shakila unaojulikana kwa jina la Sasambu pale msanii anaposema:

Mamie mwari sokauye	Sokauye mgeni kangia.
Mamie mwari sokauye	Sokauye mgeni kangia.
Mgeni wangu weee	Aaee kauye mgeni kangia
Mgeni na kapu	Aaee kauye mgeni kangia
Mgeni na ndimwa	Aaee kauye mgeni kangia
Mgeni na sembe	Aaee kauye mgeni kangia

Katika sehemu hii ya wimbo, mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayotoa fursa kwa mhakiki kutoa maana kwa mujibu wa ufahamu wake. Msanii ameonesha utamaduni wa kutoa zawadi. Tunamuona bwana harusi ambae ndie mgeni anaetajwa katika sehemu hiyo ya wimbo kuwa kaja kwa mama mkwe wake akiwa na ndimwa ndani ya kapu pamoja na sembe. Hii ni zawadi na huu ni utamaduni hasa wa Waswahili kupeana zawadi. Hivyo kimsingi wapewaji wa zawadi wanatakiwa watambue kwamba baada ya kupewa na wao watoe japo sio kwa wakati

ule. Haya yanasisitizwa katika wimbo maarufu wa taarab asilia unaoimbwa na Al-watani Makame Faki katika kikundi cha Culture Musical Club unaosema:

Kupeana ni kikoa utoe nawe upewe
Kama huwezi kutoa cha mtu usichukue
Kupeana ni kikoa utoe nawe upewe
Kama huwezi kutoa cha mtu usichukue

Maelezo ya beti hii ya wimbo yanasisitiza na kutilia mkazo kauli ya hapo juu kuwa ubora wa zawadi ni kupeana ila watu wanatakiwa kuelewa kuwa zawadi ni chochote kupeana wasichoke.

4.2.1.2.4 Utamaduni wa Kusasambua Begi

Kusasambua begi ni kitendo cha kufungua na kutoa vitu vilivyomo katika begi la bi harusi alilokabidhiwa na mume wake. Sherehe hii kufanywa ili kumueleza biharusi matumizi na umuhimu wa kila kilichomo katika begi ili aweze kuvifanyia kazi kwa misingi ya kuilinda, kuithibiti na kuinusuru nyumba yake. Ailinde nyumba hiyo kutokana na maadui ambao wanaweza kuingia kwa mlango wowote kwa lengo la kuwavurugia ndoa yao. Mtafiti ameigundua dhamira hii ya utamaduni wa kusasambua begi katika wimbo wa msanii Shakila unaoitwa *Sasambu* kwenye sehemu ya wimbo huo inayosema:

Mwaiona sasambu sasambura nkurore
Ameileta baba sasambura nkurore
Kanga amemtilia sasambura nkurore
Zipatazo ishirini sasambura nkurore
Sabuni za kuogea sasambura nkurore
Nyingi zisizo kifani sasambura nkurore
Na nyngi za kufulia sasambura nkurore
Na zakupaka usoni sasambura nkurore
Kanzu amemshonea sasambura nkurore
Na viatu vya thamani sasambura nkurore
Kihanjifu sidiria sasambura nkurore

Na nguo zake za ndani sasambura nkurore
Hakuna kilobakia sasambura nkurore
Pete bangili na cheni sasambura nkurore
Sasambu sasambu aeeee
Sasambu sasambu sasambura nkurore
Sasambu sasambu aeeee
Sasambu sasambu sasambura nkurore
Sasambu sasambu aeeee
Sasambu sasambu sasambura nkurore
Jamani sasambu sasambura nkurore

Katika mishororo ya wimbo huu wa *Sasambu* mtafiti amegundua kuwa utamaduni wa kusasambua begi la bi harusi ni miongoni mwa dhamira zilizozungumziwa na msanii Shakila katika usanii wake. Mtafiti amelibaini hili kwa kurejelea nadharia ya mwitiko wa msomaji inayosaidia kuchambua kazi ya fasihi kutokana na ufahamu mzuri wa mtafiti. Kwa msaada wa nadharia hiyo mtafiti ameshawishika kusema kuwa msanii alilenga kutoa maana na matumizi ya kila kilichokuwemo katika begi hilo ili kumjuvya biharusi aelewe matumizi sahihi ya vitu hivyo. Matumizi bora ya vilivyomo katika begi ni miongoni mwa kitulizanisho na kidhibiti cha mume na penzi lake. Kwa hivyo msanii aliposasambua kanga, sabuni, kanzu viatu, hanjifu, bangili, cheni na nguo za ndani alikusudia kumuelekeza mwari wake kuwa atakapovitumia kama alivyomuelekeza atasitirika na kuheshimika kutokana na kuwa hivyo ni vitu vinavyomuweka mke katika ndoa. Vinamfanya awe mwenye kuvutia na kuyanogesha mapenzi kwa mume wake kwa sababu mke ni pambo la nyumba.

Pia mtafiti amegundua dhamira ya utamaduni kupitia mishororo hiyo ya wimbo wa sasambu. Msanii anaposasambua begi anaadhimisha lengo zima la kumuelezea bi harusi kuwa hicho alichokikutia katika begi yake aliyoandaliwa na mume/jamaa wa

mume ndio uwezo wao ikiwa ni kikubwa au ni kidogo apokee kwa roho safi. Waswahili wana msemo maarufu unaosema kwamba *kila ndege huruka kwa ubawa wake.* Msemo huu una maana nzito kwani kwa mujibu wa uelewa wa mtafiti ni kwamba kila mtu hufanya jambo kulingana na uwezo alionao. Kwa sababu hiyo mtu atakapolazimisha kupata asichokuwa na uwezo nacho ataingia katika matatizo yanayoweza kuharibu penzi lao na hata kuvunjika kwa ndoa yao. Haya ni mawazo ya mtafiti yakiongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji katika muhimili wake unaoangazia masuali ya kijamii.

4.2.1.3 Dhamira ya Usaliti

Usaliti ni kitendo cha kufanyiwa ubaya au kugeukwa katika jambo fulani na mtu ambaye ulijenga imani kwake (https://evockcrm.wordpress.com/2016/10/16/ malcolm-x-na-chuki-dhidi-ya-usaliti/). Dhamira ya usaliti ni moja miongoni mwa dhamira zilizooneshwa na msanii katika baadhi ya nyimbo zake zilizoteuliwa. Usaliti unajitokeza katika wimbo wa *Macho yanacheka.* Katika wimbo huu msanii amekusudia kuwaambia wanajamii kuwa kuna mtu kasalitiwa kimapenzi na mpenzi wake kiasi kwamba macho yanacheka lakini moyo unalia. Katika wimbo huu msanii alikuwa na maana kwamba “ingawa watu wanamuona yupo lakini yupo kimwili tu kiakili hayupo. Hali hii imetokea kwa sababu mtu huyu alikuwa na mwandani wake ambae kabadilika tabia kiasi kwamba hampi raha katika kuishi bali anateseka na kulia na njia kila anapofikiria mabadiliko ya tabia za mpenzi wake. Haya ni maoni ya mtafiti yanayoongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji na yanathibitika katika ubeti wa kwanza (1) msanii anaposema:-

Macho yanacheka moyo unalia

Macho yanacheka moyo unalia
Macho yanacheka moyo unalia
Macho yanacheka moyo unalia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Chozi hunitoka kwa zake tabia
Chozi hunitoka kwa zake tabia
Chozi hunitoka kwa zake tabia
Chozi hunitoka kwa zake tabia

Maneno hayo katika beti yanadhihirisha wazi usaliti aliotendewa Shakila na mwenza wake, pamoja na kumsabilia penzi lake la dhati lakini aliamua kumsaliti na kumpa taabu hivyo baada ya kusalitiwa akaamua kumwambia mwenza huyo kwa maelezo ya kumnasihi kuwa awache mwenendo wake mbovu na arejee katika penzi la dhati la habibi wake. Alimpa nasaha hizo kwa sababu anamuhurumia asije akapata taabu pindi watakapotengana anamuwasa kwa kusema:

Nenda nateseka nalia na njia
Nenda nateseka nalia na njia
Nenda nateseka nalia na njia
Nenda nateseka nalia na njia
Siku itafika kukugeukia
Siku itafika kukugeukia
Siku itafika kukugeukia
Siku itafika kukugeukia
Wajahangaika ulie na njia
Wajahangaika ulie na njia
Wajahangaika ulie na njia
Wajahangaika ulie na njia

Kwa maoni ya mtafiti beti hii ni nasaha baada ya kusalitiwa kwake anaamua kumuasa mpenzi wake kuwa maamuzi yake hayo sio sahihi. Anamuonya kwamba ipo siku ambayo mambo yatakuja badilika badala ya kulia yeye msanii aliesalitiwa kilio kitahamia kwa msaliti. Kwa muktadha huo ndio maana anamwambia siku

itafika mambo kukugeukia, wajahangaika ulie na njia. Pia mtafiti amegundua usaliti katika wimbo wa *Oh Rabbi sinipe mapenzi* pale msanii Shakila anaposema katika ubeti wa nne (4) wa wimbo huo:

> Simsahau milele kila ninapomuona
> Nakumbuka vile vile yalopita mwaka jana
> Mimi na kiumbe yule oooh
> Mimi na kiumbe yule naapa sirudi tena.

Mtafiti akiongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji anapata fursa ya kusema kuwa beti hiyo ya wimbo wa msanii Shakila inadhamiria na kushadidia namna alivyokataliwa na kusalitiwa na mpenzi wake na ndio anasimulia hivyo kwamba "Simsahau milele kila ninapomuona". Hii inaonesha kwamba Shakila alikuwa akimpenda kwa dhati mpenzi wake bila kuwa na kinyongo lakini huyu mwenye kupendwa akakosa kutambua thamani ya penzi na kumtendea mwenza wake maudhi ambayo hadi leo angekuwa hai basi angekuwa akiyakumbuka. Msanii baada ya kutambua kuwa amesalitiwa alichukua nafasi kumwambia kuwa naye basi hana haja tena na akaapa kwamba hatorudi tena katika penzi na mtu asiethamini kupendwa. Hivyo msanii Shakila alikuwa na lengo la kuwaonya wale wanaopendwa hadi wakajua lakini mwisho wakajizuzua kuwa huo sio mwenendo sahihi wa mwanadamu. Waswahili wana misemo yao maarufu yakushadidia maelezo hayo wanaposema "*Kupewa ukaringa, wajataka usipewe ukazinga au mkataa pema pabaya pamwita*". Misemo hii inatuonesha na kutuhadharisha kwamba kila anae pata au kupewa kitu kama penzi si vizuri kumsaliti anaempenda kwani anaweza kufikwa na mitihani wakati ameshaliachia penzi safi na adimu kulipata tena atabakia kuhangaika na kulia na njia.

Aidha, usaliti umejitokeza katika wimbo wa *Aloanza peke peke* msanii katika ubeti wa 4 wa wimbo huo anaposema:

Bure unatuchukia hututoki midomoni
Fitina kututilia Majumbani na kazini
Bure unatuchukia hututoki midomoni
Fitina kututilia Majumbani na kazini
Hayo ulotutendea
Hayo ulotutendea
Hayo ulotutendea yote tunayabaini

Kwenye maelezo ya ubeti huu mtafiti anaongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kupitia mihili yake amegundua usaliti ambao ulifanywa na mmoja miongoni mwa watu wa karibu wa Shakila wa kujipendekeza kwa wakubwa wa makazini kuwasaliti wenzake kwa kuwatilia fitina ili waharibikiwe. Pia alikuwa akiwafitini watu majumbani kwao ili kuwatenganisha na mabwana zao. Lakini fitina zake alizozitia kwa lengo la kuwaharibia wenzake maisha yao hazikufanikiwa kwani walijaaliwa kumgundua mapema na ndio msanii anamwambia kwamba “Hayo ulotutendea yote tunayabaini”. Msanii katika wimbo huu amekusudia kuwaasa na kuwaonya wale wote wenye tabia mbaya ya kuwasaliti wenzao kwa sababu ya maslahi binafsi. Alikuwa akiwatilia fitina katika sehemu zao za kazi na hata majumbani kwao akiwa na shabaha ya kutaka waharibikiwe. Msanii anasisitiza kuwa huo sio mwenendo unaokubalika. Iko siku siri yao itafichuka waanze kuadhirika. Hii ni kwa sababu mfitini mwenye lengo la kusaliti mwisho wake huwa sio mwema. Maelezo haya yanapata baraka katika wimbo wa kubembeleza watoto unaosema:

Ooo fitina mbaya
Ooo fitina mbaya
Mie sikai nae fitina mbaya
Mie sikai nae fitina mbaya
Hana mwisho mwema wala haoni haya
Hana mwisho mwema wala haoni haya

Kipande hicho cha wimbo kinatuonesha ujumbe kwamba huyu mfitini kwanza huwa hana haya. Mfitini huwa sio mtu mwema, hivyo watu wenye tabia hio ni wasaliti na hawafai kuigwa na ni vyema kujitenga nao. Wafitini wanatakiwa wakumbuke kwamba mwisho wao hautakuwa mwema. Haya ni mawazo ya mtafiti yakiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji akizingatia mihimili yake inayompa wasaa wa kutoa maoni yake kwa usahihi.

4.2.1.4 Dhamira ya Dini na Imani

Dini ni mfumo wa maisha ya mwanadamu. a Imani itikadi inayohusiana na mambo ya kiroho baina ya binaadamu na Mwenyezi Mungu. Kwa vile dini ni mfumo wa maisha ni jambo ambalo haliwezi kuepukwa na kila chenye kuishi. Utafiti huu umegundua kwamba, msanii Shakila katika kazi yake hii ya utunzi na uwimbaji amekwenda sambamba na mfumo halisi wa maisha. Katika uimbaji wake ameonesha dhamira ya dini na imani. Dhamira hiyo imejitokeza katika wimbo wake wa *Aloanza pekepeke* ubeti wa pili wa wimbo huo ambapo msanii anasema:

> Alitaka kututenga kutueka mbali mbali
> Shabaha aloilenga Mungu hakuikubali
> Alitaka kututenga kutueka mbali mbali
> Shabaha aloilenga Mungu hakuikubali
> Mambo yameshamtinga
> Mambo yameshamtinga
> Mambo yameshamtinga kavurugika akili

Mtafiti wa kazi hii akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayosaidia na kutoa kibali kwa kuipa maana kazi ya fasihi aliyoisoma na kuifahamu ijapokuwa maana hio itakuwa tofauti na ile iliyotolewa na mtu mwengine, amegundua kuwa

msanii Shakila alitumia dhamira ya dini. Ameitumia dhamira hiyo akiwa na imani ndani ya nafsi yake kwamba katika jambo lolote lile Mwenyezi Mungu (S.W) ndie anaetoa baraka na kulifanya jambo hilo liwe au lisiwe. Mtazamo huu unaungwa mkono na mafunzo ya Quran yanathibitisha kuwa "Allah (SW) anaposema kuliambia jambo "kuwa basi huwa" (Quran, 36:82). Msanii Shakila hakuwa mbali na mawaidha haya ndio akadiriki kusema kuwa pamoja na shabaha aliyoilenga yule kiumbe aliekusudia kuwatenganisha lakini Mungu (SW) hakuikubali nia ya muovu huyo. Kutokana na hila yake kutokubaliwa na Allampekepeke huyo kashindwa kuwaweka mbalimbali na wakabakia kuwa pamoja na mwenza wake kwa shida na raha. Hii ni imani ya dini ya kuweza kuyatambua hayo matokeo kuwa ni kazi ya Allah (SW) aliyefanya hivyo. Watu wengi ambao hawana imani ya kutambua ya kuwa kheri na shari inatoka kwa Mwenyezi Mungu, huchukua nafasi ya kuonesha kushukuru wakineemeshwa na kukufuru kila wanapo pata mtihani wa kupungukiwa na yale wanayoyahitaji (Quran, 89: 15 – 16). Kutokana na imani hii ya dini aliyonayo msanii Shakila anaamini kwa dhati kuwa mtu yoyote hawezi kuondoa kile Mungu (S.W) alichokiweka. Na hayo anayasisitiza katika ubeti wa tatu (3) wa wimbo huo huo uliotajwa hapo juu (Aloanza pekepeke). Analithibitisha hilo katika mshororo wa mwisho wa beti hiyo unasema: "Wewe utaondoaje Mungu alichokiweka". Hivyo katika maelezo hayo mtafiti anaona kwamba msanii Shakila katika wimbo huu dhamira ya dini ameitumia ili kuwaonya wale wote wenye tabia mbaya ya kuamini zaidi maarifa yao yakiwa ya kichawi au ya kishirikina badala ya kuamini Mwenyezi Mungu (SW). Anawataka washuhudie, waone, wakubali na waamini kuwa bila ya uwezo wa Allah (SW) hakuna lolote ambalo linaweza likawa kwa sababu yeye tu ndie mfanyaji na mtengenezaji wa yote. Vile vile Shakila anatuhimiza kwamba

tunatakiwa tujuwe kwamba mtu akitaka mwega wa kutegemea usiokatika amtegemee Allah (SW). Anaehitaji msaada anatakiwa aombe msaada huo kutoka kwake tu. Hivyo ndivyo anavyosema msanii Shakila kutokana na maoni ya mtafiti yaliyobarikiwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

Pia dhamira ya dini katika nyimbo za msanii Shakila inagunduliwa na utafiti huu ndani ya wimbo wa *Nimezama kwa mapenzi.* Imani hii ya dini inajitokeza katika kila mstari wa mwisho kuanzia beti ya 2 – 6 ya wimbo huu kama ifuatavyo:

2- Ilahi Mola muweza ataniafu Mwenyezi
3- Ilahi Mola karima ataniafu Rabuka
4- Ilahi Mola karima ataniafu Rabbana
5- Ilahi Mola karima ndie mwenye kuniafu
6- Ilahi Mola karima kanepushia adhaba

Katika uchambuzi wa mishororo hii ya mwisho kwa kila ubeti mtafiti akiongozwa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amegundua kuwa imani ya dini kwa msanii Shakila ilikuwepo. Kwa sababu hiyo pamoja na dhiki aliyoielezea katika wimbo huo bado alionekana kuwa na subira na matumaini ya hali ya juu ya kumtegemea Mwenyezi Mungu (SW). Alimuomba Alla aweze kumuondolea matatizo hayo huku akitarajia kupata mafanikio mbeleni. Aliyaamin sana mafunzo ya Quran yanayosema kwamba “Basi hakika baada ya dhiki faraja” (96: 5-6). Kwa wimbo wake huo Shakila ameamua kuwaasa wale wenye tabia ya kukata tamaa mara tu wanapokumbwa na matatizo. Anawasisitiza kwamba hawana haja ya kufanya hivyo bali wanatakiwa kuzidisha subira na uvumilivu huku wakiwa wanamtegemea Mwenyezi Mungu (SW). Kwa Allah (SW) hakuna lisilowezekana. Haya yanatiliwa

mkazo na msanii maarufu Fatma Issa alipoimba wimbo wake unaoitwa “Namuamini Mwenyezi” anasema:

> Anaetoa ni Mola hawezi kuingiliwa
> Akayagawa mafungu hali ya majaliwa
> Mimi akanipa langu na lako kushaekewa
> Mambo yote kwa muala kayapanga kwa murua
> Kiitikio
> Namuamini Mwenyezi Bure mtahangaika
> Namuamini Mwenyezi Bure mtahangaika
> Na wala hamuniwezi kama yeye hajataka
> Na wala hamuniwezi kama yeye hajataka

Maneno ya msanii Fatma binti Issa yanatilia mkazo kuwa mtu yoyote ni vyema kuamini kwa Mwenyezi Mungu (SW) na kuwa mwenye kusubiri kwa kila jambo. Na wale wanaokwenda kinyume basi msanii anasema ni bure wanahangaika na wala hawataweza lolote kama Allah (SW) hajataka. Mawazo ya mtafiti chini ya mwongozo wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imemuongoza kuchambua hivyo kwa kuzingatia mihimili ya nadharia hiyo.

4.2.1.5 Dhamira ya Elimu

Elimu ni maarifa anayoyapata mtu baada ya kujifunza jambo. Maarifa haya yanaweza kuwa yenye manufaa au la itategemea namna aliyepata elimu hiyo atakavyo itumia. Mtafiti wa utafiti huu wakati wa kuchakata na kuchakatua data za utafiti aligundua kuwa msanii Shakila ametumia baadhi ya nyimbo zake kuelimisha jamii. Ametekeleza dhima hiyo kwa kutoa mafunzo mbalimbali ambayo kwayo yanaweza kujenga mustakbali mzuri wa muhusika atakaeyachukua na kuyatekeleza kwa vitendo.

Mfano wa wimbo unaothibitisha dhamira ya elimu ni pamoja na; *Akukataae hakwambii toka* ubeti wa kwanza (1) wa wimbo huu unaosema:

Akukataae hakwambii toka
Akukataae hakwambii toka
Akukataae hakwambii toka
Akukataae hakwambii toka
Huona mamboye yamebadilika
Huona mamboye yamebadilika
Waweza ukae huwezi ondoka
Waweza ukae huwezi ondoka
Waweza ukae huwezi ondoka
Waweza ukae huwezi ondoka

Mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amegungua kuwa msanii Shakila katika wimbo wake huu amekusudia kutoa elimu kwa jamii. Amekusudia kuielimisha jamii kwa kuitaka itambue kuwa katika mapenzi kuna mambo mawili makubwa. Kuuwepo kwake kunaweza kuleta utulivu katika maisha ya wanaopendana hasa katika ndoa na kukosekana kwake yanaweza kuleta balaa, misukosuko na bubujiko la huzuni. Mambo hayo ni pamoja na kujitambua na kuwa na moyo wa subira. Msanii anaposema “Akukataae hakwambii toka” ana maana kwamba kila mtu katika mapenzi awe na utambuzi kuwa kuna kupendwa na kukataliwa. Kila mdau wa mapenzi anatakiwa afahamu mipaka ya vitu hivi viwili pamoja na na mabadiliko yake. Si vyema kuwa mtu anakataliwa lakini yeye akawa anapoteza muda na kashindwa kujua hadi jambo hilo linamuingiza katika madhara. Anatakiwa ang’amue mapema asisubiri mpaka akapata kipigo au balaa nyengine yoyote inayoweza kufanywa na mlevi wa mapenzi. Baada ya kugundua mabadiliko msanii anasema kuwa “Waweza ukae huwezi ondoka”, akiwa na maana kwamba mdau wa mapenzi anatakiwa awe na subira katika vitu viwili, aidha asubirishe moyo wake na aseme nao aweze kustahamili maudhi ili abakie na mwenza huyo huku

akijiliwaza kwamba “Subira huvuta kheri”. Mawazo haya pia yanatiliwa mkazo na mwimbaji maarufu wa Culture Musical Club Mtumwa Ramadhani katika wimbo wake wa *Subira* aliposema:

Kiri moyo wangu kiri
Nibora stahamili
Iwapo nitakukera
Na maudhi yakithiri
Ilazimishe subira
Subra huvuta kheri

Kwa maoni ya mtafiti wimbo huu unatoa elimu juu ya ubora wa kusubiri na kuonesha kwamba mwisho wa subra kuwa nikupatikana kwa kheri. Hata misemo maarufu ya Waswahili husema: “Subira ina malipo, subira huvuta kheri, subra ni ufunguo wa peponi, subiri kichache upate kingi na mwenye kusubiri hajuti”. Yote hii ni misemo ya Kiswahili inayoonesha umuhimu wa kusubiri. Ama kwa upande wa pili wimbo wa Shakila unaposema “*Waweza ukae huwezi ondoka*” ana maana kuwa uwe na subira ya kusema na moyo wako ukubali moja kwa moja kutengana na mwenza huyo bila kujali matokeo yake. Mara nyengine kuondoka inaweza kuwa bora kwani huenda ikawa kubakia kusubiri ikawa ni muendelezo wa migogoro na sio kupatikana kwa nafuu yoyote. Wasawhili wanasema: *kimbia kamba usijaona ng’ombe.* Sambamba na hayo msanii Shakila anaendelea kutoa elimu katika wimbo wake wa: “Aloanza peke peke” ubeti wa 3-4 anaposema:

3 Ndugu yangu jitulize bure unahangaika
Yakweli nikueleze viumbe wanakucheka
Ndugu yangu jitulize bure unahangaika
Yakweli nikueleze viumbe wanakucheka
Wewe utaondoaje
Wewe utaondoaje
Wewe utaondoaje Mungu alichokuweka
Wewe utaondoaje Mungu alichokuweka
4 Bure unatuchukia hututoki midomoni

Fitina kututilia majumbani na kazini
Bure unatuchukia hututoki midomoni
Fitina kututilia majumbani na kazini
Hayo ulotutendea
Hayo ulotutendea
Hayo ulotutendea yote tumeyebaini
Hayo ulotutendea yote tumeyebaini

Kwa kuongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti amepata fursa tena ya kugundua dhamira ya elimu iliyotumbukizwa na msanii katika wimbo huo. Shakila anazichambua beti hizo mbili akieleza kwamba ubeti wa kwanza msanii amekusudia kumuelimisha ndugu yake kuwa kazi anayoifanya si ya maana. Anamuasa aachane na kazi hiyo kwa sababu pamoja na dhambi anayoipata kutokana na kazi ya kuwafitini watu, pia viumbe wanamcheka na wala hawezi kuondoa ambacho Mungu ameshakiweka. Ama katika ubeti wa pili msanii Shakila anaamua kuvunja ukimya na kuwaambia wanajamii kuwa “Kikulacho kinguoni mwako”. Kwa muktadha huo mtu anatakiwa asiwe na imani kubwa na rafiki hata akiwa ndugu wa damu. Wakati wowote rafiki mmoja anaweza kutilia kitumbua cha wenzake mchanga. Haya yanathibitika katika ubeti wa pili wa wimbo. Pamoja na kwamba Bi Shakila amemtaja kuwa ni ndugu yangu lakini kama alivyomchora kuwa ndie huyo huyo anaewafitini majumbani na kazini. Bi Shakila amekusudia kuielimisha jamii kuwa watu wengi wanapenda ubinafsi na hawapendi maendeleo ya wenzao. Kwa hivyo ni wazi kuwa hata ndugu wa damu anaweza kumpangulia mipango ya maisha ndugu aliyezaliwa nae. Ingawa ni kweli kwamba Mungu (SW) hafichi mnafiki, lakini watu wanaweza kumgunduwa wakati ameshaacha athari ambayo haina raba ya kuifutia.

Aidha dhamira ya elimu imegunduliwa na utafiti huu katika wimbo wa *Sasambu* pale msanii anaposema:- “ Nakupa nsomoro usomore ndembo yako”. Kwa kurejelea

nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti amegundua kuwa maana yake ni kwamba anatoa elimu kwa mwari wake juu ya maisha mapya ili ndoa yake isije ikavia. Katika wimbo huu msanii alikusudia kuwaelimisha wanawake wote namna ya kuishi vyema na waume zao. Pia msanii ana kusudia kuwaeleza wazazi kuwa pindi wanapotaka kuwapa watoto wao waume/wake kwanza wawape elimu ya ndoa ili waweze kujitambua na kuweza kuishi katika maisha yaliyobora yenye kurutubishwa kwa penzi zito la bibi na bwana. Haya ni mawazo ya mtafiti yaliyoongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji.

4.2.2 Dhamira ya Tanzia (Ukiwa)

Ponera (2014:20) anaelezea kuwa tanzia ni kinyume cha ufutuhi. Hii ni mbinu ambayo mtunzi hutumia vipengele mbali mbali vizuavyo huzuni, masikitiko, jitimai na mateso kwa hadhira yake. Vipengele hivyo huweza kujengwa na mateso, ugumu wa maisha, vifungo, mabalaa kama vile njaa, gharika, kimbunga, magonjwa na ulemavu.

Kwa hivyo mtafiti anafasiri tanzia kuwa ni huzuni zinazotokana na mikosi, misukosuko na migogoro iliyomo ndani yake. Kutokana na uoni wa mtafiti wa kazi hii unaoongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayomruhusu mtafiti kujitanafasi katika kutoa mawazo yake juu ya kazi ya fasihi aliyoifanyia kazi ameigundua dhamira hii. Shakila katika kumwaga vimondo jukwaani hakuacha kuonesha huzuni aliyokuwa nayo na kueleza sababu ya hayo na alikuwa na lengo la kuiambia hadhira yake juu ya tanzia (huzuni) inayomkuta. Aliwajulisha hilo ili nao wawe na hadhari na mambo hayo. Uthibitisho wa hili ni pale msanii alipoangusha ala zake katika wimbo wa “Mapenzi ni kama donda” katika ubeti wa 1 na 3 anaposema

1. Nimechoka vumilia leo nawapasulia
   Nimechoka vumilia leo nawapasulia
   Imekuwa siku hizi kila siku ninalia
   Imekuwa siku hizi kila siku ninalia
   Nanyi hamuniulizi kipi ninacholilia
   Kwani hamuniulizi kipi ninacholilia

3. Nimempenda Fulani jina sitowatajia
   Nimempenda Fulani jina sitowatajia
   Alikuwa msikizi kila ninalomwambia
   Alikuwa msikizi kila ninalomwambia
   Kisha ni mtimizi yote nnohitajia
   Kisha ni mtimizi yote nnohatijia

Hivyo mtafiti amegundua tanzia ya msanii Shakila iliyosababisha kushindwa kujizuia na kutamka hadharani kuwa amechoka kuvumilia kadhia yake iliyotokana na mgogoro wa kimapenzi. Mgogoro huo kwa kweli umekuwa ukimkosesha raha katika maisha yake ya ndoa. Huo ni mgogoro unaomkereketa hadi kufikia kuangusha kilio kila siku. Mtafiti amegundua kuwa kadri Bi Shakila alivyoangusha penzi lake la dhati kwa nyonda (mpenzi) wake, ilikuwa ni kujisumbua na kujipotezea muda wake kwani nyonda huyo hakujali wala kutambua thamani ya penzi alilomiminiwa na mpenzi wake (Shakila). Msanii anasema kuwa hapo kabla mpenzi wake hakuwa hivyo na anatuthibitishia hili kwa maneno yake mwenyewe yaliyomo katika mishororo ya wimbo tunaouzungumzia. Shakila anafafanua kwa kusema: *Alikuwa msikizi kila ninalomwambia, kisha ni mtimizi yote nnohitajia*. Mishororo hii inakumbusha historia ya penzi zito na adimu walilokuwa nalo wapenzi hawa wawili. Ni penzi ambalo lilikuwa la bibi na bwana, la kufa na kuzikana na kila mmoja alimjali mwenzake kwa shida na raha. Bi Shakila akawa ameonja pepo bila kifo, ameshalewa kwa huba mwisho anaachishwa kwa ghafla mithili ya mtoto aliyefiwa

na mzazi wake wakati bado anahitaji kunyonya kutoka kwa mzazi huyo. Na ndio anaonesha tanzia isiyokuwa na kifani inayoambatana na kilio cha kila wakati.

Aidha, dhamira ya tanzia imegunduliwa na mtafiti katika wimbo wa Bi Shakila wenye jina la *Kifo cha mahaba* ubeti wa kwanza (1) wa wimbo huu. Katika wimbo huu msanii anasema:

Kifo cha mahaba kina idhilali
Hakina haiba wala afadhali
Kifo cha mahaba kina idhilali
Hakinahaiba wala afadhali
Bali tajikaba nifilie mbali
Bali tajikaba nifilie mbali
Bali tajikaba nifilie mbali
nifilie mbali

Katika ubeti huu wa wimbo, tunapouhusisha na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji tunaiona tanzia kwa Bi Shakila inayosababishwa na hisia na michomo mikali ya sikitiko la mahaba lililomkabili kiasi kwamba analazimika kutoa ujumbe kwa wanaopendwa kuwa wasiombe kukataliwa. Wasiombe kufikwa na balaa hii kwani wanaweza kujiua. Kifo cha aina hii kina idhilali hakina haiba wala afadhali. Pamoja na yeye kulitambua hili bado anadhamiria kujikaba na kujiua. Hivyo tunaona jinsi msanii alivyokumbwa na janga ambalo linaonesha kuwa maisha yake yako katika hatari ya kukabiliwa na kifo na kama hatakufa basi atakuwa na dhiki kubwa itakayoleta tafsiri kuwa bora kufa kuliko uhai huo.

Wasanii wengi walijaribu kuligusia suala la ukiwa (tanzia) katika kazi zao mbalimbali. Mfano kama huo tunaugundua kwa mwimbaji Fatma Issa alipokutwa na sikitiko na mgogoro wa nafsi uliomdhoofisha na kumkosesha raha ya kujichanganya na wanajamii kutokana na wao kumtenga. Pale wanajamii

walipochukua nafasi ya kumnyanyapaa na kumwagia siri na aibu zake hadharani. Mwisho akapata jawabu ya suali lake kuwa ni vyema kuwaambia wote wenye tabia hiyo mbaya kuwa haifai kwani mso hili ana lile. Maneno haya yapo katika ubeti wake wa wimbo "*Nami ni mja mwenzio*" na anasema

Nami ni mja mwenzenu hata mkinichukia
Aibu yangu ndo yenu kama mtafikiria
Nami ni mja mwenzenu hata mkinichukia
Aibu yangu ndo yenu kama mtafikiria

Hii ni kuonyesha wazi kuwa kulikuwa na jamii ya watu ilikuwa ikimuandama kwa maneno ya kashfa na masimango ambayo yalimpelekea kuvunjika moyo. Jambo hili lilimfanya kujisikia vibaya mno hadi ikampelekea kutoa ujumbe kwa kuonyesha kuwa hali hii ilikuwa inamchukiza. Aliwahadharisha waachane na tabia hizo kwa kuwaeleza kuwa aso kasoro hakuna katika hii dunia. Hivyo ni vyema kuisitiri aibu ya mwenzako na wewe usitiriwe yako. Hayo ni maoni ya mtafiti yaliyotiliwa mkazo na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ambayo huipa maana matini kupitia mkononi mwa masomaji.

4.2.2.1 Dhamira ya Ukweli na Uwazi

Mtafiti analichukulia suala la ukweli na uwazi kuwa ni ile hali ya mtu kusema neno kama lilivyo bila ya kuficha kitu au kuona aibu yoyote. Mtafiti katika kuchambua kazi hii ameigundua dhamira ya ukweli na uwazi katika wimbo wa "*Mapenzi ni kama donda"* . ubeti wa kwanza (1) wa wimbo huu msanii anasema

Nimechoka vumilia leo nawapasulia
Nimechoka vumilia leo nawapasulia
Imekuwa siku hizi kila siku nnalia
Imekuwa siku hizi kila siku nnalia
Nanyi hamuniulizi kipi nnacholilia
Kwani hamuniulizi kipi nnacholilia

Kutokana na kadhia kubwa ya kimapenzi iliyomkuta msanii Shakila aliamua kuyaweka bayana yale ambayo yaliuthakili moyo wake. Aliamuwa kuyadhihirisha yale yaliyokuwa yanafanywa na mpenzi wake. Mambo ambayo yaliyomfanya aishi katika hali ngumu na upweke kinyume na alivyotarajia. Sokomoko hilo lilimfanya atongoe maneno makali na ya uchungu ili kupunguza joto lake. Haya ni mawazo ya mtafiti yaliyopambika kwa ladha tamu iliyonyunyiziwa nadharia ya Mwitikio wa Msomaji ambayo humpa uhuru mtafiti kutoa maana kutokana na uoni wake mwenyewe. Sambamba na hilo msanii aliendelea kudadavua dhamira ya uwazi na ukweli katika ubeti wa 2 wa wimbo huu pale aliposema:-

Ni kama donda mapenzi leo nawaelezea
Ni kama donda mapenzi leo nawaelezea
Waweza funga pumzi kuzimu ukaingia
Waweza funga pumzi kuzimu ukaingia
Wala hayana mjuzi yoyote humwelemea
Wala hayana mjuzi yoyote humwelemea

Kwa uoni wa mtafiti uliopata mashiko ya nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, ubeti huu wa wimbo unaakisi dhamira ya ukweli na uwazi. Katika ubeti huu msanii ameonesha suala la mapenzi na kuonesha ugumu wake. Msanii ameamua kufananisha mapenzi na donda kutokana na maumivu makali anayoyapata. Maumivu ya mapenzi ameyamithilisha na kidonda kinachouma sana hadi mtu kushindwa kuvumilia. Mtu hujikuta anapiga kelele kwa maumivu ya kidonda hicho. Kwa sababu hii ndio msanii Shakila akaonesha ukweli kwamba maradhi ya mapenzi ni magumu mno na janga hili limefurutu ada katika maandiko ya waandishi wengi. Jambo hili limetia fora katika jamii na ni kitu ambacho hakiwezi kuepukika. Kupitia ubeti huu mtafiti amegundua kwamba mtu anapoingia katika dimbwi hili la mapenzi hana budi kukubali matokeo kwa yale yote ambayo yatakutokezea.

Mapenzi hupelekea uchizi, kuvua nguo hadharani, kutukana na watu, kutokuwa na raha au kufanya mambo ya kiajabu ajabu ilimradi tu ikapelekea jambo lisilo la kawaida. Mtafiti wa kazi hii amegundua kuwa katika ubeti huu msanii ameweka wazi suala la mapenzi ambalo amelieleza kuwa linaweza kumuingiza mtu katika majanga yasiyo ya lazima kama msanii anaposema *Waweza ziba punzi kuzimu ukaingia.* Mapenzi yanaweza kumfanya mtu akapoteza maisha kwa sababu mapenzi. Pia msanii katika kuwaelezea wanajamii ukweli na uwazi huu anawaasa kuwa katika suala hili hakuna mjanja wala mwenye akili. Yoyote humvaa na haya yanathibitishwa na mshororo wa wimbo tunaouchambua anaposema *Wala hayana mjuzi yoyote humwelemea.* Msanii anaeleza ukweli kwamba mtu anapomuona mwenzake katika hali hiyo hatakiwi kumsimanga au kumcheka kwani ni sawa na mbio za kijiti huwenda kwa kupokezana. Kwa hivyo hakuna mjuzi wa mambo hayo kwani hata hao viongozi wa ngazi za juu hufikwa na jakamoyo la huba kwa pale wanapoona ni saizi yao kuliangusha penzi. Hayo ni mawazo ya mtafiti yakitiliwa mkazo na nadharia ya mwitikio wa msomaji.

4.2.2.2 Dhamira ya Kutunza Siri

Mtafiti anafasiri neno siri kwa kusema kuwa ni jambo lililo moyoni mwa mtu ambalo halijulikani na mtu mwengine, au ni tokeo ambalo halijatakiwa kudhihirishwa kwa watu. Mtafiti wa kazi hii ameigundua dhamira ya siri alipochambua nyimbo za msanii huyu. Mtafiti ameiweka bayana dhamira hii iliyojitokeza katika wimbo wa "*Mapenzi ni kama donda***"** katika ubeti wa tatu (3) wa wimbo huu msanii anasema. "Nimempenda Fulani jina sitowatowatajia" kama ubeti huo unavyoonesha.

Nimempenda fulani jina sitowatajia
Nimempenda fulani jina sitowatajia
Alikuwa msikizi kila ninalomwambia
Alikuwa msikizi kila ninalomwambia
Kisha ni mtimizi yote nnohitajia
Kisha ni mtimizi yote nnohatijia

Mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa msomaji inayomruhusu kutoa mawazo yake binafsi baada ya kuisoma na kuifahamu kwa kina kazi ya fasihi pamoja na tofauti ya kimaana inayoweza kutolewa na msomaji/mhakiki mwengine amegundua dhamira ya kuficha siri katika beti hiyo ya wimbo wa Bi Shakia, na inadhihirika pale anna apothibitisha kwa kauli yake kuwa *nimempenda Fulani jina sitowatajia* Hii ni kuonyesha wazi kuwa kutunza siri ni jambo muhimu sana katika maisha ya kila siku, na alidhamiria kuwaonya wale wenye tabia ya kutoa siri za ndani za majumbani mwao hasa zinazohusu pendo kwa lengo la kujifakharisha kwa watu. Hivyo msanii anawataka wajifunze kutoka kwake kwani hata jina la mpenzi wake hayuko tayari kulitaja seuze siri zake za ndani. Pia anafahamisha kuwa ni vyema kutunza siri za mkaribu wako ili na wewe ukatunziwa za kwako. Haya yamebainishwa na mwanamuziki wa taarab asilia Alwatan Othman Soud katika wimbo wake wa "*Sina haja ya mwenzako"* pale aliposema:

Sina haja ya mwenzako wewe ni saizi yangu
Changu mimi ni chako na chako ni changu

Hii inaonesha kuwa kwa vile wamesabiliana nyoyo na kukabidhiana vilivyofichikana hivyo ni kila mmoja abebe shida na raha za mziwanda wake kwa kutunziana siri ili wabaya na maadui wa wapendanao wasipate njia ya kuja kuwaharibia ndipo mapenzi yao yanaponoga na kuweza kuwaweka wapenzi hawa kuwa katika ulimwengu wa wapendanao, kwa lugha nyengine tunaweza kusema

kuwa katika pepo ya dunia. Aidha dhamira ya siri imegunduliwa na mtafiti ndani ya ubeti wa pili wa wimbo huo unaoeleza kuwa:-

Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Usinidhihaki la kweli nambie
Usinidhihaki la kweli nambie
Kama hunitaki kheri nitulie
Kama hunitaki kheri nitulie
Kama hunitaki kheri nitulie
Kama hunitaki kheri nitulie

Kwa maoni ya mtafiti yanayoongozwa ni nadharia ya mwitikio wa msomaji inayotoa fursa ya msomaji kuifasiri matini kulingana na uzoefu na ufahamu wake mwenyewe ubeti wa wimbo unaonesha dhamira ya kutunza siri inayoashiriwa na historia refu ya maisha ya wapenzi hawa wawili kwani msanii akiwa ni mmoja wa wapenzi hao anaonesha kwamba katika penzi lake kuna mabadiliko na mwenza wake anaonesha kuwa ana usiri mkubwa juu ya matendo anayomtendea mwenzake ila Shakila analigundua hilo na anamwambia "*Usinidhihaki la kweli niambie"* hivyo mshororo huu unagogoteza usiri wa mwenza wake na kudhihirisha kwamba hakuna siri hasa katika suala zima la mapenzi kwani mapenzi yakinogea kwa dhati kabisa kila muhusika atalitambua hilo kwa sababu lina viashiria vyake na hivyo hivyo linapoyonga (linapoharibika) ndio rahisi zaidi kuligundua kwani utayapokea mabadiliko ambayo hayakuwemo katika penzi lenu hapo kabla. Dai hili linatiliwa mkazo na mwimbaji / msanii Makame Faki - wa Culture Musical Club na wimbo wake wa **"** *Mazoeya yanatabu"* ubeti wa tatu (3) wa wimbo huo anagundua siri ya kukataliwa na mwenzake na anamwambia:-

Usiku kucha silali nikaavyo nakuona

Imeniruka akili hukwita kwa lako jina
Kumbe ni chako kivuli mwenyewe sinawe tena

Maneno haya ya masnii Makame Faki yanaonesha msisitizo na mgogotezo wa utokaji wa siri uliosababishwa na mabadiliko ya kimajonzi kwani msanii huyu anaashiria kuwa alikuwa na mweza wake lakini kila alivyojitahidi kuwa pamoja na kumsogeza karibu, yeye hakuwa na habari naye, kumbe alikuwa yupo kimwili tu kiakili yuko kwa mwingine.

Nadharia ya Simiotiki inatufumbulia fumbo la msanii anaposema ***"****Kumbe ni chako kivuli mwenyewe sinawe tena"*. Hivyo nikwamba nyonda huyu akili, maarifa, utii na mapenzi yote ameshamsabilia bwana mwengine na kwa Al-watani Makame Faki amebakia tu sio kwa suala la mapenzi. Haya ni maneno ya mtafiti yanayoungwa mkono na nadharia ya Simiotiki.

4.2.2.3 Dhamira ya Malezi na Huruma

Malezi ni njia moja wapo ya ukuzaji na uimarishaji wa mtu au jambo au kitu kwa kutarajia (mtu yule au kitu kile) kufuata tabia fulani zinazopendelewa na mlezi. Dhamira ya malezi imegunduliwa kuwa ni moja kati ya dhamira zilizokusudiwa kuoneshwa na msanii. Dhamira hii inapatikana katika wimbo wake wa ***"****Sasambu"* pale msanii aliyosema:

Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu

Kwa mawazo ya mtafiti yanayoongozwa na nadharia ya Simiotiki inayofanya kazi ya kufumbua fumbo na fumbuzi za kifasihi, msanii amebainisha dhamira hii ya malezi

na huruma. Katika ubeti huo tunaoneshwa kuwa hata mtoto ukimuona kaoa au kaolewa lakini kwa vile bado ana wazazi wake huyo hakuwi na kila wakati anahitaji kuelekezwa katika mustakabali nzuri wa maisha ili katika safari zake asije akaharibikiwa. Kwa kuwepo ukweli huu ndipo msanii akachukuwa nafasi kumfunza biharusi wake kwa kumpa wasia mwema wa kimalezi na huruma ili asije kuwatukanisha wazazi wake kule aendako.

Msanii anaposema "nataka nsomore nsomore ndembo yangu" ana maana kwamba anataka kutoa elimu ya malezi itakayomwezesha mwari wake kuwa na maisha ya amani endapo atafuata mafunzo hayo. Anataka mwari wake awe mtu wa mfano katika sehemu ambayo atafikia. Vile vile suala la malezi na huruma, limegunduliwa na mtafiti katika wimbo wa msanii Shakila pale anaposema "*Macho yanacheka"* ubeti wa kwanza wa wimbo huo kama ifuatavyo:-

Macho yanacheka moyo unalia
Macho yanacheka moyo unalia
Macho yanacheka moyo unalia
Macho yanacheka moyo unalia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Chozi hunitoka kwa zake tabia
Chozi hunitoka kwa zake tabia

Mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji anapata fursa ya kutoa maoni kwa kadri alivyoona. Katika beti hii ya wimbo msanii anaonesha huruma inayotokana na mapenzi ya dhati. Anashindwa kustahamili, anamuhurumia mziwanda wake hadi machozi yanamtoka. Hii ni kutokana na nafasi aliyopewa bwana huyo na msanii Shakila ya kumpenda kiasi kwamba hakuwa tayari kumkosa kwa hali yoyote. Anamuhurumia, anamuengaenga, anamkubali kwa hali zote. Lakini

pamoja na mazuri yote msanii anayomtendea, bado mpenzi wake hanasihiki wala hasemezeki. Anamzidisha vitimbi ambavyo havimpi raha ya maisha wala havimpi raha ya kudumisha penzi la dhati kama kwamba hakuna ulazima wa mwanaume kuangusha, kudhibiti na kumimina penzi zito kwa wake zao. Wanaume pia wanatakiwa kuwa na huruma kwa wanawake/wake zao au hata kwa watu wengine wawe wa ndani au nje ya familia. Kama tunavyojifunza katika diwani ya "*Malenga Wapya"* shairi la (17) lijulikanalo kwa jina la *Nini wanangu* mwandishi anabainisha na kuthibitisha hayo anaposema:-

> Niwape nini wanangu, mupate kufurahika?
> Sina kitu kilochangu, vazi langu ni mashaka
> Wamehodhi ndugu zangu, shida mimi kunyanyuka
> Musidhani nawakhini!
>
> Nifanye nini wanangu, nanyi mupate ongoka?
> Taabani hali yangu , nastahili sadaka
> Huniingia uchungu, kiwaona mwateseka
> Lakini nifanye nini!

Maelezo ya beti hizi yanathibitisha na kugogoteza namna baadhi ya wanaume wanavyokuwa na huruma kwa familia zao. Msanii kalidhihirisha hili katika beti hizo na anaonesha huruma na masikitiko kwa watoto wake ambao anawajutia kutokana na madhila na mateso wanayoyapata huku akiwa hajui namna ya kuwasaidia. Hayo ni mawazo ya mtafiti yaliyotiliwa nguvu na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika muhimili wake unaotoa fursa kwa msomaji kutoa maana ya kazi aliyoisoma kwa kadri alivyoifahamu. Kwa kweli beti hizo za ushairi unaoitwa *Nini wanangu* zimedhihirisha kwamba baadhi ya wanaume wanakuwa na huruma, na zinawaasa wote wale wenye tabia ya ukatili kuachana nayo na kuwa na upendo wa dhati na huruma kwa jamaa zao na kwa jamii yote kwa jumla.

Aidha dhamira ya malezi na huruma imegunduliwa na mtafiti katika wimbo wa msanii Shakila unaosema *Mpenzi unisamehe.* Ubeti wa kwanza wa wimbo huo msanii anaposema:-

> Kama kosa nimeridhi sirudii asilani
> Mpenzi naomba radhi tuishi kama zamani
> Mpenzi naomba radhi tuishi kama zamani
> Adhabuyo nakubali uniadhibu mwandani.

Kwa maneno ya mtafiti yanayoongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayotoa fursa kwa msomaji kujua kazi ya fasihi aliyoisoma kwa mujibu alivyoelewa yeye mwenyewe, ubeti huu wa wimbo unaonesha malezi mazuri aliyolelewa Shakila na wazazi wake. Katika beti hiyo tunamuona Shakila amefunzwa kuomba radhi baada ya kufanya kosa na kufunzwa namna ya kuwa na subira kwa adhabu yoyote atakayoamuliwa kupewa na aliyemkosea lakini anahitaji kusamehewa. Msanii Shakila katika uibuaji wa dhamira hii anakusudia kuwaonya wale wenye tabia ya kuwakosea wapenzi au watu wao wa karibu baadae wakashindwa kuomba radhi. Anakusudia kutufahamisha kwamba silka hiyo haimo na haitokani na walezi wema bali inatokana na shetani na hawatokirithisha kizazi kijacho mila na desturi nzuri zinazotokana na malezi mema. Kwa muktadha huo, Shakila anawataka watu wabadilike ili kukiokoa kizazi na majanga. Haya yanagogotezwa na semi isemayo: akiongoka/akielimika mwanamke mmoja imeelimuka jamii. Hivyo tutambue kwamba elimu ni pamoja na yale mafunzo yanayopatikana katika malezi.

4.2.2.4 Dhamira ya Anasa na Starehe

Miongoni mwa dhima za fasihi, ni kuburudisha. Dhima ya kuburudisha inapelekea anasa na starehe kwa fanani na hadhira. Mtafiti katika nyimbo za msanii Shakila ameligundua hili katika wimbo wake wa "*Mkuna na Mkunwaji"*. Wimbo huu unaowaonesha wanamuziki, wa muziki huu wa taarab wakilisakata rumba na kuonesha starehe na raha zilizowaingia katika roho hadi kuona kwamba bado hawajafikia kiwango cha kujishebeduwa, kujibenuwa na kujionesha kwa waliojaa, haya yameshadidiwa na maneno ya wimbo huo unaosema:-

> Ngoma bila kulewa nitaichezaje mie
> Ningekuwa na pesa ningelewa tilatila
> Ningekuwa na pesa ningelewa tilatila
> Ningekuwa na pajero ningelewa tilatila

Kwa mawazo ya mtafiti yakiongozwa na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji inayotoa fursa kwa msomaji/mhakiki kuifasili kazi ya fasihi ingawa atatofautiana na maana za wasomaji/wahakiki wengine, ubeti/kimalizio hiki cha wimbo **kinamaanisha** kwamba wanamuziki na wapenzi hawa wa taarab asilia waliingiwa na anasa na starehe kubwa. Starehe na anasa ziliwazidi hadi wakaanza kutamani kuiongeza nishai kwa kutumia ulevi. kwani walihisi kuwa watakapolewa watastarehe zaidi na kuweza kutenda matendo ambayo kama mtu atakuwa na akili zake timamu hatoweza kutenda matendo ya aina hiyo. Matendo waliyokusudia kuyafanya ni kama vile kutukana, kuvua nguo, kukumbatiana na kubebana hadharani na hata kukata viuno wakiwa wamenyanyua nguo zao juu ili kuonesha nyeti zao na kumwaga radhi. Kwa kuwa msanii anasema, *Ningekuwa na pesa ningelewa tilatila* katika mshororo huo hapo juu ni wazi kwamba hawakufikia katika lengo la starehe yao kwa sababu

hawakuwa na pesa za kulewea. Haya yanashadidiwa na nadharia ya Mwitikio wa Msomaji.

4.2.2.4.1 Dhamira ya Umalaya

Umalaya ni mwenendo wa baadhi ya wanaume au wanawake kuingia katika matendo ya uasharati na kuwa wazinifu au wazinzi kwa kuuza miili yao kama ni sehemu ya ajira yao au vyenginevyo. Mtafiti amegundua kuwa msanii amezungumzia maswali ya umalaya kupitia baadhi ya nyimbo zake. Kwa mujibu wa data za utafiti huu, dhamira ya umalaya imeoneshwa na msanii Shakila katika wimbo wake unaoitwa *Hujui alacho kuku* katika ubeti wa kwanza wa wimbo huo anaposema:-

> Hujui alacho kuku usingempa mgeni
> Wala kufanya shauku kumsifu hadharani

Kwa mawazo ya mtafiti yanayoongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kupitia muhimili wake wa kutoa fursa kwa msomaji kufasiri apendavyo kwa mujibu wa uelewa wake. Shakila analenga kuikosoa jamii ya baadhi ya watu wenye tabia mbaya ukiwemo umalaya hasa kipindi hiki kinachokwenda sambamba na maradhi hatari ukiwemo UKIMWI. Sehemu hiyo ya wimbo inamlenga mwanaume aliyediriki kumsifu mwanamke mrembo ambae hakuwa ndani ya ndoa yake, baadae akagundua kuwa mwanamke yule ni kiruka njia (malaya). Msanii anasema katika mshororo wa kwanza *hujui alacho kuku usingempa mgeni*. Hapa msanii ametumia mbinu ya ishara kwa kutaja kuku, ndege ambaye tabia yake ni kuchakurachakura na kudonoa donoa kila kitu bila kutosheka. Kwa mantiki hiyo msanii Shakila amemtumia ndege huyu akiashiria mwanamke malaya mwenye tabia ya kujiuza mwili wake na

kujipeleka kila sehemu ambayo biashara yake itapata soko ili tu yeye apate mali na hela zitakazomuwezesha kuishi.

Sambamba na hilo, mtafiti amegundua kuwa msanii Shakila kupitia katika wimbo tunaoujadili amechukua nafasi kuionesha jamii kuwa suala la umalaya pia lipo kwa wanaume na anawaasa kwa kuwaambia kuwa:-

Ni welewako mwajimbo usojua vya thamani
Kuku atazua jambo nakuona taabani
Utakula na utumbo kama si leo mwakani

Kwa kutumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, mtafiti anaona kuwa msanii anakusudia kuwaonya wanaume wote wenye tabia ya kuwapa hadhi wanawake wa nje na kuwadogosha wale walio ndani ya ndoa zao. Shakila anawataka wanaume wa aina hii waewe na tahadhari na balaa mbalimbali zinazoweza kusababishwa na uasharati. Haya yanashadidiwa na Bi Shakila katika mishororo ya wimbo huu huu anaposema:-

Kisikuhadae kiga kwa mnofu na laini
Akili ukavuruga ukawa ni afukani
Ola kidari na bega nyama imahali gani

Katika ubeti huu wa wimbo, mtafiti anachambua kwa kusema kuwa msanii aliendelea kuwaonesha wanaume madhara ya umalaya na ametumia neno kiga, kiungo nyeti katika viungo vya kuku chenye mnofu na mafuta ambayo yanaweza kumuathiri mlaji. Kiungo hiki kimetumiwa na msanii kumuwakilisha mwanamke wa nje ambaye pamoja na kuonekana kwake mzuri na mrembo wa kuvutia lakini anaweza akawasababishia matatizo mbalimbali kama vile UKIMWI na magonjwa mengine ya uasharati na hata umasikini. Pia msanii ametumia neno *kidari na bega* ambavyo ni viungo dhaifu vya kuku na havina mafuta na kwa mustakbali huo havina

madhara kwa watumiaji. Kidari na bega katika wimbo huu vimetumiwa na msanii kumuakilisha mwanamke wa ndoa ambaye ingawa anaonekana dhaifu na bwana wake lakini yuko safi na hawezi kumsababishia madhara. Hivyo msanii anatoa wito kwa wanawake na wanaume wautambue na waufanyie kazi msemo unaosema *kibaya chako si chema cha mwenzako.* Haya ni maoni ya mtafiti yanayoungwa mkono na nadharia ya Simiotiki sambamba na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

4.2.2.5 Dhamira ya Ukombozi

Ukombozi ni kitendo cha kubadilika kutoka katika hali duni ya maisha na kuingia katika hali nzuri ya maisha katika nyanja za kiuchumi, utamaduni, siasa na kijamii. Katika nyimbo zilizochunguzwa imebainika kuwa dhamira ya ukombozi imejitokeza katika hali mbili ambazo ni ukombozi wa kisiasa na ule wa kifikra.

4.2.2.5.1 Ukombozi wa Kisiasa

Ukombozi wa kisiasa ni kitendo kinachompelekea mtu kuwa huru na kufanya mambo yake yote ya kisiasa akiwa na mamlaka kamili. Mamlaka ya kujiamua na kutekeleza mambo yake bila masharti, chuki wala vitisho kutoka kwa wengine.

Khatib (1992) alifafanua kwamba nyimbo hapo kabla zilitumika kama chombo cha anasa na starehe tu. Hivi sasa nyimbo zimechukua mwelekeo mpya wa kuraghibisha umma katika kujenga nchi na kuzungumzia mafanikio yaliyofikiwa na nchi hizo.

Bi Shakila analithibitisha hili katika baadhi ya nyimbo zake. Bi Shakila anaonesha wazi kuwa alikwenda katika mustakbali wa mahitaji na sio utashi binafsi. Bibi huyu alikuwa anakwenda na wakati kwa kuimba nyimbo zilizohusu masuala ya ukombozi wa aina mbalimbali ukiwemo wa kisiasa. Kwa kukamilisha azma hiyo. Bi Shakila

alizungumzia jambo la kuzikomboa nchi zote za Afrika. Alizungumzia ukombozi wa nchi ambazo zilikuwa bado hazijapata uhuru. Pia aliimba nyimbo za kuwapongeza mashujaa na viongozi waliokuwa mstari wa mbele kupambana na wakoloni na wale wote ambao hawakuwa na nia njema katika kupeleka nchi za Afrika kwenye mafanikio. Katika wimbo wake *"Viva Frelimo"* Bi Shakila anachukua nafasi kumpongeza Shujaa wa Msumbiji Rais Samora Machel baada kufanikiwa kuikomboa Msumbiji iliyokuwa chini ya dola ya Mreno kwa kusema:-

Leo twakuvika taji mpendwa baba Samora
Kukomboa Msumbiji si jambo la masihara
Mreno kafa maji hivi sasa kadorora

Kwa maoni ya mtafiti yakiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa msomaji kutoa maelezo binafsi kutokana na kazi ya fasihi aliyoisoma msanii Shakila anaonesha kuwa Msumbiji ilikuwa huru chini ya Rais Samora ambae amevikwa taji kuashiria kupatikana kwa uhuru wa nchi ya hio. Uhuru ambao ulitokana na jitihada ya nchi nyingi za Afrika ikiwemo Tanzania. Haya yanapata baraka za msanii Shakila anaposema:-

Msumbiji kukomboka sisi twaona fakhari
Fakhari ya Afrika kwenye bara na bahari
Samora unaposhika waondoe mabepari

Hivyo msanii kwa kutumia maneno ya mishororo hii miwili ya mwanzo, mtafiti amepata fursa ya kugundua kuwa upendo, umoja na mshikamano uliokuwepo ndani ya Afrika ndio iliyokuwa silaha pekee ya kuung'oa ukoloni na kupatikana kwa uhuru wa nchi hizo. Mtafiti kwa anavyoona itakuwa ni jambo jema kuendeleza mahusiano na kuwa na msimamo kwamba historia ya Afrika haitajirejea tena. Suali hili linasisitizwa pia na kuungwa mkono na Khatib (2003) aliposema kupitia kitabu

chake cha *Wasakatonge* kwenye shairi lililopewa kichwa cha habari “Hatukubali”. Wazo la ukombozi linapatikana kwenye ubeti wa nne (4) wa shairi hilo unaosema:-

Hatukubali tena
Kutuletea usultani
Kutuletea na ukoloni
Kutuletea na uzayuni
Hatukubali katu
Ndani ya nchi yetu
Iliyo huru

Kwa maoni ya mtafiti ubeti huu wa ushairi unalenga kuwaonesha Waafrika wote kwa jumla kuwa Afrika ni huru hivyo waendelee kuwa na umoja ili ukoloni usirejee tena. Haya ni mawazo ya mtafiti yakiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa msomaji.

4.2.2.5.2 Ukombozi wa Kifikra

Dhana ya ukombozi wa kifikra si dhana mpya kwani imeelezwa na Kanyuma (2008) kuwa ni mabadiliko yanayotokana na elimu sahihi inayomuwezesha mtu kujitambua na kufahamu haki zake za msingi. Mtafiti anaifasiri dhana hii kuwa ni mwamko anaoupata mtu kutokana na elimu aliyofunzwa au kujifunza kutokana na matokeo yanayofanyika katika mazingira yaliyomzunguka. Ni aina ya ukombozi unaomuwezesha mtu kuweza kuelewa yaliyo ya haki na yasiyo ya haki. Mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa msomaji anapata fursa ya kuigundua dhamira hii ya ukombozi wa kifikra kupitia katika nyimbo za msanii Shakila akiwaasa wanajamii kujitambua hasa katika suala zima la kupendwa na kukataliwa.

Msanii ametumia wimbo wake wa *Mapenzi ni kama donda* kuwazindua watu kuhusu upya na ukongwe wa mapenzi yao. Msanii ametumia tashbiha kushabihisha mapenzi

na donda kwa sababu mapenzi yanapokuwa mapya huwa na starehe na hamu kubwa kwa wapendanao na kila wakati wapenzi hao huwa pamoja wakiwa karibu au mbali.

Ukongwe wa mapenzi hupelekea shabuka, vituko na migogoro isiyokwisha katika maisha ya wapendanao na hatima ya hilo kila mmoja huwa hana hamu ya mwenzake. Sambamba na hilo upya wa donda huwa linapendeza kwa mmiliki kila wakati analisugua, analichezea na kulishughulikia kwa usafi na dawa lakini likiwa la muda mrefu hupoteza mwelekeo kwa muhusika na kuachana nalo.

Hivyo msanii alipowasilisha wimbo huu *Mapenzi ni kama donda* alidhamiria kuwaasa wanajamii kuwa penzi kila siku linaweza kuwa jipya kwa wale wenye kupendana hivyo waendelee kulienzi na kulikumbatia. Lakini litakapochakaa na kuanza kuleta athari basi waachane nalo kama linavyoachwa donda wakati linapokuwa la muda mrefu ingawa inauma. Haya yanashadidiwa na beti ya msanii Shakila katika wimbo huu wa *Mapenzi ni kama donda* kwa kusema:

> Ni kama donda mapenzi leo na waelezea
> Ni kama donda mapenzi leo na waelezea
> Wawezafunga pumzi kuzimu ukaingia
> Wawezafunga pumzi kuzimu ukaingia
> Wala hayana mjuzi yoyote humwelemea
> Wala hayana mjuzi yoyote humwelemea

Hivyo ndivyo yalivyo mapenzi. Msanii Shakila aliona kwamba, ipo haja ya kuwatanabahisha wanajamii wote kwa kuwataka wawe na utambuzi utakaowapelekea kujifahamu katika penzi lao kabla hawajafikia kuziba pumzi wakaingia kuzimu. Msanii anawataka wanajamii wajue kwamba kuna mabadiliko na changamoto zitakazotokezea katika motifu ya safari yao ya kuogelea na kupiga mbizi

ndani ya bahari ya mapenzi. Wanatakiwa wafahamu kwamba, upepo unaweza kuvuma ukawaepesisha safari kwa kutoa msukumo wa chombo, lakini wakati mwengine upepo unaweza kugeuka na ikawa sababu ya kutota kwa chombo hicho cha kuwavusha wawili hawa katika bahari ya huba. Kwa mantiki hiyo kila mmoja anatakiwa atambue viashiria vya kuharibika kwa safari ili iweze kuwa rahisi kuvaa koti la kuokolea maisha, kutumbukiza mizigo ndani ya maji na kujiachia huru kuiokoa nafsi.

Aidha dhamira ya ukombozi wa kifikra imegunduliwa na mtafiti katika wimbo wa Shakila unaoitwa *"Akukataae hakwambii toka"*, ubeti wa pili wa wimbo huo msanii anasema:

Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Usinidhihaki la kweli nambie
Usinidhihaki la kweli nambie
Kama hunitaki kheri nitulie
Kama hunitaki kheri nitulie
Kama hunitaki kheri nitulie
Kama hunitaki kheri nitulie

Katika ubeti huu wa wimbo mtafiti akiongozwa na nadharia ya mwitiko wa Msomaji inayompa mtafiti fursa ya kuichambua na kuipa maana kazi ya fasihi kwa kadri ya uwelewa na uzoefu wake mwenyewe, mtafiti amegundua kwamba Shakila amekusudia kuwaonesha njia watu ambao pamoja na maudhi wanayofanyiwa na wenza wao bado hawatambui kuwa wanakataliwa na wanafukuzwa kistaarabu. Kwani kumuondoa mtu katika himaya yako sio lazima kumtamkia kwa mdomo bali inawezekana ikawa ni pamoja na kumfanyia maudhi hadi akachokana nayo akaamua

kuondoka kwa hiyari yake (vitendo vinasema zaidi kuliko maneno). Lakini hata hivyo msanii aliona kwamba wapo ambao hata wakifanyiwa maudhi kupitilia kiwango bado wanashindwa kung'amua kuwa wanakataliwa na wanatakiwa waondoke hivyo wanabaki kukoperwa na kusemwa na weledi wa mambo wanaoshuhudia yale wanayofanyiwa na wenza wao. Haya yanathibitishwa na mwana taarab asilia Khadija Yussuf katika kikundi cha Melody cha Zanzibar kupitia wimbo unaoitwa *"Mambo yamekushinda"* ubeti unaosema:-

> Aibu mwenzangu aibu na ari ya kike huna,
> Usijitie pambani hujui kukataliwa
> Mwenzanzangu mambo yamekushinda
> Mwenzanzangu mambo yamekushinda

Beti hii ya wimbo inamuwasa mwanamke ambae tayari alishafanyiwa maudhi na mpenzi wake lakini bado anajitia huku na kujitoa huku, hivyo msanii akachukua nafasi kumkomboa kifikra kwa kumwambia kuwa iliyomfika ni aibu wala hana ari ya kike na anajitoa fahamu kwa kujitia pambani na wala hajitambui kuwa anakataliwa. Hivyo kwa mujibu wa maoni ya mtafiti yanayotiliwa nguvu na nadharia ya Mwitiko wa msomaji ni wazi kwamba mwanamke huyu alikosa kujitambua hivyo wale wanaohitaji kusaidiwa na msanii waweze kutambua kuwa akukataae hakwambii toka hivyo utakapoona mamboye yamebadilika uanze kujiyayarisha kwa safari au kama utabakia basi utambue kuwa upo tu sio kwa ajili ya mapenzi.

4.2.2.6 Dhamira ya Ulinzi na Usalama wa Nchi

Kwa mujibu wa Khatib (2003) suala la ulinzi na usalama ni muhmu katika kujenga na kuimarisha maendeleo ya nchi kwani bila ulinzi kukamilika nchi inaweza kuvamiwa na kuanza kuyumba katika nyanja zote za maisha. Bi Shakila katika kazi

zake pia amelizungumzia jambo hili la ulinzi na usalama na kuliwekea msisitizo wa hali ya juu katika wimbo wake wa *Viva Frelimo.* Katika ubeti wa nne wa wimbo huo, msanii anaposema:-

> Tanzania imara, sisi tumeshajiweka
> Kwenye bahari na bara, tuko tayari kufika
> Tutawanyoa vipara, kwa harubu na shabuka

Kutokana na maelezo hayo, mtafiti akiongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji amegundua kwamba msanii Shakila alikuwa tayari kujitolea muhanga katika suala zima la ulinzi na usalama wa nchi dhidi ya uvamizi wa watu wasioitakia mema Afrika. Pia beti hiyo inafanya kazi ya kuwaasa wale wote wasio na uzalendo ambao wanashindwa kujitolea muhanga katika kudumisha amani ya nchi na maendeleo yake, wafanye mabadiliko katika nafsi zao kwani Waswahili husema “mjenga nchi ni mwananchi” na maendeleo ya nchi yanaletwa na wananchi wenyewe. Bi Shakila ametuchorea ishara ya bara na bahari akiwa na maana ya kuwaasa Watanzania kuwa tayari kuwaondoa na kuwazuia wakoloni na hata wavamizi wa aina yoyote ile popote watakapokuwa barani Afrika. Pia msanii anakusudia kutuambia kuwa ili kufikia katika malengo ni lazima tuwe imara na utayari ili kushinda mapambano ya aina yoyote, na iwe ngome ya kuzuia ukoloni usirudi tena katika ardhi ya Afrika.

Sambamba na hayo katika wimbo huu wa *Viva Frelimo* mtafiti amegundua dhamira ya ulinzi na usalama ambayo inawaasa wananchi kuwa, pamoja na uhuru uliopatikana bado nchi za Afrika zinakabiliwa na wimbi kubwa la walaji rushwa na wabadhirifu wa mali za umma ambao kila siku wanaigharimu Serikali na kuisababishia mzigo mkubwa wa madeni na kudumaza uchumi wa nchi. Hivyo

msanii Shakila anawataka watu wote wawe raia wema, waaminifu na wazalendo kwa nchi zao vyenginevyo wataendelea kuishi Afrika (Tanzania) iliyogubikwa na migogoro ya wenyenavyo na walalahoi, wasiokuwa na uhakika wa lini wataokoka na shida iliyowakabili.

Omar katika diwani ya *Malenga Wapya* (2001:49) shairi lake la 31 anashadidia hili kwa kusema kuwa:

> Mpaka lini dhiki hii itafishwa
> Hadi lini mnyonge atadunishwa
> Jambo hili halina budi kukomeshwa
> Mpaka lini tutasemewa

Kwa maoni ya mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa msomaji anapata fursa ya kumuona mwandishi wa shairi hili kuwa anaunga mkono maelezo ya msanii Shakila ya kuwaasa watu wawe macho katika ulinzi na usalama ili kuondoa utabaka uliokithiri na kupunguza manung'uniko ya wasonacho kwa kuipunguzia serikali mzigo wa madeni yasiyo ya lazima ili iwe rahisi kuwatupia jicho na wale wote wenye hali ya duni ya maisha.

4.2.2.7 Dhamira ya Maendeleo ya Kiuchumi

Manzi (2007) anaeleza kuwa maendeleo ni mabadiliko ya mtu kutoka katika hali duni na kuingia katika hali nzuri katika nyanja zote za maisha (Ty). Suala la maendeleo sio geni kwani limekuwa likipigiwa kelele na watu mbalimbali. Miongoni mwa waliolizungumzia suali hili ni msanii Shakila Msanii huyu ameona kuwa kukuwa kwa maendeleo ya mtu ndio kukuwa kwa maendeleo ya jamii na taifa kwa jumla. Suala la maendeleo ya kiuchumi katika nyimbo za Shakila limegunduliwa na

mtafiti katika wimbo wa "*Pazia*" ubeti wa tano wa wimbo huo ambapo Shakila alisema:-

Mimi sitonunua pazia ya mlangoni
Hasara ikanitia kuifua kwa sabuni
Mimi sitoinunua pazia ya mlangoni
Hasara ikanitia kuifua kwa sabuni
Tena yatia udhia iwambapo mlangoni
Tena yatia udhia iwambapo mlangoni

Ubeti huu wa wimbo, kwa mawazo ya mtafiti yakiongozwa na nadharia ya Simiotiki katika msingi wake wa kimatokeo ambao visa na matukio huwekwa kimsimbo, mtafiti amegundua kuwa msanii anapotaja neno *pazia* anakusudia mwanamke/mwanamme wa nje, hivyo anapoelezea kuwa *Mimi sitoinunua pazia ya mlangoni* ana maana kuwa yeye hatakuwa tayari kumiliki mwanamme wa nje (mbuya). Anakataa kufanya hivyo kwa sababu anafahamu kwamba, kuwa na mtu kama huyu kulingana na uzoefu wake ni gharama kwani lazima umjali kuliko mke/mume wa ndoa. Hii ndio sababu ya msanii kusema. "Hasara ikanitia kuifua kwa sabuni". Mwisho msanii anaelezea kuwa: "tena yatia udhia iwambapo mlangoni". Mshororo huu una maana kwamba unapomiliki mtu wa aina hii anakunyima uhuru. Unashindwa kumtambulisha kwa familia na anaweza kuzidisha hali ngumu ya maisha. Huzidisha hali ngumu ya maisha kwa sababu mashirikiano kati yenu huonekana katika matumizi tu na sio kwenye uzalishaji. Hivyo baada ya msimbo wa kisimiotiki kufumbua fumbizi za kifasihi, mtafiti amebaini kuwa msanii alikusudia kuwaelekeza wote wale wenye jicho la nje kuwa kama hawatabadilika basi watashindwa kuendelea kiuchumi. Watatumia rasilimali zote kwa ajili ya kuhudumia mabibi/mabwana wa nje ya ndoa (pazia). Dai hili lilishadidiwa na methali isemayo kuwa "Mwenye mapenzi haoni ingawa macho anayo". Mwenye mapenzi anaweza

kutoa kila chake na kumkabidhi mpenzi wake. Haya yameshadidiwa na msanii Seif Salim katika wimbo wake wa *Nyonda wangu* ubeti wa nne (4) anaposema:-

Penzi nimekupa wewe liwe lako peke yako
Sitampa mwenginewe kuligawa tena mwiko
Ujitulize upowe kila changu mali yako

Maelezo ya ubeti huo wa wimbo wa msanii Seif Salim yanaunga mkono kuwa, kila mwenye kupenda haogopi hasara. Pia Seif Salum anatuonesha kwenye mshororo wa mwisho wa ubeti huo anaposema “ujitulize upowe kila changu mali yako” akithibitisha kuwa mtu anapopenda anaweza kutoa kila anachomiliki kumkabidhi mpenzi wake huyo wa nje.

Vile vile, dhamira ya maendeleo ya kiuchumi imeoneshwa na msanii katika wimbo wake wa *Mkunwa na mkunaji* anatumia tashtiti kuwazindua wadau wote kuendeleza kasi ya uwajibikaji ili kuleta maendeleo endelevu. Hili linaoneshwa na msanii katika kila mstari wa mwisho wa beti zote anaposema: *mkunwaji na mkuna muona raha ni nani?* Kwa maoni ya mtafiti yanayoongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji ubeti huu wa wimbo maana yake ni kwamba msanii anauliza kuwa kati ya raia na viongozi mwenye jukumu la kuleta maendeleo ni nani? Msanii katumia mbinu hii ili kuibua dhamira ya maendeleo ya kiuchumi na kuwaachia watu waendelee kutafiti na waibuke na jawabu kwa ajili ya maslahi yao na kizazi kijacho. Mtafiti wa utafiti huu anaona kuwa kila mtu awe kiongozi au raia ana jukumu la kufanya kazi na kuleta maendeleo. Viongozi na raia kwa nafasi zao na bila kuwasahau wanawake ambao wanatakiwa kuwa mstari wa mbele katika suala la kuleta maendeleo. Dai hili

linatiliwa mkazo na muimbaji/mtunzi chipukizi Vicki Mtetema (2014) alipoimba wimbo wake wa kuhamasisha maendeleo na uwajibikaji kwa wanawake aliposema:

> Wanawake na maendeleo
> Tufanye kazi tusonge mbele wee
> Walelewaleleee walelewalee wanawake
> Tufanye kazi tusonge mbele wee

Maelezo haya ya msanii Vicki yanawakumbusha na kuwaasa wanawake kuwa wabadilike na waondokane na mawazo kwamba mwanamke ni kwa ajili ya kupokea tu bali wawajibike kuleta maendeleo yao binafsi na taifa kwa jumla. Haya ni mawazo ya mtafiti yanayoongozwa ni nadharia ya mwitiko wa msomaji.

4.2.2.8 Dhamira ya Umoja na Mshikamano

Msanii Shakila alijitahidi sana kusisitiza umoja na mshikamano. Jambo hili lilijitokeza sana katika kazi yake ya utunzi na uimbaji wa nyimbo zake. Msanii huyu mzoefu alifanya kazi hii kwa kuangalia kwa ukaribu zaidi mahitaji ya jamii. Mtafiti anamuona Shakila kuwa ni mtu mwenye kwenda na wakati. Shakila katika nyimbo zake alijitahidi sana kutatua migogoro iliyoashiria utengano na malumbano yaliyokuwa yakimkabili yeye mwenyewe au jamii iliyomzunguka. Alihimiza umoja na mshikamano kwa kutambua kwamba bila ya kuwepo umoja na mshikamano kunaweza kupelekea mwisho mbaya utakaoathiri maisha ya familia, jamii na hata taifa kwa jumla. Kwa kuwepo utengano na mfarakano hakuna kitakachokuwa katika hali ya ufanisi. Hivyo kuna baadhi ya nyimbo zake kama vile *Akukataae hakwambii toka,* amelikemea hilo kwa kawaasa watu kuwa karibu, pamoja na kuondosha tofauti zao zinazoletwa na kasoro ndogondogo walizonazo. Shakila anaonesha haya katika ubeti wa nyimbo iliyotajwa hapo juu kwa kusema:-

Watu hutendana zaidi ya hayo
Watu hutendana zaidi ya hayo
Watu hutendana zaidi ya hayo
Watu hutendana zaidi ya hayo
Wakatukanana kupita mifano
Wakatukanana kupita mifano
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno

Katika beti hii ya wimbo mtafiti akiongozwa na nadharia ya mwitiko wa msomaji amegundua kuwa Bi Shakila amekusudia kuwaasa watu hasa wale wenye tabia ya kukata mawasiliano ya aina zote baada ya kukwaruzana hata kama ni kwa bahati mbaya watafute suluhu na kupatana. Shakila anawataka wanajamii waelewe kwamba kila mtu atakapokutwa na tatizo anatakiwa ahisi kwamba hilo ni jambo la kawaida na ni dogo tu. Watu wengine wameshafikwa na makubwa zaidi ya lililomfika yeye na wamekuwa na subira wakapatana na kuishi kama walivyokuwa zamani.

Aidha, dhamira ya umoja na mshikamano imegunduliwa na mtafiti katika wimbo wa msanii unaosema “Aloanza pekeke” ubeti wa kwanza wa wimbo huo msanii anaposema:-

Aloanza pekepeke kugombanisha wenzake
Sasa yuko peke yake kasimama kila pembe
Aloanza pekepeke kugombanisha wenzake
Sasa yuko peke yake kasimama kila pembe
Kamaliza hila zake hazifai hazifai hata chembe

Mtafiti akisuhubiana moja kwa moja na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amepata fursa ya kuiona dhamira ya umoja na mshikamano katika ubeti huu wa wimbo wa

msanii Shakila. Ubeti huu unaoonesha umuhimu wa watu kuishi pamoja kwa mshikamano uliojaa huba na mapenzi yanayomjali kila mmoja na nafasi yake. Katika ubeti huu wa wimbo, msanii ameonesha athari ya wale wanaovunja maelewano miongoni mwa watu. Watu hawa mara tu wanapogunduliwa na kitendo hicho kibaya hutengwa wao na kuanza kupata taabu kwani watu hawakubaliani na hili na wanajua fika kuwa *umoja ni nguvu utengano ni udhaifu*. Msanii akiendelea kusema kuwa "Sasa yuko peke yake kasimama kila pembe". Hapa Shakila anajaribu kuiasa jamii athari anazozipata mgombanishaji watu kuwa kila mmoja huwa na hadhari na mtu huyo na hujiweka mbali nae. Viumbe kama hawa wapo wengi kwani hawakuzungumzwa na Bi Shakila peke yake, bali hata gwiji wa taarab asilia Moh'd Elias katika wimbo wake wa *Muungwana* amewataja kwa kukuwaasa ndani ya beti za wimbo wake anaposema:-

3 - Usijipe uungwana unayo hiyo tabia
Ukweli hujaunena watu wakausikia
Vipembeni wanong'ona maovu kunizulia
Kwa mimi khabari sina bukheri nimetulia

4 - Muungwana sina shaka nimeswafi yangu nia
Yazidi yangu baraka mola aniongezea
Yangu yote yananyoka wewe waranda na njia
Wala sitoadhirika kama ulodhamiria

Maelezo ya msanii huyu kutoka katika beti hizo mbili pia yanagogoteza na kuunga mkono kuwa mgombanishaji ni mtu mwenye tabia isiyopendeza. Siku zote mwisho wa mgombanishaji sio mwema. Ubaya aliokusudia umfike mwenzake humrejea mwenyewe. Kwa muktadha huo ndio maana msanii Elias akamwambia mtu huyo kuwa, *yangu yote yananyoka wewe waranda na njia*. Elias alisema hayo ili kuikumbushia athari ya mtu anaegombanisha waliopatana na kuwaasa wanajamii

kuwa hii sio kazi njema kwani mwisho wake ni kuzuzuka, kupumbazika na kuchekwa na wanaoijua asili ya tatizo lako. Hayo ni maoni ya mtafiti yaliyoongozwa ni nadharia ya mwitiko wa msomaji.

Vilevile, dhamira ya umoja na mshikamano imegunduliwa na mtafiti alipokuwa akichambua data kwenye wimbo wa Bi Shakila unaosema *Mapenzi ni kama donda* ubeti wa kwanza wa wimbo huu anaposema:-

Nimechoka vumilia leo nawapasulia
Nimechoka vumilia leo nawapasulia
Imekuwa siku hizi kila siku nnalia
Imekuwa siku hizi kila siku nnalia
Nanyi hamuniulizi kipi nnacholilia
Nanyi hamuniulizi kipi nnacholilia

Kwa uoni wa mtafiti unaoungwa mkono na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, msanii katika wimbo huu pamoja na dhamira nyengine zilizomo, pia anazungumzia suala la umoja na mshikamano kwani anachukua nafasi kuwahimiza wanajamii kuwa pamoja kwa raha na shida. Watu wanatakiwa wasaidiane katika kila jambo litakalomfika mmoja miongoni mwao. Kwa hivyo msanii aliposema *nanyi hamuniulizi kipi nnacholilia* anakusudia kuwaasa watu kuwauliza na kuwanasihi wenzao kila wanapofikwa na hali au jambo lisilo la kufurahisha. Kuna msemo wa Kiswahili unaosema kwamba "*Akufaae kwa dhiki ndie wako rafiki*". Msemo huu unamaanisha kuwa watu wasipendane kwa raha tu bali hata katika masuala ya shida. Ijulikane kwamba akupendae hasa atakuwa msaada zaidi kwako katika wakati wa matatizo.

4.2.2.9 Dhamira ya Utii na Heshima

Utii na heshima ni moja miongoni mwa dhamira zilizotiliwa mkazo na Bi Shakila katika usanii wake, Bi Shakila kaitumia nafasi hii kuutangazia umma kuwa bila ya utii na heshima hakuna maendeleo katika maisha ya ndoa. Kwa kukosekana tunu mbili hizi adimu maendeleo hukosekana katika kazi na katika maisha ya kawaida ya wanajamii. Kwa mtazamo huo ni lazima iwepo heshima kwa raia na viongozi, mke na mume, majirani na hata jamii na wapiti njia. Mtafiti ameigundua dhamira hii katika wimbo wa msanii tajwa unaoitwa *Mpenzi unisamehe* ubeti wa kwanza wa wimbo huo ambao unasema unasema:-

> Kama kosa nimeridhi sirudii asilani
> Mpenzi naomba radhi tuishi kama zamani
> Mpenzi naomba radhi tuishi kama zamani
> Adhabuyo nakubali uniadhibu mwandani

Mtafiti akiongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika msingi wake unaosimamia msomaji kutoa maoni yake kutokana na ufahamu wake, mtafiti anashawishika kusema kuwa katika ubeti huu wa wimbo alikusudia kuwaonesha na kuwafunza watu utii na heshima kumbwa aliyokuwa nayo kwa nyonda wake. Pamoja na kwamba amemtendea kosa lakini bado tunapata picha kuwa heshima anayo na ni mtiifu sana kwa mpenzi wake. Anakiri kwamba kilichotokea ilikuwa ni mapungufu ya kibinadamu tu. Hili linadhihirishwa na viashiria vingi vya utii vilivyomo katika ubeti huo wa wimbo. Viashiria hivyo ni kama vile kukiri kosa, kudiriki kuomba radhi na kuwa tayari kupewa aina yoyote ya adhabu kutoka kwa mwandani wake. Kilicho muhimu kwake ni kuomba fursa ya kutaka arejee katika penzi adhimu la wake mpumbazi.

Msanii katika wimbo huu alidhamiria kuwaonya wale ambao wanapenda kukumbatia ukale unaotokana na silka ya kibinadamu ya kutokubali kosa. Silka mbaya ya kukataa kukubali kosa ambalo amelifanya hata ikiwa watu wamemshuhudia. Msanii anawasisitiza watu na kuwataka wabadilike kwani kubakia kwao katika msimamo huo kunachochea na kuzidisha hasira kwa yule aliyemkosea na kukerwa. Aliyerwa anaweza kubaki na usugu kiasi kwamba anaweza kukataa hata kutoa msamaha kwa yule aliyemkera. Mtu anaweza kupoteza na kukosa mengi ya thamani katika uhai wake. Anaweza kumpoteza mpenzi na penzi lake atakapoMkataa kwa kukosa kumuheshimu na kujiheshimu mwenyewe. Dai hili linatiliwa mkazo na Al – watani Makame Faki katika wimbo wake "*Kweli alikuwa wangu"*. Kiitikio cha wimbo huu kinashadidia hayo kwa kusema kuwa:-

Kiasi nimkatae
Kavunja yake heshima
Nazinge amtakae
Kwangu mimi basi tena

Hayo ndio malipo ya kukosa utii na heshima katika penzi. Msanii anaamua kumsamehe mpenzi ambaye alishindwa kujituliza na kubakia katika himaya yake. Hata hivyo alilazimisha kutoa jicho lake nje ya nyumba yake na kuangaza kwa mtu mwengine kisha akajifanya fedhuli na mwenye kakosa heshima. Hata hivyo baada ya kugundua kosa lake bado anashindwa kuomba radhi. Msanii anaamua kumkataa na kuachana nae. Haya ni mawazo ya mtafiti yanayoongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika msingi wake unaohalalisha mawazo ya msomaji wa kazi ya fasihi na kuifasiri kulingana na ufahamu na uzoefu alionao. Jambo lililo wazi ni kuwa binadamu yoyote yule anapata taabu sana kuishi na mtu aliyekosa utii na heshima na ikibidi huachana nae wakaishi mbalimbali.

Sambamba na hayo, dhamira ya utii na heshima imetumika na kugunduliwa na mtafiti katika wimbo wa Bi Shakila, *Nimezama kwa mapenzi* katika ubeti wa tano (5) wa wimbo huu, unasema:-

> Nimezama nimezama katika kina kirefu
> Kila nikijitazama moyoni napata hofu
> Nimezama nimezama katika kina kirefu
> Kila nikijitazama moyoni napata hofu
> Ilahi Mola karima ndie mwenye kuniafu

Katika ubeti huu mtafiti amegundua utii na heshima uliozungumzwa na msanii Shakila katika hali mbili. Kwanza utii wa Bi Shakila kwa mpenzi wake. Na pili utii na heshima wa msanii kwa muumba wake. Utii wa msanii kwa mpenzi wake unagundulikana pale anaposema kuwa amezama katika kina kirefu lakini kila akijitazama moyoni anapata hofu. Hii inamaana kwamba utii na heshima yake katika mapenzi ndio inayomzamisha katika penzi zito na kushindwa kutoka. Kila alipofikiria kutoka alipata taabu kwa sababu alijua fika kwamba atasababisha matatizo na upweke kwa mpenzi wake pamoja na fedhuli ya bwana huyo aliyokuwa nayo.

Utii na heshima wa aina ya pili ni wa msanii na Muumba wake. Hili linagogotezwa na msanii katika mshororo wa mwisho wa wimbo unaosema: *Ilahi Mola karima kaniepushia adhaba*.

Mshororo huu unaonesha utii na heshima ya msanii Shakila kwa Mwenyezi Mungu (SW). Pamoja na yote yanayojitokeza bado anaheshimu mamlaka na uwezo mkubwa

wa Allah (SW) wa kuweza kuwaokoa viumbe wake katika hali nzito ya majanga mbalimbali. Kuwaokoa na majanga na maafa yanawakabili yakiwemo matatizo ya kimapenzi. Haya ni mawazo ya mtafiti yanayotokana na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

4.3 Mbinu za Kisanaa zinazojitokeza katika Nyimbo za Shakila Saidi Khamisi

Neno sanaa kwa mujibu wa TUKI (1990) ni ufundi wa kuwasilisha hisia na mawazo ya binaadamu kwa maandishi, michoro, maigizo, nyimbo au uchongaji. Kwa kawaida msanii anapomudu fani kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanii huipendezesha kazi yake na kujijengea upekee hasa katika uwanja wa fasihi.

Fani ni ufundi wa kisanaa unaotumiwa na mtunzi wa kazi ya kifasihi katika kuisana kazi yake (Omary, 2011). Ufundi huo wa kisanaa unapatikana katika vipengele vya matumizi ya lugha, wahusika, mtindo, muundo na mandhari katika kazi ya fasihi (Msokile, 1992: Senkoro, 2011). Ni kutokana na ufundi huo ndio wasomaji husema wanavutiwa au kutovutiwa na kazi fulani wakati wanaposoma au kusikiliza kazi husika ya fasihi. Kazi za fasihi zinaweza kuwasilishwa kwa njia ya riwaya, ushairi, hadithi fupi, tamthiliya, vichekesho na maigizo. Ni ufundi/ustadi wa kisanaa anaoutumia msanii katika kufikisha ujumbe alioukusudia kwa jamii. Msanii hutumia ufundi huu katika kubebesha maudhui kazi yake ya fasihi.

Katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti kuhusu mbinu za kisanaa, mtafiti amezingatia lengo mahsusi la pili la utafiti huu lisemalo: Kubaini Mbinu za kisanaa zilizojitokeza katika Nyimbo Teule za Shakila Saidi. Lengo hili linakwenda

sambamba na swali la msingi la pili la utafiti huu linalosema: Ni mbinu gani za kisanaa zinazojitokeza katika nyimbo teule za Shakila Saidi? Mtafiti ili kufanikisha lengo mahususi la pili na kujibu swali la pili, aliongozwa na nadharia ya Simiotiki na Mwitiko wa Msomaji na alibaini mbinu mbalimbali za kisanaa zinazojitokeza katika nyimbo za Shakila Saidi kama ifuatavyo:

4.3.1 Matumizi ya Kejeli

Mulokozi na Kahigi (1979) wanaeleza kuwa kejeli ni usemi ambao maana yake ya ndani ni kinyume chake na inabeuwa maana yake halisi. Vilevile tunaweza kusema kwa kejeli ni usemi wa kebehi ambao kisemwacho sicho kikusudiwacho na msemaji. Mtafiti aligundua kuwa katika nyimbo za muimbaji Shakila Saidi imetumika mbinu ya kejeli ambapo baadhi ya nyimbo hizo zina mafumbo ambayo maana yake hasa ni tofauti na mwonekano wake. Kwa mfano katika nyimbo yake inayosema, *Hujui alacho kuku usingempa mgeni.* Mtafiti aliona kwamba wimbo huu umetumia mbinu ya kejeli, msanii ametumia mbinu hii kuwaasa wale wenye tabia mbaya ya kumiliki mabwana/mabibi wa nje ya ndoa kisha wakawasifu kupita kiasi na hali hawajui tabia zao. Wameshindwa kukumbuka kuwa kama alivyokwenda kwake huenda anakwenda na kwa mwengine. Kwa mantiki hii mtunzi anawataka wanajamii kuwa na hadhari sana juu ya jambo hili. Ieleweke kwamba mtu anayekubali kuunga uhusiano wa kimapenzi pasina uhalali wa kufanya hivyo ni rahisi kulikubali hilo hata kwa watu wengine. hivyo msanii anawaasa wanajamii kuachana na suala hilo au kufanya uchunguzi kabla ili kuepusha athari za kijamii na kiafya. Kufanya matendo ya mapenzi na watu wan je ya ndoa wasiojulikana tabia zao ni rahisi mno kupata maradhi ya uaasharati. Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika

msingi wake unaomruhusu mhakiki kutafsiri matini kwa mujibu wa ufahamu na uzoefu wake na bila kupoteza maana kutoka katika matini chanzi, mbinu ya kejeli inaonekana wazi katika nyimbo hii, kwani bibi/bwana wa nje ya ndoa amekejeliwa na kuitwa kuku. Hivyo kwa kuongozwa na nadharia hiyo mtafiti aliitafsiri kejeli hiyo kuwa, hujui hali halisi ilivyo juu ya tabia ya mpenzi wako huyo ya kuwa na wapenzi wengine zaidi yako kwani kama unajua usingemsifu kwa wengine ilihali wao wanamjua kuwa sio wako peke yako.

Aidha mbinu hii ya kejeli imetumiwa na msanii Shakila katika wimbo wake wa *Pazia* katika mstari wa mwanzo wa kiitikio anaposema:

Haina kinga pazia hata iwe ya thamani
Heri nunua kofia hifadhi ya utosini
Ikusitiri kwa jua lisikuchome kichwani

Katika maelezo haya mtafiti amegundua kejeli, kwani maana hasa aliyokusudia msanii Shakila anaposema haina kinga pazia hata iwe ya thamani ni kinyume kabisa na maana halisi ya maneno hayo. Kejeli hii imetumiwa na msanii Shakila kuwaonya wale wote wenye tabia mbaya ya kumiliki mabibi au mabwana wa nje ya ndoa. Shakila alikuwa anachukua fursa hii kuwaambia wanajamii kwamba katika kuliendeleza hilo hakuna faida watakayoipata hata mabibi na mabwana hao wawe na uzuri na utajiri wa kiasi gani. kubwa linaloweza kupatikana ni kuwaingiza katika matatizo na kuwaharibia mustakbali wa maisha yao ya kujipatia jina jipya la uasharati. Sambamba na hilo tabia ya uasharati hata katika vitabu vya dini inakatazwa. Kwa mafunzo ya dini zote malipo ya uasharati ni moto iwapo muhusika hajatubia ipasavyo. Quran (4:14) inaeleza kuhusu kuacha machafu yote ikiwemo zinaa (uasharati). Allah (SW) anasema: “Na anayemuasi Mwenyezi Mungu (SW) na

Mtume wake, na kuiruka mipaka yake (Mwenyezi Mungu SW) atamwingiza motoni. Humo watakaa milele na atapata adhabu ifedheheshayo.” Aya hii inaendelea kutanabahisha watu kujilinda na mambo machafu kwa sababu mwisho wa watu hao ni mbaya duniani na akhera mbele ya Allah (SW).

Haya ni mawazo ya mtafiti yaliyorejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa mhakiki wa matini kutoa mawazo yake mwenyewe. Maelezo haya pia yanaungwa mkono na semi maarufu inayoandikwa katika mikoba kisiwani Pemba inayosema: “Nienzi mimi wa ndani wa nje hana thamani”. Semi hii ina maana kwamba bibi au bwana wa nje ya ndoa thamani yake ni ndogo mno. Hana thamani hasa kulinganishwa na gharama na matatizo anayoweza kusababisha kwa mmiliki wake ni sawa na kusema kuwa hana thamani kabisa.

4.3.2 Matumizi ya Tashtiti

Tashtiti ni moja miongoni mwa mbinu za kisanaa ambapo msanii hutumia mfumo wa kuuliza maswali anayotambua jawabu zake katika kazi ya fasihi.

Baada ya kuzichambua nyimbo za muimbaji Shakila, mtafiti aligundua kwamba katika baadhi ya nyimbo hizo msanii ametumia mbinu ya tashtiti kwani anauliza maswali ambayo anaelewa jawabu zake. Kwa mfano katika wimbo wake wa *Aloanza peke peke* Ubeti (3) wa tatu msanii anaposema:

Ndugu yangu jitulize bure unahangaika
Yakweli nikueleze viumbe wanakucheka
Ndugu yangu jitulize bure unahangaika
Yakweli nikueleze viumbe wanakucheka
Wewe utaondoaje Wewe utaondoaje
Wewe utaondoaje Mungu alichokiweka?

Kutokana na maoni ya mtafiti yaliyoongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa mhakiki kufasiri matini ya kifasihi kulingana na uzoefu alionao amegundua kwamba katika ubeti huu wa wimbo, msanii ametumia mbinu ya tashtiti kwani kauliza, “Wewe utaondoaje Mungu alichokiweka?”Ameuliza hivyo ilhali akielewa kwamba alichokiamulia Mungu kindelee kuishi katika nafasi aliyokiweka hakuna yoyote ambaye ataweza kukiondoa. Ila msanii amekusudia kutoa ujumbe tu kwa wale wanaopenda kujivisha joho la Allah (SW) na kujidanganya kwamba wananguvu za kupangua na kuondoa alichokiweka yeye. Msanii anawataka watu wa aina hiyo kuwa wasijipe tabu hayo hayako katika uwezo wao. Maelezo haya pia yanashadidiwa na aya ya Qur-ani tukufu inayosema:

> "Haufiki msiba wowote ispokuwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (S.W) na anaemuamini Mwenyezi Mungu huongoza moyo wake (kwenda maliwaza mazuri) na Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu" (64:11).

Maelezo haya kutoka katika aya ya Qur-ani yana maana kwamba chochote kinachomfika mtu kikiwa cha kufurahisha au cha kuhuzunisha huwa ni mipango ya Mwenyezi Mungu na wala si uwezo wa mtu au kiumbe chochote.

Vile vilemtafiti amegundua kuwa mbinu hii ya tashtiti imetumiwa na msanii Al-anisa Shakila katika wimbo wake unaoitwa: *Nimezama kwa mapenzi* Ubeti wa pili (2) wa wimbo huu, mstari wa kwanza (1) msanii ameanza kwa kutuonesha tashtiti anapouliza:

Wenzangu nawauliza nini dawa ya mapenzi?
Waganga nimemaliza wa makombe na hirizi
Wenzangu nawau liza nini dawa ya mapenzi?
Waganga nimemaliza wa makombe na hirizi
Ilahi mola muweza ataniafu mwenyezi

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayopelekea kazi moja ya fasihi kupewa maana tofauti kulingana na ufahamu wa wasomaji wa matini hiyo. Hapa nadharia hii inatoa fursa kwa mtafiti wa utafiti huu kusema kwamba msanii katika ubeti huu wa wimbo ametumia tashtiti ya kuuliza kwa wenzake nini dawa ya mapenzi huku akitambua kwa upana kabisa kuwa dawa ya mapenzi ni kupendana kwa dhati. Msanii alitumia mbinu hii kuwatanabahisha watu kuwa katika kupendana watambue uzito wa penzi kwa wenza wao. Hii ni kwa sababu mapenzi yanapozidi kwa mmoja kumpenda mwenzake bila mwenza huyu kutojali na kuthamini penzi zito alilonalo mpenzi wake kwake anaweza kumsababishia maradhi ya mapenzi. Maradhi ya mapenzi ni maradhi ambayo hayasikii dawa za waganga wa makombe wala hirinzi. Dawa ya maradhi haya ni mpenzi wake amrejeshee penzi kama anavyompenda yeye. Na hii inathibitisha kwamba hakuna dawa yoyote inayotibu maradhi ya mapenzi au kumtuliza na kumfanya mtu asiyetaka kupenda apende kwa lazima. Na endapo vitatumika vitu hivyo kwa ajili ya kutulizia pendo, baada ya muda penzi hilo humaliza nguvu na migogoro huanza upya. Migogoro huzuka upya kwa kuwa inakuwa hapakutumika ridhaa bali kumetumika nguvu na hadaa na penzi ni hiari na kushibana moyoni. Ushahidi unaoonesha hayo umeelezwa na kuungwa mkono na Sengo (2009) katika diwani yake ya *Tungizi za Mnyagatwa* katika shairi lake la *Kila rika na uzuri* ubeti wa pili (2) wa shairi hilo msanii anaposema:

> Ukafutikwa moyoni, kwa huba si kwa hadaa
> Ukatiwa na damuni, na yako ikamvaa
> Mkahemukwa milini, kama vile ni sanaa
> Kila rika na uzuri, safari kakuteuwa

Kwa mujibu wa nadharia ya Mwitiko wa Msomaji, fursa inapatikana ya kuifasiri beti hii ya ushairi kuwa ni jawabu ya suala la msanii Shakila anapouliza kuwa *nini dawa*

ya mapenzi? Na anajibiwa kwa kuambiwa kuwa dawa ya mapenzi ni kupendana kwani mapenzi ni jambo la hiari sio la hadaa wala kulazimishana.

4.3.3 Matumizi ya Methali

Senkoro (1984) anaeleza kuwa methali ni semi au sehemu ya lugha ambayo hufananishwa na kiungo cha lugha au kitoweo cha lugha. Pia methali hutumiwa kwa kutafakari na kupima maisha, kufunzia jumuia na kutawalia jamii na mazingira ya binaadamu. Ameendelea kusema kuwa methali hufunua dhamira ya jamii na hekima ya wale wanaoitumia katika mazungumzo yao. Hivyo uwepo wa methali ni utajirisho wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi.

Mtafiti wa kazi hii, amegundua kwamba, nyimbo za msanii Shakila zimetumia mbinu za kisanaa tofauti zikiwemo methali. Mfano wa methali hizo ni ile iliopo katika wimbo wake usemao *Akukatae hakwambii toka* Maelezo ya utungo huu yanatoka moja kwa moja katika methali isemayo, akufukuzae hakwambii toka kama alivyoitumia katika ubeti wa kwanza wa nyimbo hiyo unaosema:-

Akukatae	hakwambii toka
Akukatae	hakwambii toka
Akukatae	hakwambii toka
Akukatae	hakwambii toka
Huona mamboye	yamebadilika
Huona mamboye	yamebadilika
Waweza ukae	huwezi ondoka
Waweza ukae	huwezi ondoka
Waweza ukae	huwezi ondoka
Waweza ukae	huwezi ondoka

Katika beti hii, mtafiti alirejelea nadharia ya Simiotiki kufumbua fumbo lililopo katika methali iliyotumiwa na msanii Shakila na kugundua kuwa msanii ametumia methali hii kuwaelimisha watu wanaopenda. Anawapa elimu kuhusu dalili za

kukataliwa kwani sio lazima mtu awambiwe ondoka, anaweza tu kugundua kutokana na matendo ya kila siku ya mpenzi wake anayomtendea kinyume na mazowea aliyokuwa nayo wakati alipokuwa na mapenzi ya dhati kwake.

Dai hili lilitiliwa nguvu na msanii huyu katika wimbo wake huu wa "*Akukatae hakwambii toka"* katika ubeti wake wa pili (2) wa wimbo huo unasema:-

Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Usinidhihaki la kweli nambie
Usinidhihaki la kweli nambie
Kama hunitaki heri nitulie
Kama hunitaki heri nitulie
Kama hunitaki heri nitulie
Kama hunitaki heri nitulie

Maelezo haya ya ubeti yanashadidia maana ya methali hii. Msanii alishagundua tabia za mwenza wake na namna zilivyobadilika na ndio maana anachukua nafasi hii kumwambia usinidhihaki la kweli nambie. Amemwambia hivyo baada ya kugundua tabia mbaya iliyoashiria kuvunjika kwa pendo lao, msanii akaona na kumwambia, "*kama hunitaki heri nitulie",* yaani aanze kuachana na kuwa mbali nae.

Sambamba na hilo, msanii kupitia methali hii anawaeleza watu kuwa wanapochokana na wenza wao wasiwape tabu na kuwadhalilisha katika minyororo. Ni vyema wawape uhuru wa kwenda kwengine kwani pamoja na kuona mabadiliko ya tabia kama wapo katika mkataba mfano wa ndoa bado wapo ndani ya minyororo. Haya ni mawazo ya mtafiti yanayoungwa mkono na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

4.3.4 Matumizi ya Majazi

Majazi ni mbinu ya kumpa mtu jina linaloakisi au linaloelekeza kwenye wasifu wa tabia zake. Wamitila (2010) anaeleza kuwa majazi ni majina ambayo yana maana fulani, majina haya yanaweza kuhusiana na tabia, maisha, matabaka, mitazamo na elimu ya wahusika.

Mtafiti amegundua mbinu hii ya majazi imetumiwa na msanii Shakila katika baadhi ya nyimbo zake. Mfano, katika wimbo unaoitwa "*Oh rabi sinipe mapenzi*" msanii ametumia majazi katika ubeti wa nne unaosema:-

Simsahau milele kila ninapomuona
Nakumbuka vile vile yalopita mwaka jana
Mimi na kiumbe yule ooh
Mimi na kiumbe yule naapa sirudi tena

Katika ubeti huu msanii ametumia neno "*kiumbe*", kama majazi. Kawaida kiumbe ni miongoni mwa viumbwa vya Allah vyote ambavyo huvipa uhai na kuishi. Vinaweza kuwa ni mtu, ndege, mnyama au miti. Lakini hapa maana ya neno kiumbe limetumika kama jitu ovu na lenye tabia mbaya zinazomchosha mpenzi wake. Shakila anamwita kiumbe kutokana na kuchoka kwake kumstahamilia na anakula kiapo kuwa yeye na kiumbe huyo basi na wala hatorudi tena kuishi nae.

Haya ni mawazo ya mtafiti yanayoongozwa na nadharia ya simiotiki katika msimbo wake wa kihemenitiki ambao hufumbua majina yaliyofumbata maana na ujumbe nzito ulio ndani yake. Msanii Shakila hakuweza kusema kuwa yeye na jitu lile, jeuri,

fedhuli, katili, jinga hawezi kuishi nalo tena. Badala yake ametumia majazi "*kiumbe"* kusitiri maana zilizomo ndani ya fumbo hilo.

4.3.5 Matumizi ya Takriri

Jilala (2016:177) anasema kuwa takriri ni mtindo wa usemi ambao msemaji hurudia neno au maneno yale yale kwa lengo la kutia mkazo au kusisitiza jambo. Mtafiti anaona kwamba takriri ni mbinu ya kisanaa ya kurudia neno/maneno/msitari/ubeti kwa lengo la kutilia mkazo na msisitizo wazo linalowasilishwa kwa walengwa.

Mtafiti katika kukusanya na kuchambua data amegundua kwamba msanii Shakila ameitumia mbinu hii ya kurudiarudia mistari na maneno katika baadhi ya nyimbo zake. Mfano wa nyimbo ambazo msanii ametumia mbinu ya kurudia neno ni pamoja na wimbo usemao "*Nimezama kwa mapenzi*". Katika wimbo huu amelirudia neno "nimezama″ kama linavyoonekana katika ubeti wa 3 hadi wa 6 wa wimbo huo anaposema:

> Nimezama nimezama sijui kama tatoka
> Kujikwamua siwezi taabani nateseka
> Nimezama kwa mapenzi sijui kama tatoka
> Kujikwamua siwezi taabani nateseka
> Ilahi Mola Mwenyezi ataniafu Rabuka

Msanii wa wimbo huu amerudiarudia neno "nimezama" ili kuonesha uzito wa penzi alilonalo. Kuzama maana yake ni hali ya kitu kufunikwa kiasi kwamba hakiwezi kuonekana. Shakila na yeye amekusudia kuiambia jamii kuwa amenogewa na penzi kiasi ambacho limemfunika haonekani wala haoni chengine chochote kilichopo ulimwenguni hata kikiwa na thamani na uzuri wa kiasi gani. Analoliona ni penzi tu ambalo limemzamisha, amelikumbatia na kuling'ang'ania lisimtoke.

Aidha msanii Shakila ametumia mbinu ya kurudiarudia mistari ya beti za nyimbo zake. Mfano wa mbinu hii tunauona katika wimbo wake unaosema *"Kuku na yai"*, ubeti wa kwanza anaposema:-

Nawauliza nisai marijali mukiweza
Nawauliza nisai marijali mukiweza
Hivi sasa niko hoi moja linanitatiza
Hivi sasa niko hoi moja linanitatiza
Kati ya kuku na yai ni kipi kilichoanza
Kati ya kuku na yai ni kipi kilichoanza

Katika ubeti huu msanii amerudia kila mstari mara mbili ili kusisitiza lengo alilokusudia. Mfano katika mstari wa mwisho unaosema, *kati ya kuku na yai ni kipi kilichoanza.* Mtafiti akiungwa mkono na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayomruhusu mhakiki kuihakiki kazi ya fasihi kulingana na ufahamu na uzoefu alionao, amegundua kwamba takriri iliyotumika imekusudia kuwasisitiza wale walioulizwa kutoa jawabu kwa haraka zaidi. Msanii anahisi asingerudia walioulizwa wangalidharau na kutokulipa uzito unaostahili suala ambalo wameulizwa na msanii.

Vile vile mtafiti amegundua utumiaji wa takriri ya mstari katika hali ya upokeano baina ya mwimbaji Shakila na waitikiaji wa wimbo wake. Mtafiti amegundua hili katika wimbo wa "Sasambu" kama ifuatavyo:-

Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore aaeee
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore aaeee
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro aaeee
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako

Nakupa nsomoro aaeee
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako

Al-anisa Shakila amerudia mistari hiyo ya ubeti zaidi ya mara moja huku akisaidiwa na waitikiaji wake kwa lengo la kusisitiza na kugogoteza mafunzo anayoyatoa kwa mwari wake. Amefanya hivyo ili mapenzi hayo yawe yenye kufana na yenye kuzalisha pendo litakalostawi na kukuza maisha bora ya ndoa yake. Kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayompa fursa mhakiki kuipa maana kazi ya msanii fulani, mhakiki amegundua kwamba katika mstari unaosema, "*nataka nsomore nsomore ndembo yangu*" bi - Shakila alikusudia kusema kwa kusisitiza kumwambia mwari wake kuwa natoa elimu kukufunza mwari wangu juu ya kumuenzi mume na kumsabilia kila kitu alichowajibikiwa kupewa kwa ajili ya kuimarisha penzi. Neno nsomore maana yake ni kutoa au kuchomoa kwa ajili ya kumridhisha mtu. Haya yameelezwa na Sengo katika muhadhara na wanafunzi wake wa M.A. Kiswahili mwaka 2016 katika Skuli ya Madungu Sekondari, Pemba.

Pia mtafiti amegundua kuwa, msanii Shakila kupitia wimbo wake wa *Mapenzi yamepungua* amerudia beti ya kwanza ya wimbo huu kila baada ya ubeti mmoja na kuufanya ubeti huo kuwa ni kiitikio cha wimbo wote. Beti hii iliyorudiwa inasomeka kama ifuatavyo:-

Mapenzi yamepungua mimi nimeshayaona
Kila nikiyachungua hakushwi kuoneana
Kheri nipate pumua kwako sina haja tena

Kiitikio
Mapenzi yamepungua mimi nimeshayaona
Kila nikiyachungua hakushwi kuoneana
Hakushwi kuoneana mapenzi yamepungua

Kutokana na maono ya mtafiti yanayoongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Mmaji, msanii ametumia mbinu ya kurudia ubeti wa kwanza na kuufanya kuwa kiitikio kinachokaririwa kila baada ya ubeti mmoja wa wimbo huo ili kuieleza hadhira kwamba mapenzi ya mwenza wake yamepungua kwa kiwango kikubwa sana. na si jambo la kusemwa mara moja likapita kwa sababu athari ya kupungukiwa na mapenzi hayo ni kubwa sana na hawezi kuvumilia wala kuificha hivyo iko wazi. Lazima jambo hilo lizungumzwe kila mara kutokana na ukubwa wake na ikiwezekana asaidiwe ili pendo lake lirejee kama ilivyokuwa zamani.

Maelezo hayo ya kupungukiwa na mapenzi yanaweza kumkuta mtu yoyote kwani yamewahi kumkuta hata al-watani Makame Faki jambo ambalo lilimfanya aweze kuimba wimbo wa *Sina raha* akiwa na kikundi cha Culture Musical Club. Tatizo hili la kupungukiwa na mapenzi ya mpenzi wake analionesha katika ubeti wa tatu (3) wa wimbo huo unaosema:-

Ajue naangamia asiifanye khiyana
Niliyotenda ridhia madhali tutapendana
Kumkosa naumia na maradhi sitapona

Ubeti huu unatuonesha athari alizozipata msanii kwa kukataliwa na mwenza wake na kushindwa kuvumilia hadi alipochukua hatua alizohisi zitamsaidia kulirejesha penzi lake. Anasema msanii katika kiitikio cha wimbo wake tulioutaja hapo juu kuwa:-

Wajumbe nimewatuma salamu wakuletee
Kwako waje hima hima na wewe uwapokee
Wallah si uzima ila wewe urejee

Hivyo mtafiti anakubaliana na wasanii hawa kuwa, kukosa mapenzi ya umpendae ni hatari inayoweza hata kusababisha kifo. Hivyo mbinu hii ya takriri imetumika katika nyimbo za msanii Shakila kwa lengo la kushadidia na kutowa msisitizo wa anachokieleza kama wanavyoitumia wasanii wengine wa kazi za fasihi.

4.3.6 Matumizi ya Taswira/Ishara

Jilala (2016) anafafanua kuwa taswira/ishara ni dhana inayotumika kuelezea kitu fulani ambacho huwakilisha kitu kingine. Ishara ni upeo wa sitiari. Katika ishara kitu kinachofahamika au kuaminika katika jamii inayohusika hutumika kama alama ya kitu kingine au hueleweka hivyo kwa wanajamii wengi. Kwa mfano msalaba ni ishara ya ukiristo na mwezi ni ishara ya uislam (Mulokozi 1996).

Mtafiti wa utafiti huu ameona kuwa ishara ni uwakilishi wa kitu kwa kutumia kitu chengine ambacho hakina uhusiano wa kimaana wala kiumbo. Uhusiano wao unaweza kuja kutokana na sifa fulani ya kitu hicho. Kwa mfano kuna baadhi ya watunzi huweka neno *ua* na huwakilisha mwanamke kutokana na sifa nzuri ya rangi na harufu ya kuvutia katika macho na moyo wa mtazamaji. Ua hunasibishwa na mwanamke kwa sababu mwanamke anazo sifa za uzuri na humpagawisha mwanamme hata kudiriki kumuita *ua* kutokana na mapambo na harufu yake nzuri.

Mtafiti akiungwa mkono na nadharia ya Simiotiki yenye msingi wa kisemantiki ambao humsaidia mhakiki kufumbua mafumbo ambayo kisemantiki yana maana lakini kimsingi msanii hakusudii analolisema. Tunaona kwamba Bi Shakila ameitumia mbinu hii ya kisanaa katika kazi yake. Kwa mfano ametumia neno

“kofia” na "pazia", kiishara katika kiitikio cha wimbo unaoitwa *Pazia.* Ubeti huo unaimbika kama ifuatavyo:-

Haina kinga pazia hata iwe na thamani
Heri nunua kofia hifadhi ya utosini
Ikusitiri kwa jua
Ikusitiri kwa jua lisikuchome kichwani
Ikusitiri kwa jua
Ikusitiri kwa jua lisikuchome kichwani

Kisemantiki kofia ni vazi la kiume linalovaliwa juu ya kichwa na pazia ni kitambaa kikubwa kinachofungwa pahala kama vile mlangoni au dirishani ili kuzuia kuona upande wa pili wa ndani au wa nje kutegemea zaidi mazingira yenyewe yalivyo.

Mtafiti akiongozwa na nadharia ya simiotiki katika msimbo huo alioutaja hapo juu anaona kwamba neno pazia limetumiwa na msanii Shakila kuashiria Bwana/Bibi wa nje ya ndoa. Bibi/Bwana wa njee hana stara yoyote kwa mmiliki wake na husaidia katika raha tu. Katika shida hawezi kusaidia kitu na ndio msanii akasema “*Haina kinga pazia hata iwe na thamani*”. Hili amelisema kwa sababu pazia makazi yake ni sehemu maalumu yaani ndani tu. Mmilki wake hawezi kwenda nayo kwenye safari, iwe harusini au msibani na wala hawezi kwenda nayo hadharani watu wengine wakakuona nayo. Hivyo hivyo ndivyo kwa Bwana na Bibi wa nje, mmiliki hawezi kumgotoa/kumtambulisha kwa familia akashiriki katika masuala ya kifamilia. Kinyume na neno na kofia ambalo limetumiwa na msanii kuashiria Mke/Mume, yaani Bwana/Bibi wa ndani ya ndoa ambae kwa nafasi yake anaweza kukusitiri kwa shida na raha. Unajifaharisha nae au unakwenda na kurudi nar ukiwa peke yako au ukiwa na familia. kofia ni vazi ambalo unaweza kutoka ukaenda nalo popote bila watu kukushangaa na kukuona mwendawazimu.

Aidha, katika wimbo wa *Nimezama kwa mapenzi* Mtafiti amegundua neno bahari lilotumiwa na msanii kiishara. Katika maana ya kisemantiki bahari katika mazingira au muktadha huu ni eneo kubwa lenye maji ya chumvi yenye kina kirefu ambacho hakuna mtu yoyote anaeweza kusimama au kutambaa katika maji hayo bila kuwa na vifaa maalumu.

Kwa kurejea nadharia ya Simiotiki, mtafiti anaona kwamba neno bahari limetumika kama ishara inayoashiria kiwango kikubwa cha penzi ambalo lilimkumba msanii wa wimbo huu Shakila binti Said kiasi kwamba lilimzingira na kumjalia hata ikawa hawezi kujizuia na ndipo alipoyasema haya:

Nimezama nimezama kwenye bahari ya huba
Moyo wangu walalama nalia hitia toba
Nimezama nimezama kwenye bahari ya huba
Moyo wangu walalama nalia hitia toba
Ilahi mola karima kanepushia adhaba

Hivyo msanii katika ubeti huu wa wimbo ametumia neno *bahari* kumaanisha huba zinazotokana na penzi la dhati na zito alilokuwa nalo kiasi moyo wake kulalama, kulia na kutia toba. Ameonesha hali hiyo kuonesha kwamba penzi hilo zito linaning'inia hewani kwa sababu ya kukosa mtu wa kulidhibiti, kulikinga, kulisegeka na kuliengaenga ili lisiendelee kumuathiri msanii, Shakila. Hali hii msanii aliifananisha na bahari kutokana na uzito na ukubwa wake. Haya ni mawazo ya mtafiti yaliyoungwa mkono na nadharia ya Simiotiki inayosaidia kufumbua mafumbo ya kiishara.

4.3.7 Matumizi ya Sala

Mulokozi (1996:51) anaeleza kwamba sala ni maombi ya msaada wa kiungu katika utatuzi wa matatizo ya kimaisha. Maomi kama haya huletwa pale muombaji anapokuwa kashindwa kuyafumbua kwa uwezo wake mwenyewe. Mara nyingi maombi haya hutumia lugha ya kisanaa na wakati mwengine hutumia hata nyimbo na mashairi. Sala huweza kuwekwa katika mikondo ya dua, maapizo na tabano. Mtafiti katika kazi ya msanii Shakila amegundua mbinu ya sala aina ya dua na maapizo kama ifuatavyo:

4.3.7.1 Dua

Dua ni maombi ya mja kwa mola wake ili apate mahitaji yake. Aidha dua ni maombi ya kawaida kwa mizimu, miungu na Mwenyezi Mungu (Mulokozi, 1996). Mbinu hii ya sala imetumiwa na msanii katika baadhi ya nyimbo zake. Mtafiti amegundua kuwa msanii amejiombea dua kwa Allah (SW) katika nyimbo zake. Mfano wa nyimbo iliyotumia mbinu hii ni pamoja na wimbo wa *Nimezama kwa mapenzi* ambapo dua imetumika katika kila mstari wa mwisho kwa beti zote za wimbo huo. Mfano katika ubeti wa pili wa wimbo huo, msanii anaposema:-

Wenzangu nawauliza	nini dawa ya mapenzi
Waganga nimemaliza	wa makombe na hirinzi
Wenzangu nawauliza	nini dawa ya mapenzi
Waganga nimemaliza	wa makombe na hirinzi
Ilahi Mola muweza	ataniafu Mwenyezi

Kwa mawazo ya mtafiti yaliyoongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayotoa fursa kwa mhakiki kuitafsiri matini kwa mujibu wa alivyoelewa. Katika mstari wa mwisho wa ubeti uliopo hapo juu, mtafiti amegundua kuwa al-anisa

Shakila amejiombea dua kwa Mola wake ili apate msaada wa kutatua matatizo ambayo yamemkabili. Hii ni baada ya kuhangaika sana kwa waganga wa makombe na hirinzi na kushindwa kupata utatuzi wa tatizo lake na alionesha moja kwa moja kuwa njia hiyo haikumsaidia kupata dawa ya matatizo yake ya mapenzi hivyo akaona ni heri anyanyue mikono kumuomba Mola Mwenyezi ili amuafu kuondokana na matatizo yaliomkabili. Vile vile mtafiti amegundua mbinu hii ya sala aina ya dua imetumiwa na msanii katika wimbo wake wa:"*Oh Rabi usinipe mapenzi"* na inaonekana katika ubeti wa kwanza na katika kiitikio cha wimbo huo kama ifuatavyo:-

Rabi sinipe mapenzi na wapendwao hakuna
Ninakuomba Mwenyezi kupendwa sitaki tena
Mapenzi ya siku hizi oooh
Mapenzi ya siku hizi watu kuhadaiana

Kiitikio
Ooh rabbi sinipe mapenzi
Ooh rabbi sinipe mapenzi
Nawapendwao hakuna
Nawapendwao hakuna

Kutokana na mawazo ya mtafiti yanayoungwa mkono na nadharia ya Mwitiko ya Msomaji inayotoa fursa kwa mhakiki kuihukumu kazi ya fasihi kulingana na ufahamu na uzoefu wake, tunaweza kusema kwamba, msanii ametumia mbinu ya dua kuomba msaada kwa Mwenyezi Mungu. Alimuomba Mwenyeezi Mungu asimjaalie kumpa mapenzi kwa sababu watu wa siku hizi hawapendeki na ndio sababu ya kusema *na wapendwao hakuna.* Hii haina maana kwamba hakuna mtu wa kumpenda bali hata ukimpenda atakuwa anakusumbua kwani hawezi kukupa pendo la dhati kama unavyompenda wewe. Ukimpenda mtu atakusumbua tu na kukupotezea muda na nguvu zako bure. Mwisho atakulipa maovu uone tabu hata

kuyazungumza mbele ya watu. Haya yanathibitishwa tena na Bi-Shakila katika ubeti wa pili (2) na wa tatu (3) anaposema:-

2. Sisemi kwa uchukivu mambo nimeshayaona
Nilitupa nyingi nguvu kwa usiku na mchana
Alinilipa maovu ooh
Alinilipa maovu hisani hakuna tena

3. Kwa dhati nilimpenda haya nilikuwa sina
Visa alivyonitenda ni fedheha kuvisema
Niliugua vidonda ooh
Niliugua vidonda sasa nimekwishapona

Maelezo ya beti hizi yanaonesha wazi ni kwa nini msanii amuombe Allah (SW) asipewe mapenzi. Hii inaonesha mateso na madhila aliyoyapata kutoka kwa mpenzi wake mpaka raha ikageuka kuwa karaha. Akafikia kuuguza vidonda na ndio akaanza kuchukiwa na tendo la kupenda na kumuomba Mwenyezi Mungu (SW) kwamba yeye na mpenzi wake waweko mbalimbali wasiwe na uhusiano wowote kwa kuogopa historia yake isije ikajirejea tena. Haya ni maoni ya mtafiti yaliyoongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji.

4.3.7.2 Apizo

Mulokozi (1996) anafafanua kwamba apizo ni ombi mahsusi linaloambatana na vitendo vya kimila vya kuitaka mizimu au miungu au Mwenyezi Mungu (SW) amwadhibu mtu fulani kwa sababu ya uovu aliomtendea muombaji. Mtafiti aliona kwamba apizo ni laana anayoiomba mtu aliekosewa, kutoka kwa Allah (S.W) kumtakia yule aliemkosea. Anatoa ombi la aina hiyo moja kwa moja iwe ni angamizo kwake ili aweze kujifunza na kupata onyo kutokana na udhaifu wake.

Katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu, mtafiti amegundua kuwa msanii Shakila ametumia mbinu hii ya sala aina ya apizo katika baadhi ya nyimbo zake zilizoteuliwa. Mfano dhahiri upo kataka wimbo wake uitwao "*Hujui alacho kuku*" katika ubeti wa tatu anaposema:

Ni wele wako mwajimbo Usojua vya thamani
Ni wele wako mwajimbo Usojua vya thamani
Kuku atazua mambo Nakuona taabani
Utakula na utumbo Kama si leo mwakani
Utakula na utumbo Kama si leo mwakani

Kwa mawazo ya mtafiti yanayotiliwa nguvu na nadharia ya Simiotiki katika msingi wake wa kiutamaduni unaoelezea kwamba yanapoainishwa maeneo, mavazi, hali au vyakula fulani katika kazi ya fasihi, vinaweza kujenga dhamira mbalimbali alizokusudia msanii kuziibua katika kazi yake na kuzifikisha katika jamii husika. Hivyo mtafiti kwa kurejelea nadharia hiyo amegundua msanii alipotumia neno "*welewako"* alikusudia kumtakia mtu laana kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Neno "*welewako"* kwa Waswahili lina maana ya kumwapiza aliyekukosea ili asirejee tena lile alilolitenda. Shakila ametumia neno hilo kumwombea maangamizi yule aliyemkosea kwani kaendelea kumwambia kuwa "*Utakula na utumbo kama si leo mwakani"* kuonesha kuwa laana itamfuata hadi siku za mbele. Anakusudia kumueleza kuwa kwa vile hatosheki na mke wake wa ndoa huenda akala na utumbo yaani akawavizia hata wale waliokharamishwa kwake kufanya nao tendo la ndoa (ambao ni dada, mama na watoto wake). Msanii anamuapiza mwenza wake kwa kumwambia atatembea na hao kama si leo mwakani. Kwa kawaida maapizo na dua zinapotakabaliwa aliepatwa husutwa na kuambiwa hayo ni malipo ya madhambi yako. Haya yanathibishwa na msanii maarufu Al- anisa Sabah Salum kutoka katika

kikundi cha Culture Musical Club kupitia wimbo wake wa fimbo ya Mungu kwenye ubeti wa tatu (3) wa wimbo huo anaposema:-

Maovu ulonitenda hapa hapa duniani
Mungu ananilipia aaa
Sinapo nilipokwenda sikukesha ugangani
Yangu nikuomba duaaa
Nikiomba zinapanda zinafika arshini
Mola anazipokeaaa
Mambo yameshakushinda fikiria kwa makini
Mungu si wa kuchezeaaa
Umebakia kuranda si mtu ni hayawani
Unachekwa na duniaaa.

Mtafiti akirejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na kutumia fursa ya kuchambua beti hii kulingana na uzoefu wake anaona kuwa pamoja na msanii kutaja neno dua katika ubeti huu wa wimbo. Dua hio iligeuka kuwa apizo lililomsababishia mlengwa kushindwa na mambo na kuchekwa na dunia. Mwisho alianza kumsimanga kwa kumwambia, *maovu ulonitenda hapa hapa duniani Mungu amenilipia bila kukesha ugangani, langu mimi ilikuwa ni kuomba dua tu.* Hivyo mbinu hii ya dua na apizo kumbe inasawiri kwa wasanii mbalimbali wa taarab asilia kama tulivyoiona kwa Shakila na Sabah Salum.

4.3.8 Matumizi ya Misimu

Wamitila (2004) anafafanua kuwa, misimu ni semi (hata maneno pia) za kimafumbo ambazo huficha maana yake na huhitaji uchunguzi kuitambua. Kimsingi, semi hizi huhusishwa na kikundi kidogo cha wanajamii na matumizi yake huwa sio rasmi. Misimu ikipata mashiko ya kutosha huingia katika msamiati rasmi. Kwa vile misimu huzaliwa, inaweza kukuwa na hatimae kufa. Misimu inayosanifiwa na kubakia katika

matumizi ya lugha hivyo hata matumizi yake yanaendelea kuwepo wakati wa uhai wake tu.

Katika uchambuzi wa data, mtafiti amegundua kuwa msanii Shakila ametumia mbinu ya misimu katika baadhi ya nyimbo zake. Ametumia misimu ili kupamba kazi yake na kuwabainisha wahusika au hadhira yake kwa kutumia lugha ambayo inalandana nao. Mfano wa msimu katika nyimbo za msanii Shakila ni ule uliogunduliwa na mtafiti katika kiitikio cha wimbo wa "*mkuna na mkunwaji*" kinachosema:-

Ngoma bila kulewa nitaichezaje mie?
Ngoma bila kulewa nitaichezaje mie?
Ngoma bila kulewa nitaichezaje mie?
Ngoma bila kulewa nitaichezaje mie?
Ningekuwa na pesa ningelewa tilatila
Ningekuwa na pesa ningelewa tilatila
Ningekuwa na pajero ningelewa tilatila
Ningekuwa na pajero ningelewa tilatila

Kwa mawazo ya mtafiti yanayoongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Neno pajero ni msimu uliozuka wakati ilipoanza kutumika noti ya Tanzania ya Shilingi mia tano. Ili vijana waoneshe tofauti yao katika matumizi ya lugha wakaiita noti hii pajero. Hata walivyoambiana wakiwa katika makundi yao, oya nipe pajero, walifahamiana kwa urahisi.

Kwa kuwa katika ubeti uiopo hapo juu, msanii Shakila amelitumia neno *pajero* akiwa na maana hio hio iliyotumiwa katika mantiki ya uwanzishwaji wa msimu huo. Hivyo tunaweza kusema kwamba dai lake ni kuwa angalikuwa na pesa angaliweza kununua ulevi wa kutosha akalewa hadi akawa hajitambui. Maneno haya yanayothibitisha kwamba neno pajero ni msimu. Matumizi ya misimu pia

yanaungwa mkono na wanatarabu asilia wa Kizanzibar kutoka katika kikundi cha Zanzibar Modern Tarab. Matumizi hayo yanajitokeza katika wimbo unaosema *Shida yako* ulioghaniwa na Omar Koppa kama unavyoonekana hapo chini:-

Shida yako pajero oo pajero
Tulia utapata utapata
Shida yako kilomberooo kilombero
Tulia utapata utapata
Kumbe wewe kumbe
Kumbe wewe kumbe
Kumbe wewe kumbe
Una wengi kumbe
Kumbe wewe kumbe
Huyawezi kumbe

Ubeti huu wa wimbo unathibitisha kuwa pajero ni msimu wenye maana ya noti ya Tanzania yenye thamani ya shilingi mia tano. Msanii alikusudia kumtuliza kila mtu mwenye tabia ya kurukaruka, akatumia msimu huu pajero kumwambia kuwa shida yako ni pajero au pesa kwa ajili ya matumizi tulia utapata. Si vizuri kuwa na tabia ya kurukaruka kwa ajili ya kutafuta pesa. Kwa kufanya hivyo mwisho wake unaweza kuwa mbaya na kukuingiza katika matatizo ya maradhi au ya kimaisha. Haya ni mawazo ya mtafiti yanayotiliwa nguvu na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inayotoa fursa kwa mtafiti kuifasiri kazi ya fasihi kwa kadri ya alivyoelewa.

4.3.9 Matumizi ya Uhamishaji wa Ndimi

Wamitila (2004) anaelezea kuwa kuhamisha ndimi ni mbinu ambayo muhusika au msemaji anatumia lugha moja tu bila kuchanganya au kuingiza maneno ya lugha nyengine. Mtafiti wa utafiti huu anaona kwamba kuchanganya ndimi ni mbinu ya kisanaa anayoitumia mtunzi wa kazi ya fasihi katika hali ya kuridhika na matumizi ya lugha moja tu pasina kuingiza neno lolote kutoka katika lugha nyengine.

Mtafiti katika kuchambua data za utafiti huu amegundua kwamba, msanii Shakila ameepuka kabisa suala la kuchanganya ndimi na badala yake ametumia mbinu ya kuhamisha ndimi ili abakie na matumizi ya Kiswahili safi cha Mwambao wa Afrika Mashariki.

Mtafiti akirejelea nadharia ya mwitiko wa msomaji na kwa kutumia ufahamu na uzoefu wake ameona kuwa, Shakila alihamisha ndimi katika nyimbo zake ili kukikuza na kukieneza Kiswahili kupitia fani yake ya uimbaji. Alikusudia kujiongezea hadhira Kwa sababu sauti yake ilisikika katika nchi zote za Waswahili na zisizokuwa za Waswahili. Alitaka kuirahisishia hadhira yake kufikiwa na ujumbe alioukusudia kwa wepesi na kwa muda mfupi zaidi. Mfano msanii Shakila alipoimba wimbo unaoitwa *Oh rabi sinipe mapenzi* alitumia Kiswahili safi na rahisi kufahamika kwa Waswahili wote kama ifuatavyo:-

Rabi sinipe mapenzi na wapendwao hakuna
Ninakuomba Mwenyezi kupendwa sitaki tena
Mapenzi ya siku hizi oooh
Mapenzi ya siku hizi watu kuhadaiana
Kiitikio
Ooh rabbi sinipe mapenzi
Ooh rabbi sinipe mapenzi
Nawapendwao hakuna
Nawapendwao hakuna

Sehemu hii ya wimbo iliyochukuliwa na mtafiti katika wimbo unaosema *Ooh rabbi sinipe mapenzi* unadhihirisha na kuthibisha ukweli wa mtafiti kuwa msanii Shakila amehamisha ndimi katika nyimbo zake zilizoteuliwa na kufanyiwa kazi. Pia Shakila alitumia mbinu hii ya kuhamisha ndimi ili kuitangaza nchi yake ya Tanzania

kiutamaduni kwa vile miongoni mwa mihimili ya nchi ni utamaduni na moja miongoni mwa kitambulisho cha utamaduni ni matumizi ya lugha.

4.3.9.1 Matumizi ya Mbinu ya Umbo la Kishairi Mapokeo

Umbo la kishairi ni sura au umbile la nje la shairi na tanzu zake. Umbo kama hilo linaweza kubainishwa kwa kutumia vipande, mishororo, beti, urari wa mizani, vina na mpangilio wake (Mulokozi, 1996:97). Mtafiti amegundua kwamba msanii Shakila amefaulu hasa kuziweka nyimbo zake katika umbo la kishairi mapokeo. Katika nyimbo takribani zote zilizoteuliwa Shakila amezibainisha kanunui hizo zilizotajwa hapo juu kama zitakavyoonekana hapo chini.

4.3.9.2 Vipande

Kipande ni sehemu ya kitu kilichokatwa kutoka katika kitu kizima. Katika dhana ya ushairi kipande ni sehemu ya mshororo wa shairi. Kwa kawaida mashairi mengi huwa na vipande viwili tu katika kila mshororo. Hata hivyo yapo mashairi mengine yenye vipande vitatu au zaidi katika mshororo mmoja (Mulokozi, 1996). Mtafiti amegundua mbinu hii ya vipande imetumiwa na msanii Shakila katika baadhi ya nyimbo zake na ameianisha kwa kutumia vipande viwili kila mshororo kama ilivyotumika katika wimbo wake wa "*mpenzi unisamehe*" ubeti wa tatu anaonesha umbo la vipande viwili kama ifuatavyo:-

1	2
Nadhani umeridhika	nilokwambia fulani
Mpenzi sitie shaka	sitakuudhi mwandani
Na mimi ninavyotaka	nisameheke moyoni

Mbinu hii ya matumizi ya vipande viwili imetumiwa na wasanii wengi katika uwanja huu wa ushairi. Miongoni mwa wasanii waliotumia mtindo huo ni Sengo (2009), kama alivyobainisha katika diwani yake ya Tungizi za Mnyagatwa. Tunayaona wazi matumizi ya mbinu hii katika shari lake la *Ujinga usiomeno* ubeti wa kwanza (1) wa shairi hili unaosema:-

1	2
Chandarua cha mzuka	ni chakula cha thamani
Wajuao kukipika	hawauzi hadigwani
Duniya duniya kaka	haina mwenye kundani
Mchoweya hujauka	akarejea ngamani
Kushikilia ubantu	ujinga usio meno

Ubeti huu wa ushairi kutoka katika diwani ya Tungizi za Mnyagatwa unadhihirisha wazi kuwa wasanii wengi hutumia mbinu hii ya vipande katika utunzi wa mashairi yao.

4.3.9.2.1 Mshororo

Sengo (2009) anafafanua kuwa mshororo katika tungo ni mstari wa maandiko, kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Mulokozi (1996: 98) anaeleza kwamba mshororo ni mstari mzima wa shairi wenye kujitosheleza kimaana. Mshororo huweza kuwa na kipande kimoja, viwili au zaidi, kuutegemea aina ya shairi. Na kwa mawazo ya mtafiti mshororo ni kila mstari mmoja katika shairi. Mtafiti amegundua kuwa msanii Shakila ametumia mbinu hii kwa ajili ya kulipamba umbo la nje la shairi katika nyimbo zake. Mshororo katika nyimbo za msanii huyu imewekwa kama inavyoonekana katika wimbo wake wa *Mpenzi unisamehe* hapo chini.

Mshororo 1: Kama kosa nimeridhi sirudii asilani
Mshororo 2: Mpenzi naomba radhi tuishi kama zamani

Mshororo 3: Adhabuyo nakubali uniadhibu mwandani

Mtafiti kwa kurejelea nadharia ya mwitiko wa msomaji amegundua uwepo wa mishororo katika nyimbo za msanii Shakila jambo ambalo limesaidia sana kuweka usawa wa mizani na kuifanya mistari hii kuwa na uwezo wa kujitosheleza. Kwa mfano mshororo wa kwanza unaosema " kama kosa nimeridhi sirudii asilani". maana yake iko wazi kwa kila mhakiki. maana ya mshororo huu ni kuwa msanii anaomba radhi kwa mpenzi wake na anakiri kosa na kuahidi kuwa hatorudia tena.

4.3.10 Ubeti

Ubeti ni idadi maalumu ya mistari iliyomo katika shairi. Mistari hiyo huwekwa kimafungu na huwa na maana kamili na uwezo mkubwa wa kutoa ishara na kuchora picha katika mambo mbalimbali aliyoyaashiria msanii katika kazi yake.

Mtafiti wa kazi hii amegundua kwamba msanii Shakila ametumia mbinu hii ya ubeti katika mashairi yake. Kila baada ya beti moja hupumzika kwa kuwapa nafasi waitikiaji wake kushadidia aliyoyasema kwa kutumia kiitikio. Pia mtafiti amegundua kuwa katika nyimbo za msanii huyu zipo zenye beti kuanzia 2 hadi 6. Tofauti ya wingi au uchache wa beti unategemea ukubwa wa dhamira iliyokusudiwa. Kwa mfano wimbo wake unaosema *Nimezama kwa mapenzi* una beti sita, beti ya sita ya wimbo huo ni hii ifuatayo:-

6. Nimezama nimezama kwenye bahari ya huba
Moyo wangu walalama nalia hitia toba
Nimezama nimezama kwenye bahari ya huba
Moyo wangu walalama nalia hitia toba
Ilahi mola karima kanepushia adhaba

Fungu hili la mistari alililoliweka msanii huyu katika wimbo uliotajwa hapo juu ndio linalojulikana kwa jina la beti au ubeti.

4.3.10.1 Vina

Wamitila (2004:218) anaeleza kuwa vina ni silabi zinazofanana na ambazo hupatikana katika sehemu moja katika mpangilio wa shairi. Mtafiti anaona kwamba vina hasa katika mashairi ya kijadi ni silabi zenye milio inayofanana na huwekwa mwishoni au katikati ya mistari. Uwekaji wa vina hutegemea aina ya shairi. Mtafiti katika uchambuzi wa data amegundua kuwa msanii Shakila ameonesha umahiri mkubwa wa kimapokeo katika matumizi ya vina. Kanuni hii ameitumia katika nyimbo zake zote zilizoteuliwa na mtafiti. Kwa mfano wimbo wake wa *Mkumwa na mkunaji* ubeti wa pili (2) unawakilisha nyimbo nyengine za Shakila katika kuthibitisha suala hili la vina.

Haya ninayoyanena msambe ni ya utani
Bali nataka bayana nami nipate baini
Mkunwaji na mkuna muona raha ni nani

Katika ubeti huu wa wimbo mtafiti amegundua ubobezi wa hali ya juu uliotumika katika utunzi wa nyimbo za msanii Shakila. umetokana na matumizi ya vina sawa vya kati ambavyo vimewekwa kwa silabi *na* kwenye miishio yote ya vipande vya mwanzo vya mishororo na ametumia silabi ni kuvifanya vina vya mwisho kuwa sawa katika mishororo yote.

4.3.10.2 Mizani

Mizani ni idadi ya harufu katika kila mshororo na kuweza kulinganisha na hisabu ya kila mshororo kuwa sawa kufuata mkondo wake (Sengo:2006). Kwa mujibu wa

Mulokozi (1996) mizani ni silabi au ni ulinganifu wa silabi katika vipande au mistari. Mtafiti amelichambua neno mizani kwa kusema kuwa ni silabi zenye kutamkika na kuleta ulingano baina ya kipande kimoja na chengine cha mstari au mshororo wa beti. Mtafiti katika kuzichambua nyimbo za Shakila na kwa kuongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amelinasa hili la matumizi ya mizani alilolifanya msanii katika nyimbo zake takriban zote jambo ambalo limekoleza uzuri na ladha ya nyimbo hizo kwa wasikilizaji wake. Ukweli wa haya unathibitika katika wimbo wake wa *kifo cha mahaba* Msanii anaposema:

1	2	3	4	5	6		1	2	3	4	5	6
Ku	fa	kwa	ma	ha	ba		ni	a	dha	bu	ka	li

Mtafiti kama alivyoonesha kukubaliana kwa mizani katika mstari huu wa beti ndivyo hivyo alivyogundua mfuatano na kukubaliana kwao katika wimbo wote wa *kifo cha mahaba.* Kila uketo umepangiliwa kwa mizani 6 na kila ukwapi umewasilishwa kwa mizani 6 na kufanya idadi ya mizani 12 katika kila mshororo uliomo katika beti hii.

4.3.11 Mbinu ya Mshonano wa Mawazo (Muundo)

Muundo mfuatano, mpangilio au mtiririko wa matukio katika kazi ya fasihi. Mtafiti anaona kwamba mfano wa muundo katika kazi ya fasihi hutegemeana na aina ya utanzu wa fasihi. Katika tamthilia muundo ni mgusano wa mambo yote katika maonesho. Katika riwaya muundo ni mpangilio wa sura kuanzia mwanzo na namna zinavyounganisha tukio moja na jengine. Ni mtiririko wa mawazo/sura moja na nyengine na kuweza kukamilisha lengo la msanii (mtunzi). Katika ushairi muundo ni mshonano wa mawazo yaliyomo baina ya beti moja na nyengine.

Mtafiti wa utafiti huu ameigundua mbinu hii ya mshonano wa mawazo katika nyimbo zote teule za Al- Anisa Shakila. Mtafiti ana lithibitisha hilo kwa kutumia mfano wa nyimbo yake moja inayojulikana kwa jina la Mpenzi unisamehe.

1. Kama kosa nimeridhi Sirudii asilani
Mpenzi naomba radhi Tuishi kama zamani
Mpenzi naomba radhi Tuishi kama zamani
Adhabuyo nakubali Uniadhibu mwandani

2. Niliyotenda kwa kweli Wala sikukusudia
Shetani kanisaili Ndipo yakatokezea
Shetani kanisaili Ndipo yakatokezea
Na sasa nimemlani Akili imenijia

3. Nadhani umeridhika Nilokwambia fulani
Mpenzi sitieshaka Sitakuudhi mwandani
Mpenzi sitieshaka Sitakuudhi mwandani
Na mimi ninavyotaka Nisameheke moyoni

Kiitikio
Mpenzi unisamehe Nirudi tena nyumbani
Mpenzi unisamehe Nirudi tena nyumbani
Nirudi tena nyumbani

Katika wimbo huu msanii anaonesha kuwa kweli alimudu kuyashona mawazo na kuyaweka katika mfumo wa kikufu chenye kuendelea na kutoa picha halisi ya utegemeano kati ya beti ya kwanza, ya pili na ya tatu, katika kukamilisha ujumbe na lengo la wimbo wote nzima. Kama tunavyoona katika wimbo huu msanii ameanza kwa kuelezea sababu hasa iliyompeleka kwa mpenzi wake. Alikwenda kwa sababu ya kumuomba radhi baada ya makosa aliyomtendea. Msanii ameonesha kwama yuko tayari kupokea adhabu ya aina yoyote kutoka kwake ili asameheke. Ubeti wa pili wa wimbo huo Bi Shakila anaeleza kwa kujitetea sababu ya kutenda kosa alilolitaja. Amefanya hivyo ili iwe ni rahisi kusameheka. Katika ubeti wa tatu wa wimbo huu msanii anahitaji kutamkiwa na mpenzi wake kuwa ameshamsamehe na anachukuwa ahadi mbele yake kuwa hatamuudhi tena baada ya kupata ridhaa ya kuwa tena

pamoja nae. Kwa hivyo Bi Shakila alizishona beti hizo tatu za wimmbo na kama angetakiwa kuelezea kwa maelezo ya kawaida angalisema: “Samahani mpenzi wangu nakuomba unisamehe japo ni kwa kunipa adhabu kwani nimekukosea ingawaje sikukusudia. Nilifanya makosa haya kwa sababu shetani kanizaini tu. Naahidi kwako mpenzi wangu kuwa sitakuudhi tena hadi mwisho wa maisha yetu”. Haya ni mawazo ya mtafiti yaliyoshibishwa na kunogeshwa kwa misingi ya nadharia ya Mwitiko wa msomaji. Kwa ujumla mtafiti amegundua kwamba msanii Shakila ni mweledi na mahiri sana katika matunzi ya fani hasa katika mbinu za kisanaa. Msanii huyu katika nyimbo zake ametumia mbinu kama vile kejeli, tashtiti, takriri, ishara, majazi, sala, misemo, methali, lugha ya kishairi na nyengine ambazo kila moja ilichukua nafasi yake katika uibuaji wa maudhui na kupendezesha. Mbinu za sanaa hizo zilizifanya nyimbo za muimbaji Shakila kuwa na mvuto unaowaleta karibu na kuwaweka tayari kwa usikilizaji na utazamaji wanachama na wapenzi wote wa taarab asilia. Pia uwezo huu wa msanii Shakila katika matumizi mazuri ya mbinu za kisanaa umempelekea kuwa na upekee unaowashangaza wengi. Matumizi ya mbinu hizo kwa msaada wa sauti yake nyororo yanamfanya kuwa tofauti na umri wake pia na mwonekano wake kwa wapenzi wa nyimbo zake. Wengi waliosikiliza mashairi yake bila kumuona, hawakuamini macho yao siku walipomuona bi - Shakila akighani mashairi yale mbele yao. Hii ni kutokana na matumizi mazuri ya mbinu za kisanaa katika nyimbo zake.

4.4 Hitimisho

Kwa kuhitimisha tunaona kuwa uchambuzi wa data za utafiti huu, uliotumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji na nadharia ya Simiotiki umesibu kuyafikia malengo

mahsusi na kupatikana kwa jawabu za maswali yote mawili zilizo kifu na kusadifu mahitaji ya lengo kuu la utafiti. Na ifuatayo ni sura ya tano iliyoelezea hitimishi, muhutasari na mapendekezo ya utafiti.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHI, MUHUTASARI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii imebeba sehemu tatu, sehemu ya kwanza inahusu hitimisho la utafiti, sehemu ya pili imebeba dhima ya kuelezea muhutasari wa utafiti na sehemu ya tatu imehitimisha kwa mapendekezo ya utafiti.

5.2 Hitimisho

Mtafiti wa utafiti huu alikusudia kutafiti dhamira na fani zilizomo katika nyimbo za taarab asilia mifano kutoka katika nyimbo za msanii Shakila Saidi. Utafiti ulikuwa wa maktabani na uliongozwa na malengo mahsusi mawili. Lengo la kwanza ilikuwa ni kuchambua dhamira katika nyimbo teule za Shakila Saidi. Lengo la pili ilikuwa ni kubainisha mbinu za kisanaa zinazojitokeza katika nyimbo za Shakila Saidi. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji. Nadharia hizi zilitoa msaada mkubwa na fursa ya kufasiri kazi za fasihi kwa kadri mtafiti alivyoiona kazi hiyo. Nadharia ya Simiotiki imemsaidia mtafiti kufumbua fumbo na fumbizi mbalimbali zilizokuwemo katika nyimbo zilizoteuliwa. Utafiti uliwasilishwa kwa njia ya maelezo na ulitumia mbinu ya usomaji makini kukusanya data. Na kumalizia kwa kuwasilisha matokeo ya utafiti yaliyoendana na malengo mahsusi ya utafiti huu.

5.3 Muhutasari wa Tasnifu

Kukamilika kwa hatua ya uchambuzi wa data, mtafiti alipata fursa ya kueleza

matokeo kulingana na mahitaji ya maswali na malengo mahsusi ya utafiti huu. Katika lengo mahsusi la kwanza, mtafiti amebainisha dhamira mbalimbali alizozigundua katika nyimbo teule za msanii Shakila. Dhamira zilizogunduliwa na Mtafiti ni mapenzi, utamaduni, usaliti, dini na imani, elimu, ukweli na uwazi, ukombozi, umalaya na dhamira nyenginezo. Kwa upande wa lengo mahsusi la pili, mtafiti aligundua mbinu mbalimbali za kisanaa zilizotumiwa na Bi Shakila katika nyimbo zake. Miongoni mwa mbinu hizo za kisanaa ni pamoja na mbinu ya kejeli, mbinu ya tashtiti, mbinu ya majazi, mbinu ya taswira na ishara, mbinu ya sala, mbinu ya takriri na mbinu nyenginezo za kisanii. Katika utafiti huu, dhamira na mbinu mbalimbali za kisanaa zimegunduliwa na mtafiti wakati wa ukusanyaji na uchambuzi wa data zilizopatikana katika vyanzo halisi vya data. Pia utafiti umegundua kuwa aliyoyasema msanii Shakila katika nyimbo zake zilizotumiwa na mtafiti wa utafiti huu yanaakisi maisha halisi ya wanajamii na ameyafikia hayo kutokana na ubobezi na umahiri mkubwa wa matumizi sahihi ya mbinu za kisanii. Mbinu alizozitumia Shakila moja kwa moja ziliibua dhamira nzito zenye kuchoma ndani ya nyoyo za waathirika wa yale yaliyogogotezwa na Shakila Said.

5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Kutokana na uchunguzi wa data uliofanywa na mtafiti wa utafiti huu, mapendekezo kwa makundi mbalimbali yametolewa:-

5.4.1 Mapendekezo ya Kitaaluma

Tafiti mpya zifanyike za kuangalia faida inayopatikana kwa kuwaenzi wasanii wa taarab asilia na kazi zao. Tafiti hizo zinapaswa kufanywa ili iwe ni sehemu za

makumbusho kwa ajili ya kizazi kilichopo na kijacho. Pia wasomi wajisogeze karibu na maktaba za taaluma ambazo kazi za fasihi kama hizi zinapatikana ili kujionea namna watafiti na waandishi watangulizi walipofikia. Waione taaluma waliyoikusanya ndani ya vitabu hivyo na kwa namna gani wataweza kuichukuwa na kuifanyia kazi.

5.4.2 Mapendekezo ya Kijamii

Jamii iwe tayari kutafuta na kuyafanyia kazi yale yaliyomo katika nyimbo za taarab asilia hasa zile za msanii Shakila ili iwe na mtazamo unaokubalika katika jamii hizo. Vilevile wanapaswa kuchunguza ili kuzibaini na kuzipiga vita nyimbo zote ambazo kwa namna moja au nyengine zinapotosha utamaduni, maadili na silka za jamii. Wanapaswa kuzibaini nakusimamia uendelezwaji wa zile nyimbo zote zenye kuadilisha na kuonesha njia ya kusonga mbele kuelekea katika wema.

5.4.3 Mapendekezo kwa Tafiti zijazo

Watafiti tarajali watupie jicho katika eneo hili la taarab asilia ndani ya nyimbo za msanii Shakila ili kuziba mwanya ambao umeachwa wazi na mtafiti wa utafiti huu. Pia watafiti hao wanapaswa wawaangalie wasanii wanaume ambao walishiriki katika uimbaji wa nyimbo za taarab asilia ili kuchunguza mchango wao kwa jamii ya Waswahili.

5.4.4 Mapendekezo kwa Wasanii

Mtafiti anawashauri wasanii wote watunge nyimbo ambazo zinadhamiria kuunganisha, kuhamasisha na kuelekeza watu katika suala zima la kujitambua na kuongeza hamu ya kupeleka mbele maendeleo ya mtu na taifa kwa ujumla.

5.4.5 Mapendekezo kwa Serikali

Waimbaji wa nyimbo za taarab asilia hasa wale wa zamani waenziwe na nyimbo zao zipewe kipaumbele. Hili lifanyike kwa sababu nyimbo za wasanii hawa ndizo zinazoendana na mila na desturi za wanajamii wa Kiswahili na mafunzo yaliyomo ndani ya nyimbo zao yana msaada kwa kila ambaye anahitaji kuendelea.

5.4.6 Mapendekezo kwa Vyombo vya Habari

Miongoni mwa dhima za vyombo vya habari ni kuipasha jamii habari zenye kuwajengea wanajamii mustakbali mzuri wa maisha na sio kuwapoteza kwa kuwapa taarifa zisizofaa. Kwa muktadha huo wanahabari wanapaswa wajipange zaidi kutumbuiza rikodi ya nyimbo zenye kuielimisha jamii na kupiga nyimbo za wasanii wakongwe ambazo zinaonekana kupotea siku hadi siku.

5.5 Hitimisho la Sura ya Tano

Sura hii imejikita na kutoa maelezo kwenye hitimishi, muhutasari wa utafiti na mapendekezo ya utafiti yaliyogusia na kuelekezwa kwa wataaluma, wanajamii, watafiti tarajali, serikali na vyombo vya habari.

MAREJELEO

Al-Farsy, A.S. (1991). *Tafsiri ya Qur-an.* Nairobi: The Islamic Foundation.

Ameir, H. (2007). Maadili yanayopatikana katika Nyimbo za ukungwi wa Zanzibar.

Barthes, R. (1994). *The Simiotic Challenges*. Califonia: Barkey University of Califonia Press.

Chimera, R. (2007). Ufundishaji wa Fasihi. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Cooper, R (1989). Language Planning and Social Change. Cambridge: Cambridge University Press.

Cresswell J. W. (2009). Research Design Qualitative, quantitative and mixed method approache. Los Angels: SAGE Publication.

Enon, J. C. (1998). Education Research Statistics and Measurement. Kampala: Makerere University Press.

Fair, L. (2013). Historia ya Jamii ya Zanzibar na Nyimbo za Siti Binti Saad.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Dar es Salaam: Nairobi Oxford University Press.

Furlong, N. (2000). *Research Method and Statistics: An Intergrated Approach.* NewYork: Hart Court College Publish

Gibbe, A. G. (1978). Fasihi na Jamii. Baadhi ya Washairi wa Kiswahili 1960 -1977. Katika Kiswahili 48/1. Dar es Salaam: TUKI.

Jilala, H. (2016). Misingi ya Fasihi Linganishi. Nadharia Mbinu na Matumizi. Dar es Salaam: Daud Publishing Company.

Kanyuma na Wenzake (2008). *Tahakiki Vitabu teule vya Fasihi*.Kidato cha 3 na 4. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Khamis (2012). Matumizi ya Mafumbo na Taswira katika Nyimbo za Mapenzi za Taarab Asilia Zanzibar: M.A.Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Khamis S. (1999). Local and Global Aspect of Taarab Popular Music Entertaiment in Africa

Khatib, M. S. (1992). Taarab Zanzibar, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House

Khatib, M. S. (2003). *Wasakatonge.* Dar es Salaam: Oxford University PressTanzania Ltd.

Kothari, S (2004). *Research Methodology, Method and Techniques (2nd).* NewDelhi: New Age International Publishers Limited.

Lyatuu, J (2011). Usawiri wa wanawake katika fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa waandishi wa kike na wakiume .Uchunguzi katika riwaya teule.Tasnifu ya M.A.Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Makilla. S. http://fitimbae Africa blogsport.com 2012/6 Taarab asilia-ni –urithi – usiopotea, html imesomwa 6/8/2017.

Manzi, Z. (2007) *Civics Manual for Secondary Schools Book Three,* Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Mbwana, H. KH . (2016). Mabadiliko ya Nyimbo za Harusi Kwenda Kasida za Harusi. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Tanzania: Dar es Salaam

Mgana, I (1996), Jukwaa la Taarab Zanzibar. Helsinki: Mradi wa Mediafrica.

Mkwera, F. M. V. (1978). *Sarufi na Fasihi. Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam TPH

Mlama, S. A. K (1996),” Utamaduni wa Mwafrika katika riwaya ya Bwana

Mnyombekere na Bibi Bogonoka,” Katika Muliko namba 23,Dar es Salaam: TUKI, kur 25– 35.

Msokile. M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi, EAEP,

Mulokozi, M.M (1996) *Fasihi ya Kiswahili* .Dar es salaam : Chuo kikuu Huria.

Mzee, A. F. (2013), Nafasi ya Maudhui katika Nyimbo za Taarab za Bishakila Zinavyosawiri Hali Halisi katika Jamii, Tasnifu ya M. A. Chuo Cha Dar es Salaam.

Ndungo, C. Y. na Wafula, R. M. (1993), *Tanzu za Fasihi Simulizi*, Nairobi: University of Nairobi.

Njogu, K. na Wafula, R M. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jommo Kenyatta Foundation.

Ponera A. S. (2014). Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi. Dar es Salaam. Karljamer Print Technology

Rajab, F. H. (2016). Chanjo ya Mapenzi katika Nyimbo za Taarab Asilia za Seif Salim. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Rayya, (2002), Song in Kiswahili Wedding: (Hakijachapishwa).

Robert, S. (2003). Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini. Nairobi: Nelson

Robert, S. (2010). Adili na Nduguze. Nairobi: Macmillani

Robson, C. (2007), How to do a research Project. A guide for Undergraduate student, Cariton Victoria: Blockwell Publisher.

Samwel, M (2010/2011) Masuala ya Kisiasa katika Mashairi ya Mapenzi ya Muziki wa Bongo Fleva: Mulika namba 29 na 30, uk 16-28. Dar es Salaam TATAKI.

Sengo, T. S. Y. M. (2007) *Utendi wa Mambo Mambo,* Dar es Salaam Mfuko wa wadhamini wa Akademiya.

Sengo, T. S. Y. M. (2015) *Diwani ya Midulu,* Dar es Salaam Mfuko wa wadhamini wa Akademiya.

Sengo, T. S. Y. M. (2006) *Tungizi za Mnyagatwa,* Dar es Salaam, AL – AMIN Educationaly and Research Academy

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam KAUTTU LTD

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam Press and Publicity Centre

Starehe, (2016) Mwandishi wa habari: Gazeti la Mwananchi, Mahojiano kati yake na Bi Shakila Saidi. Chalinze 15/05/2016.

TAKILUKI, (2001) *Malenga Wapya,* Dar es Salaam: Oxford University Press.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. (Toleo la 2) Nairobi. Oxford University Press

Wamitila K. W. (2004) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*, Nairobi: Focus Publication Limited.

Wamitila K. W. (2002), Uhakiki Wa Fasihi Misingi Na Vipengele Vyake, Nairobi, Phoenix

Wazir, M. (2015). Nyimbo za Singo katika Kijiji cha Uzini. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Tanzania: Dar es Salaam

Yego, A (2011), Nafasi ya Mwanamke: Jinsi inavyotetewa katika Nyimbo za Taarab za Zanzibar, Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

VIAMBATANISHO

1. PAZIA

i) Mwenzangu ungeniambia yantue akilini
Ulo nunua pazia kutundika mlangoni
Mwenzangu ungeniambia yantue akilini
Ulo nunua pazia kutundika mlangoni
Mimi naifikiria faidae siioni
Mimi naifikiria faidae siioni

ii) Kama ingempokea mgeni mwenye imani
Kama ingempokea mgeni mwenye imani
Kisha likamkemea fedhuli na hayawani
Kisha likamkemea fedhuli na hayawani
Nami nge inunua nikaweka mlangoni
Nami nge inunua nikaweka mlangoni

iii) 3. Bwana ingetokea mfano kenda dukani
Nyuma akaja ingia mgeni hadi chumbani
Bwana ingetokea mfano kenda dukani
Nyuma akaja ingia mgeni hadi chumbani
Pazia ikamwambia kwamba kaja fulani
Pazia ikamwambia kwamba kaja Fulani

iv) 4. Mimi sitoininua pazia ya mlangoni
Hasara ikaingia kuifua kwa sabuni
Mimi sitoininua pazia ya mlangoni
Hasara ikaingia kuifua kwa sabuni
Tena yatia uzia iwambapo mlangoni
Tena yatia uzia iwambapo mlangoni

KIITIKIO
Haina kinga pazia hata iwe ya thamani
Heri nunua kofia hifadhi ya utosini
Ikusitiri kwa jua ikusitiri kwa jua
Lisikuchome kichwani
Ikusitiri kwa jua ikusitiri kwa jua
Lisikuchome kichwani

2. ALOANZA PEKE PEKE

1. Aloanza peke peke Kugombanisha viumbe
Sasa yuko peke yake kasimama kila pembe
Aloanza peke peke Kugombanisha viumbe
Sasa yuko peke yake kasimama kila pembe

Kamaliza hila zake hazifai hata chembe
Kamaliza hila zake hazifai hata chembe

2. Alitaka kututenga kutueka mbali mbali
Shabaha aloilenga Mungu hakuikubali
Alitaka kututenga kutueka mbali mbali
Shabaha aloilenga Mungu hakuikubali
Mambo yameshamtinga
Mambo yameshamtinga
Mambo yameshamtinga kavurugika akili
Mambo yameshamtinga kavurugika akili

3. Ndugu yangu jitulize bure unahangaika
Yakweli nikueleze viumbe wanakucheka
Ndugu yangu jitulize bure unahangaika
Yakweli nikueleze viumbe wanakucheka
Wewe utaondoaje
Wewe utaondoaje
Wewe utaondoaje Mungu alichokiweka
Wewe utaondoaje Mungu alichokiweka

4. Bure unatuchukia Hututoki midomoni
Fitina kututilia Majumbani na kazini
Bure unatuchukia Hututoki midomoni
Fitina kututilia Majumbani na kazini
Hayo ulotutendea
Hayo ulotutendea
Hayo ulotutendea yote tumeyabaini
Hayo ulotutendea yote tumeyabaini

KIITIKIO

Aloanza peke peke Kugombanisha viumbe
Sasa yuko peke yake kasimama kila pembe
Aloanza peke peke Kugombanisha viumbe
Sasa yuko peke yake kasimama kila pembe
Kamaliza hila zake hazifai hata chembe
Kamaliza hila zake hazifai hata chembe

3. MAPENZI YAMEPUNGUA

1. Mapenzi yamepungua mimi nimeshayaona
Kila nikiyachungua Hakwishi kuoneana
Kheri nipate pumua Kwako sina haja tena

2. Ulipokuwa na pendo Na ikawa twapendana
Hukuwa navyo vishindo Wala hatukupigana
Umebadilika mwendo Ni kheri tukaachana

3. Duniani wengi wako Wapenzi kila namna
Usidhani peke yako Uzuri unapitana
Sina haja pendo lako Dunia hii ni pana

4. Duniani wengi wako Wapenzi kila namna
Usidhani peke yako Uzuri unapitana
Sina haja pendo lako Dunia hii ni pana

KIITIKIO

Mapenzi yamepungua Mimi nimeshayaona
Kila nikiyachungua Hakwishi kuoneana
Hakwishi kuoneana Mapenzi yamepungua

4. SASAMBU

Mamie mwari sokaue Sokaue mgeni kangia
Mamie mwari sokaue Sokaue mgeni kangia
Mgeni wangu wee Aaee kaue mgeni kangia
Mgeni na ndimwa Aaee kaue mgeni kangia
Mgeni na kapu Aaee kaue mgeni kangia
Mgeni na sembe Aaee kaue mgeni kangia

Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore Aaee
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore Aaee
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nataka nsomore nsomore ndembo yangu
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro Aaee
Nakupa nsomore usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro Aaee
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako

Nakupa nsomoro usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro Aaee
Nakupa nsomore usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro Aaee
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako

Nakupa nsomoro usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako
Nakupa nsomoro usomore ndembo yako

Sasambu sasambu Aee
Sasambue sasambu sasambu sasambura nkurore
Sasambu sasambu Aee
Sasambu sasambu sasambura nkuror
Jamani sasambu Sasambura nkuro
Ameileta baba Sasambura nkurore

Sasambu sasambu Aee
Sasambue sasambu sasambu sasambura nkurore
Sasambu sasambu Aee
Sasambu sasambu sasambura nkurore
Mwaiona sasambu Sasambura nkurore
Ameileta baba Sasambura nkurore
Kamletea mkewe Sasambura nkurore
Kanga amemtilia Sasambura nkurore
Zipatazo ishirini Sasambura nkurore
Sabuni za kuogea Sasambura nkurore
Nyingi zisizo kifani Sasambura nkurore
Na nyingi za kufulia Sasambura nkurore
Na za kupaka usoni Sasambura nkurore
Kanzu amemshonea Sasambura nkurore
Na viatu vya thamani Sasambura nkurore
Kihanjifu sidiria Sasambura nkurore
Na nguo zake za ndani Sasambura nkurore
Hakuna kilobakia Sasambura nkurore
Pete bangili na cheni Sasambura nkurore
Sasambu Aeee
Sasambue sasambu sasambu Sasambura nkurore
Sasambu Sasambu Aee
Sasambu sasambu Sasambura nkurore
Sasambu sasambu Aee
Sasambu Sasambura nkurore
Jamani sasambu Sasambura nkuroreeee

5. HUJUI ALACHO KUKU

Hujui alacho kuku usinge mpa mgeni
Hujui alacho kuku usinge mpa mgeni
Wala kufanya shauku kumsifu hadharani
Hebu zunguka kwa huku umtizame jaani
Hebu zunguka kwa huku umtizame jaani

Kama kuku yuna hadhi kufishwa mahadharani
Kama kuku yuna hadhi kufishwa mahadharani
Mbona kichwa hukiridhi kukitia mchuzini
Umekieka baadhi atae kula ni nani
Umekieka baadhi mlaji kichwa ni nani

Ni wele wako mwajimbo usojua vya thamani
Ni wele wako mwajimbo usojua vya thamani
Kuku atazua mambo na kuona taabani
Utakula na utumbo kama si leo mwakani
Utakula na utumbo kama si leo mwakani
Kisikuhadae kiga kwa mnofu na laini
Kisikuhadae kiga kwa mnofu na laini
Akili ukavuruga ukawania fukani
Ola kidari na bega nyama imahala gani
Ola kidari na bega nyama imahala gani

KIITIKIO

Kuku yunahadhi gani mgeni kukirimiwa
Kuku yunahadhi gani mgeni kukirimiwa

6. MAPENZI NI KAMA DONDA

1. Nimechoka vumilia leo nawapasulia
   Nimechoka vumilia leo nawapasulia
   Imekuwa siku hizi kila siku ninalia
   Imekuwa siku hizi kila siku ninalia
   Nanyi hamuniulizi kipi ninacholilia
   Kwani hamuniulizi kipi ninacholilia

2. Ni kama donda mapenzi leo nawaelezea
   Ni kama donda mapenzi leo nawaelezea
   Waweza funga pumzi kuzimu ukaingia
   Waweza funga pumzi kuzimu ukaingia
   Wala hayana mjuzi yoyote humwelemea
   Wala hayana mjuzi yoyote humwelemea

3. Nimempenda Fulani jina sitowatajia
   Nimempenda Fulani jina sitowatajia
   Alikuwa msikizi kila ninalomwambia
   Alikuwa msikizi kila ninalomwambia
   Kisha ni mtimizi yote nno hitajia
   Alikuwa mtimizi yote nno hitajia

KIITIKIO

Mapenzi ni kama donda yaingiapo moyoni

Nimechoka kuvumilia leo nawapasuliwa
Mapenzi ni kama donda yaingiapo moyoni
Nimechoka kuvumilia leo nawapasuliwa

7. AKUKATAAE HAKWAMBII TOKA

1. Akukataae hakwambii tokaa
Akukataae hakwambii tokaa
Akukataae hakwambii tokaae
Akukataae hakwambii tokaa
Huona mamboe yamebadilika
Huona mamboe yamebadilika
Waweza ukae huwezi ondokaaa
Waweza ukae huwezi ondokaaa
Waweza ukae huwezi ondokaaa
Waweza ukae huwezi ondokaaa

KIITIKIO
Huwezi ondoka
Huwezi ondoka
Huwezi ondoka
Huwezi ondoka
Waweza ukae huwezi ondoka
Waweza ukae huwezi ondoka
Waweza ukae huwezi ondoka
Waweza ukae huwezi ondoka

2. Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Nipende kwa dhati au nikatae
Usinidhihaki la kweli nambie
Usinidhihaki la kweli nambie
Kama hunitaki kheri nitulie mimi
Kama hunitaki kheri nitulie
Kama hunitaki kheri nitulie kwangu
Kama hunitaki kheri nitulie

KIITIKIO
Kheri nitulie
Kheri nitulie
Kheri nitulie
Kheri nitulie
Kama hunitaki kheri nitulie
Kama hunitaki kheri nitulie
Kama hunitaki kheri nitulie

Kama hunitaki kheri nitulie

3. Watu hutendana zaidi ya hayo
Watu hutendana zaidi ya hayo
Watu hutendana zaidi ya hayo
Watu hutendana zaidi ya hayo
Wakatukanana kupita mifano
Wakatukanana kupita mifano
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno

KIITIKIO
yakesha maneno
yakesha maneno
yakesha maneno
yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno
Mwisho hupatana yakesha maneno

8. NIMEZAMA KWA MAPENZI

1. Nimezama kwa mapenzi
Sijui kama tazuka
Nimezama kwa mapenzi
Sijui kama tazuka
Naiona yangu hali Mimi nimedhofika
Mimi nimedhofika

KIITIKIO
Nimezama kwa mapenzi
Sijui kama tazuka
2. Wenzangu nawauliza nini dawa ya mapenzi
Waganga nimemaliza wa makombe na hirinzi
Wenzangu nawauliza nini dawa ya mapenzi
Waganga nimemalizawa makombe na hirinzi
Ilahi Mola muweza ataniafu
Mwenyezi

KIITIKIO

Nimezama kwa mapenzi
Sijui kama tazuka

Nimezama kwa mapenzi sijui kama tatoka
Kujikwamua siwezi taabani nateseka
Nimezama kwa mapenzi sijui kama tatoka
Kujikwamua siwezi taabani nateseka
Ilahi Mwenyezi ataniafu rabuka

KIITIKIO

Nimezama kwa mapenzi
Sijui kama tazuka
Nimezama nimezama mwenzenu katika kina
Nimebaki natizama lakutenda sina tena
Nimezama nimezama mwenzenu katika kina
Nimebaki natizama lakutenda sina tena
Ilahi Mola karima ataniafu rabana

KIITIKIO

Nimezama kwa mapenzi
Sijui kama tazuka

Nimezama nimezama katika kina kirefu
Kila nikijitizama moyoni Napata hofu
Nimezama nimezama katika kina kirefu
Kila nikijitizama moyoni Napata hofu
Ilahi Mola karima ndie mwenye kuniafu

KIITIKIO

Nimezama kwa mapenzi
Sijui kama tazuka
Nimezama nimezama kwenye bahari ya huba
Moyo wangu walalama nalia hitia toba
Nimezama nimezama kwenye bahari ya huba
Moyo wangu walalama nalia hitia toba
Ilahi Mola karima kanepushia adhaba

KIITIKIO

Nimezama kwa mapenzi
Sijui kama tazuka
Naiona yangu hali mimi nimedhofika
mimi nimedhofika

KIITIKIO

Nimezama kwa mapenzi
Sijui kama tazuka
Nimezama kwa mapenzi
Sijui kama tazuka
Nimezama kwa mapenzi
Sijui kama tazuka

9. KUKU NA YAI

1. Nawauliza nisai Marijali mukiweza
Nawauliza nisai Marijali mukiweza

Hivi sasa niko hoi Moja linanitatiza
Hivi sasa niko hoi Moja linanitatiza
Kati ya kuku na yai Ni kipi kilichoanza
Kati ya kuku na yai Ni kipi kilichoanza

2. Kama lilianza yai kuku akafuatia
Kama lilianza yai kuku akafuatia
Nani alitaga yai Hata kuku kutokea
Nani alitaga yai Hata kuku kutokea
Ukampata uhai Maisha kufurahia
Ukampata uhai Maisha kufurahia

3. Endepo kaanza kuku Kuwapo kwenye dunia
Endepo kaanza kuku Kuwapo kwenye dunia
Wapi alitoka kuku Kama yai halikuwa
Wapi alitoka kuku Kama yai halikuwa
Ikampata shauku Vyakula kuvidonoa
Ikampata shauku Vyakula kuvidonoa

4. Nyama ya kuku ni tamu Kula nikinywa bikai
Nyama ya kuku ni tamu Kula nikinywa bikai
Yai halinishi hamu Huila nikinywa chai
Yai halinishi hamu Huila nikinywa chai
Lakini sikifahamu kilianza kitu gani
Lakini sikifahamu kilianza kitu gani

KIITIKIO

Nawauliza wahenga Wabara na visiwani
Nawauliza wahenga Wabara na visiwani
Wahenga na manyakanga Jawabu nipatieni
Wahenga na manyakanga Jawabu nipatieni
Kuku yai na mvinga Hasa kimeanza nini
Kuku yai na mvinga Hasa kimeanza nini

10. MPENZI UNISAMEHE

1. Kama kosa nimeridhi Sirudii asilani
Mpenzi naomba radhi Tuishi kama zamani
Mpenzi naomba radhi Tuishi kama zamani
Adhabuyo nakubali Uniadhibu mwandani

2. Niliyotenda kwa kweli Wala sikukusudia
Shetani kanisaili Ndipo yakatokezea
Shetani kanisaili Ndipo yakatokezea
Na sasa nimemlani Akili imenijia

3. Nadhani umeridhika Nilokwambia fulani
Mpenzi sitieshaka Sitakuudhi mwandani
Mpenzi sitieshaka Sitakuudhi mwandani
Na mimi ninavyotaka Nisameheke moyoni

KIITIKIO

Mpenzi unisamehe Nirudi tena nyumbani
Mpenzi unisamehe Nirudi tena nyumbani
Nirudi tena nyumbani

11. MACHO YANACHEKA

1. Macho yanacheka Moyo unalia
Macho yanacheka Moyo unalia
Macho yanacheka Moyo unalia
Macho yanacheka Moyo unalia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Nikimkumbuka wangu maridhia
Chozihunitoka kwa zake tabia
Chozihunitoka kwa zake tabia
Chozihunitoka kwa zake tabia
Chozihunitoka kwa zake tabia

2. Nenda nateseka nalia na njia
Nenda nateseka nalia na njia
Nenda nateseka nalia na njia
Nenda nateseka nalia na njia
Siku zitafika kukugeukia
Siku zitafika kukugeukia
Siku zitafika kukugeukia
Siku zitafika kukugeukia
Wajahangaika ulie na njia
Wajahangaika ulie na njia
Wajahangaika ulie na njia
Wajahangaika ulie na njia

3. Uwache dhihaka mpenzi sikia
Uwache dhihaka mpenzi sikia
Uwache dhihaka mpenzi sikia

Uwache dhihaka mpenzi sikia
Moyo waniwaka kweli nakwambia
Moyo waniwaka kweli nakwambia
Moyo waniwaka kweli nakwambia
Moyo waniwaka kweli nakwambia
Wanipa mashaka kwa zako tabia
Wanipa mashaka kwa zako tabia
Wanipa mashaka kwa zako tabia
Wanipa mashaka kwa zako tabia

Hauna kiitikio

12. KIFO CHA MAHABA

1. Kifo cha mahaba Kina idhilali
Hakina haiba Wala afadhali
Kifo cha mahaba Kina idhilali
Hakina haiba Wala afadhali
Hakina haiba Wala afadhali
Bali tajikaba Nifilie mbali
Bali tajikaba Nifilie mbali
Bali tajikaba Nifilie mbali
Nifilie mbali
2. Kufa kwa mahaba Ni adhabu kali
Leo ni msiba Usio mithali
Kesho ni adhaba Mbele ya jalali
3. Ewe mahabuba Niepushe hili
Ni wewe twabiba Hapana wa pili
Tapanda jaziba Tajiuwa kweli

13. MKUNA NA MKUNAJI

1. Kwambizana ni umbuji Ni ada tangu zamani
Nna jambo nataraji Nami nipate baini
Mkuna na mkunwaji Muona raha ni nani
2. Haya ninayoyanena Msambe ni ya utani
Bali nataka bayana Nami nipate baini
Mkunwaji na mkuna Muona raha ni nani
3. Tulizeni waungwana Wa bara hadi wa wani
Munipe jbu la maana lenye vina na mizani
Mkunwaji na mkuna Muona raha ni nani
4. Kwambizana ni umbuji Ndio kiwanaadamu
Nina jambo nataraji Nami nipatefahamu
Mkuna na mkunwaji Muona raha ni nani
5. Yaosha niliyonena Kuwajuza wahisani

Nataka jibu la maana nami nipateebaini
Mkunwaji na mkuna Muona raha ni nani
Kimalizio
Ngoma bila kulewa nitaichezaje mie
Ningekuwa na pesa ningelewa tila tia
Ningekuwa na pajero ningelewa tila tia

14. OH RABBI SINIPE MAPENZI

1. Rabi sinipe mapenzi Nawapendwao hakuna
Ninakuomba mwenyezi kupendwa sitaki tena
Mapenzi ya siku hizi
Mapenzi ya siku hizi Watu kuhadaiana
2. Sisemi kwa uchukivu Mambo nimeshayaona
Nilitupa nyingi nguvu kwa usiku na mchana
Alinilipa maovu oooh
Alinilipa maovu Hisani hakuna tena
3. Kwa dhati nilimpenda Haya nilikuwa sina
Visa alivyonitenda Ni fedheha kuvinena
Niliugua vidonda oooh
Niliugua vidonda sasa vimekwishapona
3. Simsahau milele kila ninapomuona
Nakumbuka vile vile Yalopita mwaka jana
Mimi na kiumbe yule oooh
Mimi na kiumbe yule Naapa sirudi tena

KIITIKIO

Oh rabbi sinipe mapenzi
Oh rabbi sinipe mapenzi
Nawapendwao hakuna
Nawapendwao hakuna

15. VIVA FRELIMO

1) Leo twakuvika taji mpendwa baba Samora
Kukomboa msumbiji sijambo la masikhara
Mreno kafa maji hivi sasa kadorora

2) Msumbiji kukomboka sisi twaona fakhari
Fakhari ya Afrika kwenye bara na bahari
Samora unaposhika waondoe mabepari

3) Umeleta uhuru ni ushindi wa maana
Wareno na makaburu hawajitambui tena
Mungu atawanusuru mashujaa waungwana

4) Tanzania imara sisi tumeshajiwe
Kwenye bahari na bara tuko tayari kushika
Tutawanyoa vipara kwa harubu na shabuka
KIITIKIO

Viva Frelimo, Viva Samora, Viva Msumbiji
Viva Tanzania, Viva Nyerere.